

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Nane – Tarehe 25 Machi, 2015

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mtaona kuna hitilafu Order Paper, mashine imechelewesha kwa hiyo nadhani mtapata katika dakika mbili zijazo. Wagawieni kwanza waliokaa na wengine watapata baadaye.

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Vincent J. Nyerere, atauliza swali la kwanza.

Na. 80

Fedha Zilizotengwa kwa Ajili ya Maafa

MHE. VINCENT J. NYERERE aliuliza:-

Kila mwaka Serikali imekuwa ikitenga fedha za maafa.

Je, ni kiasi gani cha fedha hutengwa kwa Mkoa wa mara?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vincent J. Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuataavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya kukabili maafa mbalimbali nchini na kuzihifadhi katika Mfuko wa Maafa uliopo Benki Kuu ya Tanzania (BoT). kwa kuwa, tukio la maafa haliwezi kutabirika, Serikali huwa haitengi fedha kimko bali hutoa kiasi cha fedha kinachohitajika pale maafa yanapotokea.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012/2013 Wilaya za Musoma Vijijini, Ranya na Bunda katika Mkoa wa Mara zilikumbwa na uhaba wa chakula kutokana na ukame. Ili kukabiliana na hali hiyo, Serikali ilitoa jumla ya tani 2,436.1 za Mahindi ambapo tani 332.9 zenye thamani ya shilingi 189,753,000/= zilitolewa bure kwa wananchi wasiokuwa na uwezo wa kununua na tani 2,192.66 zenye thamani ya shilingi 1,249,782,000/= ziliuzwa kwa bei yenye punguzo (subsidized price) ya shilingi 50,000 kwa tani badala ya shilingi 570,000 kwa tani. Jumla ya shilingi 370,936,170/= zilitolewa kusafirisha chakula hicho.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013/2014 Mkoa wa Mara ulipewa tani 1,266 za Mahindi ambapo ni tani 127 zenyе thamani ya shilingi 72,390,000/= zilitolewa bure kwa familia zisizokuwa na uwezo wa tani 1,139 zenyе thamani ya shilingi 649,230,000/= ziliuzwa kwa bei yenye punguzo ya shilingi 50,000/= badala ya shilingi 570,000/= kwa tani. Kiasi cha shilingi 198,453,225.6 zilitumika kusafirisha chakula hicho kwenda Halmashauri zilizokuwa na mahitaji ya chakula Mkoani Mara.

Aidha, Serikali ilitoa jumla ya shingi 49,500,000/= kwa lengo la kurekebisha miundombinu iliyoharibika kutokana na mvua zilizonyesha katika Wilaya ya Serengeti mwezi Machi/Aprili, 2013.

MHE. VINCENT J. NYERERE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mbali na ubadhifuru katika misaada bado kumekuwa na ugawaji wa misaada kwa misingi ya itikadi. Ni nini tamko la Serikali?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vincent Nyerere, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto ambazo zimekuwa zikijitokeza katika suala zima la uratibu na *management* ya kuhudumia waathirika katika maafa mbalimbali nchini.

Kwa kuona tatizo hilo limekuwa kubwa ndiyo maana mwaka huu na katika mkutano huu wa Bunge Serikali imeamua kuleta Muswada mpya ili kutunga sheria sasa itakayoweza kuratibu na kusimamia *management* yote ya maafa nchini ili kuondoa matatizo yote yaliyokuwa yakijitokeza kutokana na namna moja ama nyingine katika kushughulikia suala zima la maafa nchini.

MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, nina swali moja la nyongeza.

Kwanza nianze kwa kuishukuru Serikali kwa kuleta sheria mpya, lakini dalili zote kwa sasa zinaonyesha kwamba kutakuwa na uhaba wa chakula na huko nyuma uzoefu unaonyesha kwamba chakula kinapelekwa wakati tayari njaa imeshaingia na inapelekwa kwa takwimu ambazo ni za nyuma.

Kwa hiyo, chakula kinachopelekwa kinafika mahali kwamba wananchi wengine wameshakuwa na njaa kali. Kikipelekwa inaonekana tunawagawa wananchi, kuna wanaopata na kuna wanaokosa. Mwaka huu Serikali inatuahidi nini kwamba chakula kitapelekwa kwa wakati na hasa ukizingatia kwamba dalili zinaonyesha kutakuwa na uhaba wa chakula?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Shekifu kwa swali la nyongeza.

Napenda kujibu swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, tumeshagundua na kuona kwamba kunaweza kuwa na dalili ya njaa katika maeneo mengi nchini Tanzania, naomba nichukue nafasi hii kuwaagiza viongozi wote wa Mikoa, Wilaya na Halmashauri kuanza kufanya tathmini ya kina katika

Nakala ya Mtandao (Online Document)

maeneo yao na hivyo basi tathmini hizo zifike kwenye ofisi zetu zinazohusika mapema ili kuanza kuinga kabla ya kutibu muda ambaa utakuwa labda umeshachelewa kufanya kazi hiyo ya kuwahudumia Watanzania ili wasipate tatizo la njaa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kumekuwa na tabia ya kuchelewa kupeleka huduma kwa wahanga wa maafa yanayotokea na dalili zinaonyesha kwamba mvua ambazo zinaendelea kunyesha hivi sasa ndani ya nchi yetu kuna uwezekano wa kutokea mafuriko na kwa sababu mafuriko hayo tayari yameshaanza kujitokeza katika maeneo mbalimbali kama Dar es Salaam maeneo ya Mnyamani na kadhalika. Na muda mrefu hivi sasa ni kwamba Serikali mmekuwa mkituahidi kwamba mtapeleka vifaa vile mmejidhatiti na kujipanga vizuri kuhakikisha kwamba vifaa wakati wowote wa mafuriko watu wataweza kuokolewa bila tatizo lolote.

Ni nini kauli ya Serikali juu ya kuwaokoa watu ambaa watapata mafuriko katika maeneo ya Tanzania nzima?

SPIKA: Wewe omba Mungu yasitokee. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, majibu!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Masoud kama ifuatavyo:-

Ni kweli kabisa nchi yetu kutokana na mabadiliko ya tabia nchi, hali ya hewa, shughuli za kilimo, kiuchumi na kijamii majanga haya ya mafuriko yamekuwa yakitokea katika maeneo tofauti na kwa namna tofauti.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itajitahidi kufanya kila linalowezekana ili kuhakikisha kwamba kila eneo ambalo linapata matatizo basi Serikali iweze kusaidia.

Lakini nitoe wito kwa wananchi na Watanzania wote kwa ujumla, suala la maafa si suala la Serikali peke yake bali kila mdau na Mtanzania yeoyote atakayeguswa na tatizo la maafa basi tushirikiane kwa pamja ili kuhakikisha kwamba tunawenza kusaidiana katika majanga mbalimbali ambayo yanatokea katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile baada ya kuona upungufu uliyopo katika sheria ya zamani ambayo ilikuwa inasistiza katika suala la kugawa misaada wakati wa maafa, Sheria mpya imeweka sasa utaratibu wa kuhakikisha tunatathmini, tunachukua tahadhari na kinga kabla ya maafa na yanapotoka tunashughulika na baada ya maafa kutokea tunarejesha hali ya kawaida katika hali ya kawaida katika maeneo yaliyopata maafa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawashukuru sana Wabunge kwa kuipitisha sheria ile sasa mipango ya maafa itawekwa katika mipango ya Maendeleo ya Taifa.

SPIKA: Baada ya Rais kusaini hiyo sheria, bado haijasainiwa. Tuendelee na swali linalofuata Mheshimiwa Alhaji Mohamed Missanga, kwa niaba yake Mheshimiwa Diana Chilolo.

Matengenezo ya Daraja la Minyughe Tarafa ya Ihanja

MHE. DIANA M. CHILOLO (K.n.y. MHE. MOHAMED H. MISSANGA) aliuliza:-

Uongozi wa Wilaya ya Ikungi pamoja na Mbunge wa Jimbo wamekuwa wakiombwa Serikali mara kwa mara kusaidia katika ujenzi wa daraja la Minyaghe Tarafa ya Ihanja bila kupatiwa majibu.

(a) Je, Serikali imefikia wapi juu ya ombi hilo?

(b) Je, Serikali haioni kuwa inawaumiza wananchi wa maeneo hayo kimaendeleo na kiuchumi kwani wakati wa masika hushindwa kusafiri kutokana na ubovu wa daraja hilo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YAS WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga, Mbunge wa Singida Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, daraja jipya la Mtavira linalotegemea kujengwa katika Tarafa ya Ihanja lipo katika Barabara ya Minyughe – Mtavira ambayo lina urefu wa kilomita 20. Serikali kwa mwaka wa Fedha 2014/2015 imeidhinishia Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi fedha kiasi cha shilingi 776.3 wa ajili ya ujenzi wa daraja hili. Fedha hizi mpaka sasa hivi hazijapokelewa.

Hata hivyo, Halmashauri ilitangaza zabuni ya kumtafuta Mhandisi Mshauri wa kusanifu daraja hili kupitia gazeti la Mwananchi la tarehe 31 Oktoba, 2014 ambapo makampuni manne yalijitokeza kununua nyaraka za zabuni. Zabuni zilifunguliwa tarehe 29 Januari, 2015 na tathmini inategemea kufanyika muda wowote.

(b) Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa katika sehemu (a) ya jibu hili, tayari Serikali ipo katika hatua za mwisho za kujenga daraja hilo na kuwaondolea adha ya usafiri wananchi wa maeneo hayo. Vile vile, Serikali imeidhinisha fedha kiasi cha shilingi 210,940,000/= kwa ajili ya matengenezo ya barabara na vivuko katika barabara ya Minyughe Mtavira.

Fedha zote zimepokelewa. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 180.9 zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa drift 3 na kalavati 15 na shilingi milioni 30.0 zimetumika kwa ajili ya matengenezo ya kawaida ya barabara kilomita 12. Mkandarasi anayetekeleza mradi huu ni Victoria wa Mjini Singida kwa mkatabata wa shilingi milioni 206.5. Mkandarasi amelipwa shilingi milioni 100.00 kwa ajili ya kazi hiyo.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwanza, kwa kuwa, fedha hizi zimeshapelekwa na upembuzi yakinifu umeshafanyika.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Je, Serikali inaweza ikasema ni muda gani utatumika kuhakikisha ujenzi wa barabara hii umekamilika ili wananchi wa maeneo hayo ambao wengi wao wamepoteza kwa kushindwa kuvuka mto huo mkubwa wanapokuwa na mgonjwa mahututi?

Tujue muda wa kuanza na kukamilika, najua Serikali inafahamu tathmini ya namna hiyo.

Pili, kwa kuwa pia katika Mkoa wa Singida Mheshimiwa Rais aliahidi kutengeneza barabara kwa kiwango cha lami, barabara ya kutoka Singida Mjini kwenda Iliongo na kwenye utaratibu wa kukamilisha ahadi hii ilikuwa ni mwaka wa fedha 2014/2015, mwaka huu sasa unakwisha na miaka mitano inaisha. Je, wananchi wa eneo hilo tuwaambie nini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, naomba muwe mnauliza maswali kwa kifupi ili kusudi tuwe na waulizaji maswali wengi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Singida, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii kama nilivyoleza ni kwamba inafanyiwa kazi sasa hivi tunavyozungumza na kama anavyosema Mheshimiwa Diana Chilolo ni kweli barabara hii ni muhimu sana kwa sababu inaunganisha Mkoa wa Singida na Tabora na wananchi na wafanyakishara wanaitegemea kwani wanalima vizuri sana kule, wanafanya kazi nzuri lakini kazi yote ile itakuwa ni kazi bure kama hii barabara itakuwa haikukamilika.

Hapa kinachogomba sasa ni hizo shilingi milioni 771 ambazo hizo nakiri kwamba hazijaenda, awamu ya kwanza tumepeleka shilingi milioni 380 na fedha hizi zinaendelea kwenda kwa sababu tunawasiliana na wenzetu wa Hazina na hizi fedha ni za Road Fund.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa ya Bunge lako Tukufu kwa kawaada ukiangalia trend na pattern ya mapato yanayotokana na road fund, about 90% -100%zinapatikana. Kwa hiyo, hizi fedha zitakopokuwa zimepatikana hapa kazi hii itakuwa imekwisha. Najua kwamba Mheshimiwa anataka nitamke hapa ni kwa wakati gani na wakati gani itakuwa imekamilika. Naomba aniamini, tunaposema kwamba kazi yote hii itafanya.

Pili, anazungumzia kuhusu barabara ambayo Mheshimiwa Rais aliahidi, Rais akiahidi jambo kwetu sisi kama Wizara ni sheria yaani hakuna mdahalo hapo. Hatuwezi kukaa hapa tunaanza ku-debate kwamba itakuwaje na kadhalika. Sisi maelekezo tuliyonayo ni kwamba shughuli zote na ahadi zote zilizotolewa na Rais zitatekelezwa kama ilivyokuwa imeelezwa na mmemsikia Mheshimiwa Rais mwenyewe mimi namsikia anasema anajitahidi kwa kila njia kuhakikisha kwamba ahadi zote alizotoa zinakamilika. (Makofii)

SPIKA: Mheshimiwa Christowaja Mtinda.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mimi swali langu la nyongeza lipo katika majibu ya msingi au majibu ya nyongeza katika barabara ya kutoka Singida Mjini mpaka Mgungira ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri amesema Rais akitoa ahadi ni sheria tayari.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba barabara hiyo imepewa angalizo lakini swali langu ni kwamba hiyo barabara pamoja na kwamba sasa hivi tunasubiri pesa ili iweze kutengenezwa katika kiwango cha lami kila mwaka imekuwa ikitengewa fedha na Halmashauri kwa ajili ya kuitengeneza ili wananchi waweze kupita kutoka Singida Mjini mpaka maeneo mengine ya Sepuka na Mgongila.

Mheshimiwa Spika, lakini Wakandarasi wanaoitengeneza barabara hii wao wanaitengeneza chini ya kiwango, mpaka sasa hivi ninavyozungumza ni mashimo matupu badala ya kutumia dakika 20 kutoka Sepuka mpaka Singida Mjini unatumia masaa mawili.

Sasa je, Serikali inasemaje kuhusu Mkandarasi huyo ambaye hafanyi kazi yake sawasawa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Christowaja Mtinda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mimi nitai-follow up na tutaifuatilia hii barabara anayoisema kwa sababu anataka kauli ya Serikali.

Mkandarasi akienda pale Halmashauri za kwetu kama tulivyokuwa tunaeleza jana uwezo wake ni mdogo sana, Mkandarasi akienda anajenga barabara chini ya kiwango, sisi tunakwenda kwa Contractors Registration Board na kwenda kumshitaki na kumwambia kwamba huyu amekwenda katika Halmashauri ya Singida amechukua fedha halafu anatujengea barabara ambayo iko chini ya kiwango.

Mheshimiwa Spika, sisi tutatuma watu wetu waende wakakague hiyo barabara lakini cha kwanza ni kwamba retention ya pesa yoyote ambayo haijalipwa hapa tutakwenda kuizua. Mimi nataka nijue mazingira mazuri ambayo yamejitokeza hapa.

Lakini kama anachosema na sina haja ya kum-doubt Mbunge anachozungumza hapa, tutakwenda kuikagua hiyo barabara na kama tukikuta iko chini ya kiwango tutampeleka Mkandarasi mpaka kwenye mamlaka zinazohusika. Kwanza tunam-charge engineer wetu aliyeo Singida kwamba alikuwa wapi wakati barabara inatengenezwa chini ya kiwango na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri alikuwa anafanya nini katika jambo hilo. Hayo ndiyo ambayo tunaweza tukasema hapa.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka nikuambie kwamba tutaifuatilia.

SPIKA: Ahsante sana, ilikuwa ni swali la nyongeza tu, Mheshimiwa Ezekia D. Wenje, atauliza swali hilo na kwa niaba yake Mheshimiwa Susan Lyimo.

Na. 82

Kuchangia Ujenzi wa Maabara

MHE. SUSAN A. J. LYIMO (K.n.y. MHE. EZEKIA D. WENJE) aliuliza:-

Serikali imekuwa ikikusanya kodi mbalimbali kutoka kwa wananchi kwa njia mbalimbali na lengo kuu la kukusanya kodi hiyo ni ili kuwafikishia wananchi huduma mbalimbali za kijamii ikiwemo elimu bora.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Je, kwa nini Serikali inawalazimisha wananchi, wafanyakazi na wafanyabiashara kuchangia ujenzi wa Maabara, huku wakilipa kodi inayopaswa kufanya shughuli hizo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel Dibogo Wenje, Mbunge wa Nyamagana, kama ifuatavyo:-

Mheshimwia Spika, ujenzi wa miundombinu ya shule nchini umekuwa unatekelezwa kwa ubia kati ya Serikali, wanachi na wadau wa Maendeleo. Wakati wa ujenzi wa shule nyingi za Kata baadhi ya miundombinu muhimu ikiwemo maabara haikukamilika. Kutokana na umuhimu wa maabara katika Shule za Sekondari, Halmashauri zote nchini ziliagizwa kukamilisha miundombinu hii ili kuimarisha utoaji wa Elimu ya Sekondari nchini.

Mheshimwia Spika, katika maeneo mbalimbali ikiwemo katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza, wananchi wamekuwa wanashirikishwa kuitia mikutano na vikao kuanzia ngazi za mtaa ili waone umuhimu wa kushiriki kwa hiari katika ukamilishaji wa ujenzi wa maabara.

Halmashauri ya Jiji la Mwanza, imetumia shilingi bilioni 1.2 (1,217,800,000.00) kukamilisha ujenzi wa Maabara 13 na 68 zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Serikali kuitia Halmashauri ya Jiji la Mwanza imechangia shilingi milioni 960, wananchi shilingi milioni 217 na Mheshimiwa Mbunge shilingi milioni 40.8 kuitia mfuko wa Jimbo.

Mheshimwia Spika, hatua hii ya kuwashirikisha wananchi inawafanya wawe sehemu ya utekelezaji wa shughuli za Maendeleo, waweze kuimiliki Miradi husina na kuongeza kasi ya mafanikio. Kuitia Mbunge na wananchi wote nchini kwa kuitikia wito wa Serikali kutekeleza shughuli hii muhimu ya ujenzi wa maabara. Wito kwa Wakurugenzi wote ni kuhakikisha kuwa uhamasishaji unafanyika bila kutumia nguvu kuwashirikisha wananchi.

Inatekelezwa kwa ubia kati ya Serikali, wananchi na wadau wa maendeleo wakati wa ujenzi wa shule nyingi za Kata baadhi ya Miundombinu muhimu ikiwemo maabara hazikukamilika, kutokana na umuhimu wa maabara katika shule za sekondari, Halmashauri zote nchini ziliagizwa kukamilisha miundombinu hii ili kuimarisha utoaji wa elimu ya sekondari nchini kote.

Katika maeneo mbalimbali ikiwemo Halmashauri ya Jiji la Mwanza, wananchi wamekuwa wanashirikishwa kuitia mikutano na vikao kuanzia ngazi ya Mtaa ili waone umuhimu wa kushiriki kwa hiari katika ukamilishaji wa ujenzi wa maabara. Halmashauri ya Jiji la Mwanza imetumia shilingi bilioni 1.2 kukamilisha ujenzi wa maabara 13 na maabara 18 ziko katika hatua mbalimbali za ujenzi.

Serikali kuitia Halmashauri ya Jiji la Mwanza imechangia shilingi milioni 960, wananchi wamechangia shilingi milioni 217 na Mheshimiwa Mbunge Wenje amechangia shilingi milioni 40.8 kuitia Mfuko wa Jimbo. Hatua hii ya kuwashirikisha wananchi inawafanya wawe ni sehemu ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo, waweze kuimiliki miradi husika na kuongeza kasi ya mafanikio.

Pia kuitia Bunge lako Tukufu ninapenda kuwapongeza sana wananchi wa Nyamagana, Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote nchini kwa kuitikia wito wa Serikali kutekeleza shughuli hii ya ujenzi wa maabara.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, wito kwa Wakurugenzi wote nchini ni kuhakikisha kuwa uhamasishaji ufanyike bila ya kutumia nguvu, kuwashirikisha wananchi kwenye shughuli hii. (Makofi)

MHE. SUSAN J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana na ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake ni kweli kwamba maabara ni jambo la msingi sana katika elimu hususani kwa watoto wetu wa sekondari lakini Mheshimiwa Spika, ninatambua kwamba agizo la Mheshimiwa Rais limetekelezwa kwa kiasi kikubwa lakini cha kushangaza nilitaka Serikali ituambie ni nani aliruhusu fedha katika Halmashauri karibu zote nchini zitumike kujenga maabara wakati tayari tulishapitisha Bajeti ya Serikali Kuu?

Swali la pili, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri anasema kwamba michango ni hiari, lakini tuna taarifa ya Mafisa Elimu mbalimbali nchini ambao waliwaandikia walimu barua za kukatwa mishahara yao kwa ajili ya kujenga maabara. Ni sawa na kuwaambia madaktari wajenge hospitali na Wabunge tujenge jengo la Bunge.

Je, ni kwa nini walimu ambao wanateseka sana, hawapati mishahara yao kwa wakati, walimu hawa hawa wanalazimishwa kuchangia maabara?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Susan Lyimo kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza ni suala la ujenzi wa maabara nchini kote lilipoagizwa ilikuwa ni jukumu la Halamshauri yenyewe kutafuta vyanzo mbalimbali nya kukamilisha shughuli hiyo ikiwemo na kushirikisha wananchi kama ambavyo nimeeleza kwenye jibu la msingi la ujenzi wa miundombinu ya shule, hujengwa kwa ubia kati ya Serikali, wananchi na wadau.

Suala la Halmashauri kuchukua fedha zilizokuwa kwenye Bajeti hilo sasa tutapata taarifa kutoka Halmashauri zenyewe. Lakini kubwa zaidi ni kwamba Halmashauri zenyewe zina mapato yake ya ndani ambayo pia zingweza kutumia mapato ya ndani kuweza kufanya kazi hiyo.

Matumizi yote ya Halmashauri ya Fedha kwenye Halmashauri yanaidhinishwa na Baraza la Madiwani kuititia Baraza lao, wakifanya maamuzi yao wao wenyewe hilo ni jukumu lao wao wenyewe. (Makofi)

Swali la pili, swali la kulazimishwa kama ambavyo nimeeleza kwenye jibu la msingi inawezekana pia ziko Halmashauri hazikufanya vizuri kwa kulazimisha watu kufanya kazi hii. Lakini agizo hili lilipotolewa ilikuwa ni lazima Halmashauri kuititia mpango wa kila Halmashauri kutekeleza kwa utaratibu wao wenyewe ikiwemo kuelimisha wananchi umuhimu wa kuchangia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo pia ambayo watumishi wamechangia kwa kuelimishwa lakini siyo walimu peke yao. Kwa hiyo, maeneo mbalimbali yamefanya kazi hiyo.

Kwa mfano Nyamagana, Nyamagana Mkurugenzi wa Jiji kuititia vikao aliita Watumishi wote kuhamasisha kuchangia, lakini pia imetokea hata walimu wenyewe hawakuridhia kwa sababu ilikuwa ni hiari na hakuna aliyewalazimisha na hawakuchangia. Kwa hiyo, mambo haya yameendelea katika Halmashauri zote nchini. (Makofi)

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, ninajua moja ya kutaka kuendeleza kiwango cha elimu ya sekondari ni pamoja na ujenzi wa maabara, lakini pia ni kuhakikisha hata wanafunzi pia wanapata vyakula katika shule za msingi na sekondari. Lakini hivi tunavyoongea

Nakala ya Mtandao (Online Document)

wakandarasi wanao supply vyakula shuleni inasemekana hawajalipwa kwa Mkoa wa Mara peke yake ambao wanaidai Serikali karibia bilioni mbili(2).

Sasa nilitaka kujua ni lini Serikali itawalipa watu hawa kwa sababu wengi wamekopa mikopo benki wanashindwa kurejesha hizo fedha kwa sababu hamjawalipa hizo fedha za kusambaza vyakula mashulen.

SPIKA: Usinifundishe kufanya kazi, swali hilo Mheshimiwa Ester Bulaya, kweli wewe mwenyewe unafikiri lina justify ukweli wenyewe?

Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkoo, kwa sababu linahusu watoto naomba ujibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa shule zetu za sekondari za Bweni zote zinahudumiwa chakula na Serikali na katika uendeshaji huu kupitia wazabuni nikiri kuwa yapo madeni ambayo wazabuni wetu wanadai kwenye maeneo haya. Tulishafanya uhakiki nchi nzima tumepata viwango tunavyotakiwa kulipia na tayari Hazina kwa mara ya mwisho mwezi wa Januari, mwaka huu (2015) tulishapeleka fedha kwenye Halmashauri ili kupunguza madeni haya.

Madeni yaliyobaki, Hazina inaendelea kuratibu na kupeleka fedha hizi kwenye shule zetu kupitia Wakurugenzi ili tuweze kuwalipa watoa huduma wetu waweze kuendelea kutoa huduma hiyo ya kutoa huduma hiyo ya kutoa chakula mashauleni.

Tunachosisitiza hapa ni kwamba tunahitaji matumizi ya pamoja, Mkoo wa shule na chini ya usimamizi wa Wakurugenzi na Wazabuni ili bei zinazotumika kununua vyakula hivi ziwe ni halisia ili tuweze kupunguza mrundikano wa madeni makubwa kwenye shule zetu na kupelekea huduma hii kutotolewa ipasavyo.

Na. 83

Barabara ya Kutoka Liwale Hadi Mahenge Kupitia Kijiji cha Ndapata

MHE. FATMA ABDALLAH MIKIDADI (K.n.y. FAITH M. MITAMBO) aliuliza:-

Barabara ya kutoka liwale kwenda Mahenge kupitia Kijiji cha Ndapata na Selous Game Reserve ni kiungo kikubwa katika Lindi na Mtwara.

Je, Serikali inasema nini juu ya kufungua na kujenga barabara hiyo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Liwale hadi Mahenge kupitia Kijiji cha Ndapata ina umbali wa kilomita 525.1 katika ya umbali huo kilomita 75.1 kutoka Liwale Mjini hadi Ndapata ambazo haziko ndani ya Hifadhi zinahudumiwa na Halamshauri ya Wilaya ya Liwale.

Sehemu inayobaki ambayo ni kilomita 450 zimo ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Selous Game Reserve katika Bajeti ya Mwaka 2014/2015 Halmashauri ya Wilaya ya Liwale ilitengewa shilingi milioni 99.5 kwa ajili ya matengenezo ya muda maalum.

Kati ya hizo fedha zilizopokelewa ni shhilingi milioni 55.4 ambazo zimetumika kufanya matengenezo umbali wa kilomita 5 kwa kuweka changarawe na ujenzi wa kalvati moja.

Vilevile katika mwaka wa fedha 2015/2016 Halmashauri imetenga shilingi milioni 119 kwa ajili ya matengenezo ya muda maalum sehemu korofii, kalvati na matengenezo ya kawaida ili kuifanya ipitike kwa muda wote.

Mheshimiwa Spika, sehemu iliyobaki ambayo ni kilomita 450 ziko ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Seleous kwa mantiki hiyo Serikali haiwezi kuendeleza ujenzi katika sehemu hiyo ya barabara kwa sababu eneo hilo linasimamiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii chini ya Sheria ya Hifadhi ya Barabara, kwa sababu eneo hilo linasimamiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii chini ya Sheria ya uhifadhi wa wanyama pori ya mwaka 2009 ambayo inazuia barabara kujengwa katika hifadhi za wanyama pori kutokana na athari kwa wanyama hao.

MHE. FATMA ABDALLAH MIKIDADI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninataka kusema tu kwamba sehemu kubwa ya Wilaya ya Liwale ina pori kubwa la Seleou Game Reserve na tukiachia barabara zote zinazotembea katika Hifadhi ya wanayama pori ya Selous Game Reserve kwa kweli tutakuwa hatuna maendeleo.

Sasa inabidi Sheria hii ya Wanayamapor ya mwaka 2009 ambayo huzuia barabara kujengwa katika Hifadhi za wanayama pori kutokana na athari kwa wanayama hao irekebishwe. Kwa mfano hapa kilomita 450 hazijengwi kwa sababu ya Hifadhi ya Wanayamapor.

Kwa hiyo, tunataka tuambiwe ni Sheria hizi ziangaliwe upya ili barabara hizi ziweze kujengwa ili kuleta maendeleo katika Mkoa wa Lindi kupiria Selous Game Reserve.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, hapa sasa mimi hapa nitatafuta mgogoro ambaa sitauweza. Hapa Mheshimiwa Nyalandu, akisikia mimi ninajibu hili wakati mimi ni sehemu ya Serikali. Nimehangaini hapa, nimewaita watu wa Liwale, nimezungumza na Kaimu Mkurugenzi, nimemtafuta Mkuu wa Mkoo nikawaambia hivi kuna mahali popote mewahi kuzungumzia hii barabara? Wananiambia sisi ndiyo tunaisikia hiyo barabara.

Yaani nimehaha nayo nimekaa nimefukuza vijana wangu wote pale ofisini nikawaambia ninataka mniambie hii habari mmeizungumza wapi?

Kilomita hizi ninazozisema ndizo hizo ninazozisema kwamba ziko chini ya Halmashauri hizo 475 kuzitolea kauli hapa mimi nitachukua swali hili la Mheshimiwa Fatma Mikidadi, nimpelekee Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, nimwambie Wabunge wanashauri kuwa hii habari hii tuangalie jinsi ya kuitisha barabara Selous Game Reserve ili waitafakari wote kwa pamoja tuone kama hili jambo linawezekana.

Mheshimiwa Spika, mimi kimoja ambacho ninakifahamu ni kwamba katika Wizara ambayo ina contribute katika Government Revenue ambayo inaongoza ni hii Wizara tunayoizungumza hapa na imeweza kufanya hivyo kwa sababu tumejiwekea masharti wenyewe ya kuhakikisha kuwa tusizivuruge mbuga za wanyama.

The moment unaruhusu watu wanakatisha mle ndani mnaona hakuna utalii. Habari imekwisha Mheshimiwa Fatma Mikidadi, ninakuheshimu sana Mama yangu tena ninakuheshimu sana hili jambo mimi ninaomba usinitie majoribuni, nitampelekea Nyalandu aende akaangalie mwenyewe kule halafu alipeleke huko kunakohusika.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI: Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza. Barabara hii ya Liwale inafanana na barabara ya Rufiji ambayo inatoka Ikwiriri - Mkongo, inakwenda Mloka inapita Selous Game Reserve na barabara hii inapitisha watalii wengi sana.

Lakini matengenezo yake yamekuwa yakisuasua sana na kila mwaka kwenye Bajeti ninaiona Wizara ya Ujenzi inapitisha pesa na barabara hii inasimamiwa na ngazi ya Mkoa lakini matengenezo yake yamekuwa yakisuasua na pesa nyingi zinatengwa na hata wiki iliyopita barabara iko katika hali mbaya sana.

Je Serikali inasema nini juu ya barabara hii ya Vikumbulu – Mloka – Mkongo hadi Ikwiriri?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli, kama ifuatavyo:-

Samahani Mheshimiwa Kuruthumu ni kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, unajua maswali haya yanakuja ghafla.

SPIKA: Endelea sawa tumekuelewa wewe jibu tu swali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Sijasikia unachosema.

SPIKA: Ninasema jibu tu swali tumekuelewa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, ninachosema ni kwamba hii barabara iko chini ya Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa John Pombe Magufuli, iko chini ya Wizara ya Ujenzi halafu hii nayo inasemekana inapita huko huko kwenye Hifadhi hiyo hiyo unaona tatizo linapokuja hapa?

Kwa hiyo, mimi ninayachukua yote haya ya Mheshimiwa Fatuma Mikidadi na Mheshimiwa Kuruthum nitakwenda kuzunguza na Mamlaka zinazohusika mimi hapa siingizi mdomo wangu, wala siingizi maneno hapa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu italeta matatizo makubwa hapa. Ninaomba nilichukue Mheshimiwa Kuruthum tutalishughulikia kwa misingi hiyo.

SPIKA: Leo akina Mama wamekupa majaribu, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Silvestry Francis Koka.

Na. 84

Huduma za Zimamoto

MHE. SILVESTRY F. KOKA aliuliza:-

Huduma za Zimamoto ni muhimu sana sana kwa wananchi hasa Mijini kutokana na mpangilio wa makazi na shughuli zao za biashara:-

Je, ni upi utaratibu wa kumpa mwananchi huduma hiyo muhimu?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Utaratibu wa upatikanaji wa huduma hii kwa wananchi ni kwa Jeshi la Zimamoto kupata taarifa ya moto kupitia njia mbalimbali ikiwemo miito ya dharura kwa kutumia namba ya dharura 114. Namba hiyo hupatikana kwa kutumia mitandao yote hapa nchini na bila gharama.

Pia namba hiyo iko wazi kwa ajili ya utoaji wa huduma hii saa 24. Namba hii mara ipigwapo huingia mara moja katika kituo cha karibu cha Zimamoto ama katika Ofisi ya Mkoa husika.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Zimamoto na Ukoaji katika kutambua umuhimu wa huduma hii kwa wananchi limeshamiri kupunguza matukio ya moto kwa kutoa elimu, tihadhari na kinga za zimamoto kwa wananchi kupitia maonyesho na kupitia vyombo vya habari kama vile television na kwenda mashuleni ili kufundisha somo la moto.

Elimu hii imekuwa ikitolewa kwenye mikusanyiko ya watu wengi hasa kwenye masoko, Jeshi limeendelea kutoa elimu ya vitendo kwa wananchi kwa kuonyesha mazoezi hai ya kuzima moto kwa kutumia vifaa vya huduma ya kwanza ya kuzima moto na kuwashauri wananchi juu ya kifaa sahihi cha kuweka pindi itokeapo dharura katika makazi yao.

MHE. SILVESTRY F. KOKA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali ninayo maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo. Mnamo tarehe 11 Novemba, 2014 ulizuka moto katika shule ya Sekondari ya Philbert Bayi na kwa takribani masaa zaidi ya matatu na nusu huduma hii iliombwa na haikuweza kupatikana. Matokeo yake mabweni yaliteketea na hasara ya takribani milioni 800 ilipatikana.

Lakini pamoja na hilo tarehe 8 Novemba, 2014 mwezi huo huo moto ulizuka Maili Moja pale Mjini Kibaha na maduka takribani 10 yakiwepo pamoja na nla Ndugu Khalafan Mwembamba, Ali Gonzo, Adam Mwasha, Mohammed Katundi, Ulisha Kisusa, Hamza Kassim, Mikidadi na Zainab yote yaliungua na kuteketea na inakadiriwa ni hasara ya zaidi ya shilingi milioni 600.

Mheshimiwa Spika, jitihada za kupata huduma hii zilifanyika ikiwa ni pamoja na mimi mwenyewe kupiga simu lakini ilichukua zaidi ya saa tatu na nusu ndipo gari lilipokuja gari la Zimamoto jambo ambalo liliwapa wananchi hasira hata kudiriki kutupia magari haya mawe. Sasa maswali.

Swali la kwanza, huduma ilikuwa inapatikana katika Halmashauri na ilikuwa ni rahisi kufikia na sasa inapatikana Wizarani ni kwa nini huduma hii isirudi Halmashauri ili wananchi waweze kuipata kirahisi ikiwa ni pamoja na kupeleka huduma karibu na wananchi?

Swali la pili, kuna tozo kwa ajili ya moto na tozo hii inalipwa na wafanyabiashara wote na watu wote kwenye taasisi mbalimbali zinazotoa huduma.

Mfano shule ya Philbert Bayi inalipa hadi shilingi milioni 800 kwa mwaka, lakini wafanyabiashara wanalipa kadi ya shilingi 70,000/= hadi 100,000/= ni kwa nini wafanyabiashara hawa au wananchi hawa waendelee kulipa fedha hizi wakati huduma hii ni duni na mara nyingi hata wakihitaji wataambiwa ni bovu fedha hizi zinakwenda wapi?

Ninaomba Serikali itoe majibu ambayo yataridhisha wananchi kwa tozo hii.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri na Waheshimiwa Wabunge, ninaomba maswali yenu yawe mafupi jamani mnachukua muda mwangi sana mpaka sasa tupo swali la tano tu na muda umepita.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Francis Koka Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza ametaja matukio ambayo yametokea mwezi wa Novemba, 2014 (mwaka jana) kwenye shule ya Philbert Bayi na maduka maili moja jibu sasa la nini kilitokea siku hizi mbili sina.

Lakini kwa kawaida inapotokea dharura kama hii ni kupiga simu hiyo ambayo nimeisema na gari ambalo mimi ninajua Kibaha kuna gari ambalo lina uwezo wa lita 4,000. Sasa kuchukua masaa matatu na nusu sijaelewa lakini gari Kibaha lipo.

Sasa kuchukua masaa matatu na nusu sijaelewa, lakini gari Kibaha lipo na halitakiwi moto ukitokea Kibaha lichukue muda wote huo. Mimi pia nitalifuatilia nione kwa nini masaa matatu na nusu Kibaha gari lisifike. Lakini tunalo gari na hakuna sababu ye yeyote lichukue muda huo.

Ninatoa pole kwa wakazi wa Kibaha kwa hili lilitokea lakini mimi nitalifuatilia nione kwa nini tulichelewa kupeleka huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu tozo, tozo imewekwa kisheria na kifungu cha 32 (g) cha sheria ya Zimamoto kimesema kwamba kutakuwa na tozo kwa ajili ya *inspection*. Lakini pia na kutoa maarifa kuhusu moto, kujikinga na pale utakapotokea tufanye nini. Hii tozo ni ya kisheria.

Kwanza sikubaliani kwamba kuna mtu mmoja anaweza akatoa milioni mia nane kuhusu tozo hii, kwa sababu hakuna uwezekano wa mfanyabiashara kulipa milioni mia nane. Ukubwa wa tozo hii umeanza na elfu kumi na kwa biashara kubwa sana ambayo nafikiri ipo Kibaha ni shilingi milioni kumi.

MHE. HAMAD ALI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninashukuru kupata nafasi, nina swali moja la nyongeza.

Kumekuwa na tabia kwa baadhi ya wananchi wasiowaaminifu kupiga simu au kutoa taarifa zisizo na ukweli kwa maafisa wa Zimamoto jambo ambalo linapelekeea hasara kubwa na kwamba Maafisa wa Zimamoto wamekuwa wakilalamikia sana jambo hili, nini mkakati wa Serikali katika kulikomesha jambo hili? Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba baadhi yetu Watanzania ustaarabu wetu unatupelekeea kupiga simu hii kwamba kuna moto na wakati hakuna na inawezekana vitendo hivi ni sehemu ya matukio hata ukipiga kuna moto kweli gari linachelewa. Ninawasihi Watanzania na kwa kuitia kwa Wabunge wao, hili jambo siyo la kuchezza, kusema kuna hatari na hakuna, kuna siku kunaweza kukawa na hatari na usipate msaada.

Jambo tunalolifanya ni kwamba sasa hivi tunaweza tukazi-track namba za simu ambazo zinatumika kwa ajili hii na tayari tunajipanga ili tuchukue hatua kwa sababu hili jambo linaweza likaiunguza Tanzania nzima wakati tukijzoesha tu kwamba kunaweza katika miito minne, miwili ya uwongo basi tunaweza tukapata tatizo. (Makofii)

Na. 85

Utoaji wa Faini za Papo kwa Papo kwa Makosa ya Barabarani

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA aliuliza:-

Askari wa barabarani hutoza faini za makosa ya barabarani za papo kwa papo yaani notification na inasemekana kuwa Askari hawa hupangiwa kiwango cha kukusanya na kukiwakilisha kwa Viongozi wao na kwa sababu hiyo, Askari hawa hujali zaidi kukusanya fedha zaidi kuliko kusimamia sheria za barabarani:-

Je, Serikali inasema nini juu ya jambo hilo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda nijibu swali la Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sheria ya Usalama Barabarani Namba 67 ya Mwaka 1973 inatoa Mamlaka kwa Askari wa Usalama Barabarani kutoza faini za papo kwa papo kwa makosa mbalimbali ya usalama barabarani. Hili ni moja ya jukumu la msingi la kikosi cha Usalama Barabarani unaolenga kuimarisha usimamizi wa sheria ya usalama barabarani. Ukamataji wa makosa ya barabarani na faini ya papo kwa papo hulenga kuwatia hofu ya adhabu madereva wakorofi hivyo kuwafanya wafuate Sheria na Kanuni za usalama na kupelekea kupunguza ajali za barabarani.

Mheshimiwa Spika, hakuna kiwango cha pesa ambacho Askari wa Usalama barabarani wanapangiwa kukusanya kupeleka kwa Viongozi wao. Askari wameelekezwa kukamata makosa kwa wingi iwezekanavyo hususani makosa hatarishi kama vile mwendo kasi, ulevi, ujazaji abiria na mizigo, uendeshaji wa hatari na kadhalika.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Dereva anapokamatwa na kutozwa faini ya papo kwa papo, lakini pia anaruhusiwa kuondoka. Kwa mfano unapomkamata mtu mwenye basi amejaza abiria wengi halafu ukamtoza faini, halafu ukamruhusu kuondoka na mbele ya safari anaenda kupata ajali.

Je, faini hizi ni kweli zinasaidia kuondoa ajali za barabarani?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Madereva wanapokamatwa na wakatozwa faini za papo kwa papo wakawa hawana fedha magari yao hushikiliwa. Lakini sheria ya barabarani inatamka wazi kwamba huyo dereva anaweza kulipa faini hiyo katika siku 28.

Je, katika siku 28 ni kwanini sasa Askari wa Usalama wa Barabarani wanashikilia magari?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, faini ambazo zinatozwa za malipo ya papo kwa papo zinatakiwa zipunguze ajali, kwa sababu kabla hujambo wa utozwe pesa utaoneshwa kosa lako na utaelekezwa kwamba ulirekebishe. Kama ni ulevi wewe mwenyewe huwezi kupewa nafasi ya kuondoka. Kwa hiyo, katika uchunguzi ambao tumeufanya tozo hizi zinasaidia na ninafikiri ni jambo ambalo tumelikubali pamoja na Bunge lako Tukufu. Ninafikiri tuendelee kuzitumia kwa sababu zina manufaa kwa kupunguza ajali.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kwamba kinachotolewa barabarani ni *notification* ya kuwa umefanya kosa, umekamatwa na kosa na ile *notification* ina nakala, dereva anapewa moja. Dereva ambaye anaweza akaichukua *notification* na kufikisha malipo yale kama inavyotakiwa hana tatizo. Lakini kuna baadhi ya mambo ambayo ni lazima kama gari lina ubovu ambao hauwezi kuondosheka. Kwa kweli inabidi Askari alidhibiti au kama Askari amelewa hawezi akaendesha kama Dereva ni lazima Askari alidhibiti hata kama amempa *notification*.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mimi naomba kuuliza swali dogo tu la nyongeza, kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Waziri Waziri wa Mambo ya Ndani, katika majibu yake ya awali umesema kwamba askari wa barabarani wanaangalia makosa hasa ya mwendo kasi. Lakini Naibu Waziri tunapenda a fahamu wale askari wenye vitochi ni kero barabarani na ndiyo wa kwanza kupokea rushwa hasa zisizokuwa za msingi.

Katika Bunge lililopita ultuahidi wazi kwamba mko tayari kuleta zana za kisasa ambazo zitaonesha namba ya gari ambalo limeenda kasi na watu waliomo ndani. Lakini kwa sasa hivi mnawenza mkawa gari sita zote mkasimamishwa kwa pamoja na zote mkaoneshwa speed moja hiyo hiyo.

Je, ni lini sasa mtatuletea zile tochi zenyenye viwango zinazoweza kuonesha namba za gari ili kuondoa usumbuwa wa askari wa barabarani?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, Serikali wala Jeshi la Polisi halitaki kuwaudhi wananchi bila sababu. Fikra za kufikiri kwamba Askari ambaye yupo barabarani na tochi ni kero nafikiri tuziondoe kwa sababu wale wapo pale kwa ajili ya kuokoa maisha yetu.

Watanzania tuone kwamba tunakerwa ili tusife. Mimi ninajua kwamba tunapata ajali nydingi na ajali zote tulizonazo Wabunge zinahusiana hasa na mwendo kasi. Kama mtu kasimama na tochi unasema anakukera ili ufe baada ya kilomita mbili mimi sielewi.

Mheshimiwa Spika, naomba tuwakubali hawa Askari wanajitahidi kuokoa maisha yetu na Serikali inawaajiri inawalipa, inatafuta hivyo vifaa siyo kwa sababu tuwakere, tunataka muwe na raha. Lakini pia tunataka maisha yenu yaendelee ili raha hii muitumie siku nydingi. (Makofiki/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tunaboresha kamera ambazo tunazo, kamera ambazo tulikuwa nazo mwanzo ilikuwa inaonesha speed tu na dereva ni rahisi kusema kwamba hii haikuwa gari yangu.

Lakini sasa tuna baadhi ya kamera ambazo tumezipata tayari zinaonesha pia namba ya gari. Tunachotaka tufanye zaidi siyo kumweka huyo Askari ambaye anakera tutaweka kamera

wala hutaiona na itakuarifu tu kwamba jana ulikwenda haraka na utozwe kiasi fulani. Kama hilo litaridhisha. (Makofi)

Na. 86

Uhifadhi wa Majengo ya Kale

MHE. NAMELOK E. SOKOINE aliuliza:-

Uhifadhi wa majengo ya zamani ya kihistoria ni kumbukumbu kwa vizazi vijavyo na ni urithi kwa Taifa letu. Mfano jengo la Salamander lililojengwa Mwaka 1901 lakini limebomolewa:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuyahifadhi majengo yote ya zamani kwani ndiyo yanayohifadhi historia?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri kumbe walipozungumzia barabara za utalii na wewe ulikuwepo?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Namelok Edward Sokoine, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uhifadhi wa majengo ya kihistoria unasimamiwa na sera ya malikale ya mwaka 2008 na sheria ya Mambo ya Kale ya Mwaka 1964 na marekebisho yake ya Mwaka 1979. Sera na sheria hizi zinaainisha sifa na vigezo vya majengo vya kuhifadhiwa na kuwa kumbukumbu ya Taifa.

Jengo linalokidhi vigezo hivyo hutangazwa katika gazeti la Serikali. Uhifadhi wa majengo ya zamani una faida nyingi zikiwemo hifadhi ya historia ya Taifa ya leo, kuwa kuvutio cha utalii na pia huonesha teknolojia ilivyokuwa kipindi fulani cha ukuaji wa Mji. Vile vile hutumika kama sehemu ya mafunzo kwa kada mbalimbali na huboresha mandhari ya miji na eneo husika.

Mheshimiwa Spika, napenda ieleteke kuwa siyo majengo yote ya zamani yapo katika orodha ya urithi au utamaduni wa Taifa. Orodha hii inajumuisha majengo yaliyotangazwa na gazeti la Serikali katika Jiji la Dar es Salaam majengo na maeneo 28 yametangazwa kama maeneo ya kihistoria katika Tangazo la Serikali Na. 498 la Mwaka 1995 na Wizara inawajibika nayo katika usimamizi na uendelezaji wake kwa kushirikiana na wamiliki na wadau wengine.

Hivyo, jengo la Salamander halikuwa katika orodha ya urithi wa utamaduni wa Taifa, hivyo wamiliki wake walikuwa na mamlaka ya kulibomoa au kubadilisha matumizi yake vile wapendavyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kuhakiki orodha ya majengo yote yenye umuhimu mkubwa kihistoria nchini ili yaweze kutambuliwa kisheria na kutangazwa katika Gazeti la Serikali kwa kushirikiana na wadau wanaomiliki majengo hayo.

Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kuhifadhi majengo ya kihistoria.

Mheshimiwa Spika, Wizara inashirikiana na Jumuiya ya Ulaya kuanzisha Kituo cha Uhifadhi wa Majengo ya Kihistoria katika Jiji la Dar es Salaam (*Dar es Salaam Centre for Architectural Heritage*).

Wizara inatoa wito kwa mamlaka za mijii hapa nchini zione sifa ya kuwa na majengo ya kihistoria, kuyatunza kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo na kuyatumia kama vivutio vya utalii kama tunavyoona katika nchi nyininge.

MHE. NAMELOK E. SOKOINE: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza:-

Kwa kuwa, katika jibu lake la swali la msingi linasema kwamba Serikali imesema jengo la Salamanda lilivunjwa kwa sababu lilikuwa halimikiwi na Serikali.

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya kuuzwa kwa Posta ya Kwanza Tanganyika, iliyopo Mjini Bagamoyo na kugeuzwa kuwa Guest House huku ni kivutio na historia kubwa katika nchi yetu?

Swali langu la pili. Kwa kuwa majengo mengi yamevunjwa na yanaendelea kuvunjwa kwa sababu ya mwingiliano wa mamlaka ambapo Wizara ya Maliasili na Utalii inamiliki kisheria uhifadhi wa majengo, mamlaka za Serikali za Mitaa hutoa vibali vya kujenga na kuvunja.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutunga sheria na kuanzisha chombo kimoja kitakachosimamia ulinzi, usimamizi wa majengo kale nchini kote badala ya kuanzisha kwa Jiji la Dar es Salaam peke yake?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Namelok Sokoine, amekuwa mfuataliaji na mdau mkubwa sana katika eneo hili la utalii.

Mheshimiwa Spika, majengo haya ya kihistoria yanaweza kumilikiwa na watu binafsi, taasisi au Serikali. Hili jengo la Posta ya Bagamoyo liliuzwa na PSRC kipindi cha nyuma. Jengo hili mmiliki binafsi ana haki ya kulitumia anavyotaka.

Lakini nataka nimhakikishie tu kwamba Serikali imeshaanza mazungumzo na mmiliki binafsi kuona njia gani sahihi tunaweza kuendelea kuliboresha jengo hili. Kwa sababu jambo la msingi katika jambo hili ni kuhakikisha jengo hili halihami katika ule uhalisia wake uliokuwa zamani. Kwa hiyo, sisi kama Serikali tutaendelea kulikarabati.

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, katika Jiji la Dar es Salaam majengo yake mengi yana umri zaidi ya miaka mia moja na hata mengine kufika miaka mia moja na hamsini na kwa vile tunaona jinsi majengo hayo yanavyopukutika na kuondosha haiba na historia ya Jiji la Dar es Salaam. Ukichukulia mfano mzuri nchi ya China mbali na utajiri wake wamehifadhi mijji 32 ya majengo ya kale.

Serikali inasemaje kwa kutokutoa vibali kwa majengo yaliyobaki angalau baada ya miaka ijayo mia moja tukawa na majengo ya historia na ukaingia katika World Heritage chini ya UNESCO tukafaidika na sekta ya utalii nchini Tanzania?

SPIKA: Umekumbuka Mji Mkongwe! Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. (Makofi/Kicheko)

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba itambulike kwamba majengo yote yanaingia kwenye *Historical Heritage* yanapokuwa yanaanza miaka mia moja na kuendelea. Mwaka 2006 Serikali ilitoa GN.Na. 135 kuyatambua majengo yote ambayo tayari yalikuwa yamezidi miaka mia moja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nataka nimhakikishie tu kwamba kwa sheria na mamlaka aliyokuwa nayo Waziri ana uwezo wa kuzuia Jengo lolote lisibolewe kwa Kifungu Na. 3(1) cha sheria Na. 22 ya mwaka 1979. (Makofi)

Na. 87

Motisha kwa Wananchi wa Vijiji vinavyozunguka Pori la Akiba Uwanda

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE (K.n.y. MHE. IGNAS A. MALOCHA) aliuliza:-

Pori la akiba la Uwanda Game Reserve lililopo katika Jimbo la Kwela limezungukwa na Vijiji vya Kata za Kipeta, Kaoze na llemba na wananchi wa maeneo haya ni walini wakubwa wa pori hilo:-

Je, Serikali imewahi kutoa motisha gani kwa wananchi hao katika kusaidia miradi ya Maendeleo kama ujenzi wa shule, zahanati na vituo vya afya kama inavyofanyika kwenye maeneo mengine yanayozungukwa na hifadhi?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pori la Akiba Uwanda lenye ukubwa wa kilomita za mraba 5,000 lilianzishwa mwaka 1959 na kutangazwa upya kwa Sheria ya Uhifadhi Wanyamapor Na. 12 ya Mwaka 1974, kwa tangazo la Serikali Na. 275 la Tarehe 8 Novemba, 1974. Pori hilo kwa kipindi chote tangu mwaka 1974 hadi 2013 ilikuwa likisimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga. Mchakato wa kukabidhi pori hilo kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga, kwenda Wizara ya Maliasili na Utalii ulianza Mwaka 2013 na lilikabidhiwa rasmi tarehe 20 Januari, 2014.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni kipindi tangu Wizara ikabidhiwe Pori la Akiba la Uwanda, bado hatujachangia chochote katika shughuli za Maendeleo katika vijiji vya Kata za Kipeta, Kaoze, na llemba, zinazozunguka pori hilo.

Aidha, Wizara imeanza kuboresha na kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu ili kuhakikisha kwamba pori hilo linaludi kwenye hadhi yake ya awali.

Mheshimiwa Spika, Wizara inakiri kupokea barua ya tarehe 1 Januari, 2015 yenye maombi ya vifaa vya ujenzi wa Miradi ya Maendeleo katika vijiji vinavyozunguka pori hilo kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge wa Kwela na tayari tumeshaingiza kwenye mchakato wa kuona ni namna gani tutachangia katika shughuli za maendeleo kupitia Mfuko wa Uhifadhi Wanyamapor Tanzania (*Tanzania Wildlife Protection Fund (TWPF)*).

Aidha, tutatuma watalaam kwenda kuhamasisha kuhusu faida watakazopata wananchi na Serikali kutokana na kuhifadhi pori hilo.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; nataka Tamko la Serikali, ni lini wataanza kusaidia vijiji vinavyozunguka Pori hilo la Uwanda katika Jimbo la Kwela?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; tatizo la Serikali kutokusaidia wananchi wanaozunguka Pori la Uwanda, linafanana kabisa na tatizo la Serikali kutokusaidia Pori la Moyowosi na Kigosi lililopo katika Mkoa wa Kigoma katika Wilaya ya Kakonko, Kasulu na Kibondo. Nataka kujua sasa, Serikali inasaidia nini mpaka sasa kwenye Vijiji hivyo vinavyozunguka Pori hilo la Kigosi na Moyowosi? (Makofii)

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kama nilivyozungumza kwenye jibu la swali la msingi; Pori la Akiba la Uwanda limeanza kumilikiwa na Maliasili toka mwezi wa kwanza mwaka 2014. Kwa hiyo, tuna mwaka mmoja, lakini ikumbukwe tu nimesema Mheshimiwa Mbunge ameleta barua ya kuomba vifaa kwetu na hiyo barua tumeshaiingiza kwenye mchakato. Nataka nimhakikishie tu kwamba, mwaka huu wa fedha tutahakikisha kwamba, anapata vile vifaa alivyoviomba.

Mheshimiwa Spika, Pori la Akiba la Kigosi Moyowosi ni mionganoni mwa Mapori ya Akiba ambayo yanamilikiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii. Nataka nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge, 25% ya mapato yanayotoka kwenye uwindaji huwa tunayapeleka kwenye mapori husika na safari hii mwaka jana na mwaka huu hatukupeleka, lakini nimewasiliana na wenzangu ni kwamba, baada ya Bunge hili, watapeleka hiyo 25% katika mapori hayo.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa, tatizo hilo la Pori la Akiba la huko Kwale linafanana sana na tatizo lililoko kule Simanjiro kwa Pori la Akiba la Mkungunero ambako wananchi pamoja na kusaidia kuhifadhi hifadhi hiyo, hawajunufaika kwa namna yoyote. Je, kwa kauli ya Naibu Waziri, wananchi wanaozunguka Pori hilo la Akiba la Mkungunero na wenyewe wanafaidikaje?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwanza ieleweke sehemu kubwa ya Pori la Akiba la Mkungunero iko katika Wilaya ya Kondoa na sisi kama Wizara tunasaidia sana katika Wilaya ya Kondoa, ikiwemo kusaidia katika ujenzi wa maabara; tumetoa zaidi ya milioni 300 katika eneo hili la Kondoa.

SPIKA: Naomba tuendelee na Wizara ya Viwanda na Biashara Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya anauliza swali hilo!

Na. 88

Hitaji la Soko la Matunda Nje ya Nchi

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA aliuliza:-

Tanzania ni moja ya nchi zinazozalisha matunda kwa wingi na bado viwanda vya kusindika matunda havijakidhi haja; hali inayosababisha wakulima wengi wa matunda kukosa na matunda mengi kuozeana mashambani:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutafuta soko la matunda nje ya nchi kama zinavyofanya nchi nyingine?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mkakati wa mauzo ya nje (*National Export Strategy*) wa mwaka 2009 ulainisha pia, mikakati ya kuongeza mauzo ya matunda, maua na mbogamboga. Kutokana na hali hii thamani ya mauzo ya matunda nje imeongezeka kutoka Dola za Kimarekani 7,440,095 kwa mwaka 2010 hadi Dola za Kimarekani 32,116,895.22 kwa mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia TBS, SIDO na TANTRADE ambazo ni taasisi zilizoko chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara, wamekuwa wanatoa elimu ya uzalishaji na ufungashaji kwa kuzingatia ubora na viwango vya Kimataifa. Kwa mfano, terehe 13 Februari, 2015 Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Kuwezesha Biashara ya Canada (*Trade Facilitation Office of Canada*) iliandaa semina kwa wajasiriamali wa bidhaa za matunda kuhusu vigezo na mahitaji ya soko la nchi ya Canada.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali immeanzisha kampuni ya Global Standard One Tanzania (GS1) inayoratibu mfumo wa ufuutiliaji wa mnyororo wa bidhaa (*Traceability*) ambao ni msingi mkubwa katika kupata soko la bidhaa yoyote nje ya nchi. Serikali inaendelea kutangaza bidhaa zetu kupitia Maonyesho ya Biashara ya Ndani, Kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, TANTRADE kwa kushirikiana na Chama cha Wazalishaji Maembe (AMAGRO), inaratibu mpango wa kutoa mafunzo ya uzalishaji bora, ufungashaji na kujenga kituo cha kuchambua na kupanga ubora wa maembe (*Pack Houses*), ili kuuzwa kwenye soko la Kimataifa. Aidha, Kampuni ya AMAGRO inaendelea kuhamasisha kilimo cha maembe aina ya Tommy na Alfonso, ili kuuza soko la nje.

Mheshimiwa Spika, Mkoani Tanga tumeanzisha Program ya MUVI katika Vijiji tisa, ili kuzalisha machungwa yasiyo na mbegu kwa matumizi ya ndani na soko la nje. Kampuni ya AFRICADO inayozalisha maparachichi Wilayani Hai na Rungwe Avocado Company ambazo zote zinawashirikisha wakulima wadogo (*Out Growers*) yanazalisha kwa kuuza soko la nje.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tayari tumeanza mazungumzo na Nchi za Falme za Kiarabu kuona jinsi ya kupeleka matunda yetu kwenye soko lao. Mwisho, Serikali imewezesha kushawishi Mashirika ya Kimataifa ya Ndege kuongeza idadi ya safari pamoja na kiwango cha mzigo kinachosafirishwa kutoka Tanzania kwenda nje ya nchi. Ahsante.

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini nina masuala madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa, idadi ya fedha hizi zinazopatikana, yaani dola milioni 32, ni kidogo sana ukilinganisha na uzalishaji wa matunda nchini Tanzania na kwa kuwa, nchi kama India inapata mamilioni ya dola kusafirisha maembe ya aina ya alfonso kupeleka nchi za Ulaya. Hapa amejibu swali kwamba, kuna mpango kuanzisha mbegu hii ya tommy na alfonso. Ni lini Serikali itakuwa na mikakati ya lazima na ya uhakika ya kuhakikisha kwamba, hizi mbegu za maembe zinapatikana, ili zioteshwe nchini Tanzania kwa ajili ya kutafuta soko hilo nchi za Ulaya na Mashariki ya Kati? Swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama jawabu linavyosema hapa kwamba, alifanya ziara nchi za Mashariki ya Kati, hasa Oman, kwenda kuzungumza namna gani tunaweza tukafaidika na kusafirisha matunda. Nchi kama Oman, Dubai, Doha, ndege zake zina-serve mara mbili kwa siku nchini Tanzania. Je, kumechukuliwa initiative gani na Wizara angalau kufuatilia ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na atakubaliana nami Mheshimiwa Waziri kwamba, niko tayari kufuatana naye kwenda nchi hizo ili kutafuta hilo soko na kumsaidia? (Makofii)

SPIKA: Hiyo kali. Mheshimiwa Naibu Waziri! Itabidi umwombe Spika safari. (Kicheko)

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, kwanza nataka kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Sanya kwa mchango wake. Ni kweli, fedha tunazopata zinaweza zikaongezwa kwa sababu, tayari kuna mikakati ya kuhamasisha wakulima wengi zaidi walime matunda na mboga kwa wingi zaidi na kwa ubora zaidi. Ni imani yangu kuwa hiyo, itaongeza thamani ambayo tutakuwa tunaiapata.

Mheshimiwa Spika, na ni lini mkakati huo; mkakati tayari upo Mheshimiwa Sanya, ila tunaendelea kuufuatilia kwa karibu zaidi na kuuboresha. Kwa sababu, hata haya tunayoyafanya mpaka sasa hivi ni kutohana na huo mkakati wa *Export Strategy* kwa ajili ya hotculture products.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na safari aliyoifanya Mheshimiwa Waziri Mkuu; tunaifuatilia na tunafahamu kuwa sasa hivi kuna fursa. Hata mimi mwenyewe nilikwenda Dubai pia, tuna fursa. Kwa hivyo, ni vitu vyote ambavyo tutavifanya kazi kwa pamoja kwa kuongeza kwanza elimu kwa wakulima, wazidi kuzalisha kwa ubora zaidi, lakini vile vile kuwahamasisha katika masuala ya kufungasha vizuri kwa ajili ya kuvutia wawekezaji.

Nafurahi sana nikiweza kusafiri na wewe Mheshimiwa Sanya kwenda pamoja kwenda kutafuta soko. Ahsante sana. (Makofii)

SPIKA: Mnatafuta soko, mitandao haipo?

Mheshimiwa Soni? (Kicheko)

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri kuwa, je, ni lini kwa yale matunda ambayo siku zote tunasema tunaagiza kutoka nije ya nchi, ambayo yanaweza kuzalishwa ndani ya nchi, zile mbegu zake ziweze kusambazwa kwa wakulima wa Tanzania ili badala ya kuagiza matunda kutoka nije tuwe tunazalisha matunda humu ndani ya nchi kama zabibu za mezani, *apple, pears, peaches*, ambayo badala ya kutumia fedha nyngi za kigeni wakulima wa kwetu wangefaidi. Ni lini sasa kutakuwa na mkakati wa kusambaza hizo mbegu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri!

Kama kule kwetu *apples* na *peas* zote hizo.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, kuhusiana na ni lini sasa mbegu zitasambazwa. Huu ni mkakati ambao sasa hivi ndiyo tunaufanya kazi. Tutafanya tathmini ya kiasi gani kinachohitajika na kufanya utaratibu wa kuzipata hizo mbegu huko ambako zinapatikana.

Mheshimiwa Spika, vile vile nataka tu kutoa taarifa kuwa, hata Afrika Kusini sasa hivi tulikuwa tuna mazungumzo nao. Jana nimetoka Dar-es-Salaam kuzungumza na Waziri wa Ujasiriamali wa kule, yuko tayari kwa wawekezaji wa kule kuja kuwekeza katika mashamba kulima hapa matunda ambayo yatakuja kuzalishwa hapa kama yatakuja kuchakatwa hapa badala ya kuagiza juice na matunda kutoka nje. Kwa hiyo, huu ni mkakati ambaa tunaufanya kazi na nashukuru kwa mchango.

SPIKA: Ahsante. Tuendelee na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Victor Mwambalaswa!

Na. 89

Hitaji la Minara ya Simu Katika Jimbo la Lupa

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA aliuliza:-

Jimbo la Lupa lina maeneo mengi yasiyo na mawasiliano ya uhakika:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga minara ya simu kwenye Kata za Ifumbo, Mamba, Lualaje, Mtanila, Matwiga, Mafyeko na Kambi Katoto?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Vijiji vya Kata za Ifumbo, Lualaje, Matwiga, Mafyeko na Kambi Katoto katika Jimbo la Lupa, Wilaya ya Chunya, Mkoani Mbeya, vimeingizwa katika Mradi wa Mawasiliano Vijijini Awamu ya Pili B, unaosimamiwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa wote. Mradi huu unahusisha vijiji mbalimbali kutoka Kata 175 nchini, unatarajiwa kugharimu Dola za Kimarekani milioni 11 na kukamilika mwezi Januari mwaka, 2016.

SPIKA: Waheshimiwa utulivu! Utulivu! Na wanaotaka kuongea waende nje!

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, Kata ya Mamba imeingizwa katika Mradi wa Mawasiliano Vijijini, Awamu ya Pili A unaosimamiwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, ambapo jumla ya Kata 158 nchini ziliainishwa kwa ajili ya kipelekewa mawasiliano. Ujenzi wa mnara katika Kata hizo unatarajiwa kuanza mwezi Mei, 2015.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika jitihada zake za kufikisha mawasiliano nchi nzima, Serikali iliingia makubaliano na Kampuni ya Viettel Tanzania kufikisha huduma hiyo katika Vijiji 4,000 ndani ya miaka mitatu. Katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa makubaliano hayo kampuni hiyo itafikisha mawasiliano katika Vijiji 1,500 nchini kabla ya mwezi Juni, 2015 ambapo Kata ya Mtanila iliyopo katika Jimbo la Lupa imejumuishwa.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naishukuru Serikali kwa majibu yake mazuri. Pamoja na majibu hayo nina maswali mawili ya nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri anasema katika jibu lake kwamba, Serikali imeingia makubaliano na

Kampuni ya Viettel ili kuweza kufikisha mawasiliano kwa wananchi katika awamu ya kwanza na katika vijiji hivyo 1,500 vimo na Vijiji vya Kata ya Mтанila.

Mheshimiwa Spika, sasa Kata ya Mтанila iko kwenye Tarafa ya Kipembawe ambako mzunguko wa pesa kwa mwaka ni zaidi ya shilingi bilioni 20 kwa sababu wanalima tumbaku na kuza tumbaku. Sasa katika Tarafa hiyo kuna Kata za Lualaje, Matwiga, Mafyeko na Kambikatoto na Mamba. Sasa kwa nini Serikali isingejumuisha katika awamu ya kwanza, Mтанila na Kata zingine hizo ambazo ziko kwenye Tarafa moja?

Mheshimiwa Spika, la pili, kweli nimeona kampuni hiyo ya Viettel inachimba mtaro kutoka Mbeya kwenda Singida; sasa Kata ya Ifumbo na Vijiji vyake iko nje ya mtaro huo. Je, Serikali inasemaje kuongeza vijiji ambavyo viko kwenye Kata ya Ifumbo katika awamu hii ya kwanza?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, baada ya kupata jibu la awali nimefuatilia taarifa za ziada kuhusu miradi inayoendelea kufanywa na kampuni ya Viettel. Hadi sasa napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mwambalaswa na wananchi wa Wilaya ya Chunya kwamba, minara 14 imeanza kujengwa na Kampuni ya Viettel pamoja na Mkongo. Minara imejengwa na inaendelea kujengwa katika Kata za Mamba, Isangwana, Mafyeko na kwingineko.

Mheshimiwa Spika, vile vile nakubaliana kabisa na hoja ya Mheshimiwa Mwambalaswa kwamba, hatuwezi kuacha Vijiji vya Kata ya Ifumbo na kuendelea na maeneo mengine wakati na wenyewe wanahitaji mawasiliano. Kwa hiyo, napenda kumpa taarifa kwamba, mkongo unaendelea kujengwa kutoka Makongolosi hadi Lupa hadi Isangwana na Mafyeko, lakini tutahakikisha kwamba, wanarudi wanachepuka na kwenda katika Kata ya Ifumbo katika Jimbo la Lupa.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupewa nafasi. Suala la Lupa linafanana na Wilaya yetu ya Njombe.

Mheshimiwa Spika, tuna matatizo makubwa katika Wilaya ya Njombe juu ya mawasiliano, hususan Kata ya Kifanya, Kata ya Kitandiililo, Kata ya Ikuna, Igongolo na Kata ya Lupembe kule Ikondo. Nilizungumzia kipindi fulani hapa kwamba, mawasiliano ni tatizo katika Wilaya ya Njombe na baadhi ya maeneo watu wamekuwa wakipanda juu ya miti. Pia nilisema wakati fulani baadhi ya watu wamedondoka, wameumia, kwa kukosa mawasiliano na nilimwambia Mheshimiwa Naibu Waziri juu ya jambo hili. Ni lini sasa katika Wilaya ya Njombe, hususan maeneo ambayo hayana mawasiliano, tutapata mawasiliano? (Makofsi)

SPIKA: Nashukuru kwa kuniwakilisha. Kule kwetu mpaka leo huwezi kupata simu! (Makofsi)

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, nakubali kabisa kwamba, maeneo mengi katika nchi yetu kwa miaka mingi yamekuwa na matatizo ya mawasiliano. Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, Serikali imeongeza kasi kubwa ya kuhakikisha kwamba, maeneo hayo yanafikiwa na mawasiliano na ahadi yetu ni ile ile kwa kutumia Mfuko na Kampuni hii mpya ya Viettel kuhakikisha kwamba, tunapeleka mawasiliano kote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kumuahidi Mheshimiwa Sanga na kumpa taarifa na kukupa taarifa Mheshimiwa Spika, kwamba, binafsi nitafanya ziara katika Wilaya ya Njombe katika mwezi wa Nne, nikija na Wataalam wote wanaohusika na jambo hili pamoja na Makampuni ya Simu, ili kupita kote ambako tumewapa kazi ya kupeleka mawasiliano na

kuwahakikishia wananchi kwamba, mawasiliano yanakuja na kuyahimiza makampuni haya yafanye haraka kabla ya mwezi Julai mwaka huu.

SPIKA: Haya ahsante! Ahadi ni deni.

Mheshimiwa Engineer Athumani Mfutakamba, swali linalofuata?

MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Igala, kwanza nitoe pole kwa msiba wa mama mdogo, Binti Sefu Masapila. Sasa naomba Swali langu Namba 90, lipatiwe majibu. (Kicheko)

Na. 90

Matumizi ya Simu na Mitandao ya Pesa

MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA aliuliza:-

Je, ongezeko la matumizi ya simu za viganjani na matumizi ya pesa mtandao kwa M-Pesa, Tigo Pesa na Airtel Money yatashusha gharama kiasi gani kwa watumiaji (Economies of Scale)?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Engineer Athuman Rashid Mfutakamba, Mbunge wa Igala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sasa wananchi wanaweza kutuma pesa, kupokea, kuhamisha au kuchukua kutoka kwenye akaunti zao za benki na kufanya malipo mbalimbali kwa kutumia simu za viganjani.

Mheshimiwa Spika, kabla ya matumizi ya pesa ya mtandao kuwepo mtumiaji wa huduma za kibenki ilimlazimu asafiri hadi mahali benki ilipo, ajaze fomu, apange foleni, asafari kurudi nyumbani baada ya kupata ama kutokupata huduma husika. Watumiaji wa huduma za kibenki walikuwa wanapoteza muda mwangi na gharama za usafiri wakati wakifuata huduma mbalimbali ambapo pana huduma za kibenki.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya pesa ya mtandao yameboresha kwa kiasi kikubwa huduma za fedha nchini na kuwajumuisha watu wengi ambao hawakuwepo katika mzunguko wa fedha, vile vile kushusha gharama za upatikanaji wa huduma hizo. Kwa kutumia pesa mtandao mtumiaji wa huduma ya kibeki sasa ataokoa muda na gharama katika kufuata huduma za kibenki ambapo benki imejengwa.

Mheshimiwa Spika, mwananchi anayeishi kijiji ambaye alikuwa anatembea ama kusafiri kwa umbali wa wastani wa masaa sita kufuata huduma ya fedha ambapo kuna benki sasa kwa kutumia huduma ya fedha mtandao mwananchi huyo anaweza kupata huduma husika ndani ya wastani wa saa moja.

Mheshimiwa Spika, muda hutegemea huduma inayohitajika kuweka fedha ama kutoa fedha na umbali wa mahali ambapo huduma ya pesa ya mtandao ipo. Aidha, mtumia

huduma ya pesa mtandao anaweza kutuma fedha kutoka katika simu yake katika muda usiozidi dakika mbili. Sambamba na hilo gharama za usafiri katika kufuata huduma za kibenki hupungua kwa kiasi kikubwa.

MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, goggle, facebook, twitter, yahoo, IBM, HP na makampuni mengine Microsoft kama hizi Kampuni za Simu zingeweza kupata kiungo hai (*organic link*) baina yake na taasisi kama TICRA pamoja na COSTECH tungeweza kuwa na teknolojia, ushindani na uvumbuzi kutengeneza ajira za kutosha kwa vijana wetu.

Napenda kujua Serikali ina utaratibu gani kwa kutengeneza hub ya TEHAMA ili vijana wetu waliohitimu kwenye hisabati na mambo ya TEHAMA waweze kupata ajira? Marekani theluthi mbili ya wahitimu wanapata ajira za kujiajiri, Ulaya nusu yao wanajiajiri.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, sasa hivi iko teknolojia ya kukamata simu za uhalifu, inaitwa minara egeshi (*site simulator*) ambayo inaweza kujua simu au barua pepe au mazungumzo yanayozungumzwa baina ya watu. Je, Serikali teknolojia hii inakuja lini hapa ili kudhibiti uhalifu? Nashukuru sana. (Makof)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi muda umekwisha!

NAIBU WAZIRI W MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa kwa Bunge lako na kwa Mheshimiwa Mfutakamba kwamba Serikali tayari inacho kituo cha kuatamia uvumbuzi na mawazo ya kibashara ya vijana pale Dar es Salaam kilicho chini ya COSTECH na tumekiunganisha kituo kile na Makampuni ya Simu ambapo vijana ambao wanaweza kutengeneza *applications* mbalimbali na wanaweza kupata biashara kutoka kwenye Makampuni ya Simu.

Mheshimiwa Spika, mifano ipo mingi tu ambapo vijana wamefanya vizuri katika baadhi ya *applications* zinazotumika kwenye simu sasa hivi. Nyingi zimegunduliwa na kuatamiwa na kuendelezwa katika kituo chetu pale COSTECH na tunayo fahari kubwa kwamba katika nchi yetu tunao vijana wengi wenyе vipaji na tunaomba Bunge lako lituongezee bajeti katika kituo kile katika bajeti ijayo ili tuweze kuchukua vijana wengi zaidi kwa sababu mahitaji ni makubwa kuliko uwezo wa fedha. Kwa hiyo, hilo tayari tumeanza kulifanya kuunganisha Taasisi za Elimu pamoja na Biashara ya Makampuni ya Simu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, Serikali inao mpango na kupitia Mamlaka ya Mawasiliano kwa Wote na tumeshanunua kifaa kinaitwa *central equipment identity register* ambapo inawezekana siyo tu kutambua simu ambayo imetumika kufanya uhalifu na kuifuatilia ilipo na kama inaendelea kutumika bali hata kuizima ili isiendele kutumika katika mitandao mingine.

Mheshimiwa Spika, kinachosubiriwa sasa ni hiki kifaa cha Serikali na Makampuni ya Simu na yenyele yanunue ili kuweza kuwa na muunganiko. Kwa hiyo, siku zijazo siyo tu simu zitasajiliwa kwa maana ya *sim card* lakini hata vifaa (*devices*) tunazotumia ili ziwe ndani ya mfumo ili itakapotumika kwa uhalifu, basi mamlaka iweze kuzifuatilia.

Mheshimiwa Spika, vile vile kama unavyofahamu, katika siku chache zijazo, tutaleta Sheria hapa ya Kudhibiti Uhalifu Mitandaoni ambayo itatusaidia kwa kiasi kikubwa sana kudhibiti uhalifu unaoendelea mitandaoni, kwa kuweka taratibu mbalimbali ambazo zitabana uhalifu na

zitawezesha wao kushtakiwa na kupewa adhabu kuliko ilivyo sasa ambapo tunakosa nyenzo muhimu za kuadhibu wale ambao wanafanya uhalifu mitandaoni.

SPIKA: Haya tuendelee na Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Profesa Kahigi!

Na. 91

Mradi wa Electricity V Bukombe

MHE. ANTONY G. MBASSA (K.n.y MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI) aliuliza:-

Mradi wa Electricity V katika Wilaya ya Bukombe na Mbogwe ulizinduliwa mwaka juzi, 2013, ulitarajiwa ifikapo Juni, 2014 lakini hadi sasa mradi huo unasuasua na kuonyesha dalili za kutokamilika kwa wakati uliokusudiwa.

Je, ni lini sasa mradi huo utakamilika?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kanarwanda Kahigi, Mbunge wa Bukombe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika mradi wa Electricity V unahusisha mikataba miwili ambayo ni mkataba wa usambazaji umeme katika Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Geita na ujenzi wa vituo vya kupoozea umeme substation vya llala na Sokoine Dar es Salaam na Kituo cha Njiro Arusha. Gharama za mradi ni dola za Kimarekani 43.16 ambazo ni mkopo kutoka Africa Development Bank.

Mheshimiwa Spika, kazi za mkataba wa usambazaji wa umeme unaohusisha Wilaya ya Bukombe na Mbogwe zipo lot B ambayo inahusisha ujenzi wa njia za umeme ya msongo wa kilovoti 33, ufungaji wa transfoma 41 na kuunganisha wateja wa awali wapatao 5,011 katika Wilaya ya Msalala, Bukombe na Mbogwe.

Mheshimiwa Spika, kazi zinazoendelea katika maeneo ya Wilaya ya Bukombe na Mbogwe, Mkoani Geita ni pamoja na kusimika nguzo za utandikaji wa nyaya za msongo wa kilovoti 33 na kazi hizo zimekamilika kwa asilimia 30 mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Electricity V ulitarajiwa kukamilika Juni, 2014 kwa mujibu wa makubaliano ya mkopo kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Benki ya Maendeleo ya Afrika. Mkataba kati ya TANESCO na Mkandarasi Kampuni ya Eltel ulitarajiwa kumalizika tarehe 14 Septemba, 2014. Hata hivyo, kutokana na kuchelewa kukamilishwa kwa suala la fidia na upatikanaji wa nguzo kwa wakati mkataba wa mkandarasi sasa umeongezwa muda hadi tarehe 31 Mei, 2015 na mradi wa Electricity V unatarajiwa kukabidhiwa mnamo Juni, 2015.

MHE. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Ni kweli mradi huu umechukua muda wa kutosha na sasa umeongezwa muda. Swalii la kwanza, je, ni lini mradi huu sasa utaanza kutekelezwa katika vijiji na maeneo muhimu au center zinazokua kama Bulega, Namonge, Katoma, Yogelo, Butinsya, Bulega, Busonzo na maeneo ya huduma muhimu katika Jimbo hili la Bukombe?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa maeneo ya umeme huu wa REA yanafanana kabisa na maeneo ambayo yametekelozwa mradi huu katika Jimbo la Boharamulo Magharibi Vijiji 12 na ikumbukwe ahadi ya aliyekuwa mtangulizi katika Wizara hiyo Profesa Muhongo tarehe 26 Julai, 2013 ilikuwa kwamba kufika mwezi Desemba tumepata mashine ya umeme, lakini mpaka sasa mashine hizo hazijaja na ukizingatiwa sasa hivi....

SPIKA: Jamani naomba mnyamaze.

MHE. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Spika, ikizingatiwa sasa hivi mashine zilizopo mbili zimechoka sana kusambaza umeme Wilaya ya Biharamulo na kwa jirani yangu Dkt. Magufuli kule Chato. Je, ni lini mashine hizo za umeme zitapatikana ili kuondoa adha ya umeme kwa jimbo la Biharamulo Magharibi? Ahsante.

SPIKA: Ahsante, humu humu ndani kazima umeme. (Kicheko)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE): Mheshimiwa Spika, kuhusu Bukombe vijiji vilivyotajwa kama viko kwenye scope utekelezaji unaendelea na tarehe nilizosema Juni, 30 utakuwa umekamilika, kama viko kwenye scope, kama haviko kwenye scope, namwomba Mheshimiwa Mbunge aje tuzungumze nimweleze kama inatekelezwa sasa additional scope au ni kwenye phase inayokuja.

Mheshimiwa Spika, suala la Biharamulo na Chato. Biharamulo na Chato mna upungufu wa kilowati 400, nimezungumza na Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO kwamba jitihada zifanyike, tutafute mitambo ambayo haifanyi kazi *idle capacity* kutoka popote Tanzania, kuna sehemu mbili kuna mitambo ya *idle capacity* ihamishiwe pale. Nimewaeleza kwamba nawapa siku 45 mitambo ipelekwe pale na nitakwenda mwezi wa Nne unaokuja kusudi Biharamulo na Chato msiwe na matatizo wakati tunasubiri mtambo wenu wa **Olio** ambao utakuja baada ya miezi 13. Mimi sitaki miezi 13 nataka siku 45.

SPIKA: Naomba tuendelee, Waheshimiwa tuwe tunaangalia na saa, tunapenda sana kuuliza maswali lakini muda hautoshi. Mheshimiwa Maige swali linalofuata!

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Kabla ya kuuliza swali langu kwa ukubwa wa suala naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi ilivyoshiriki kwenye janga la maafa kwenye Kijiji cha Makata ambapo watu 47 walikufa na wengine 4,000 kuachwa bila makazi. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais alivyofika kutupa pole. Niombe wadau wengine likiwemo Bunge wazidi kutushika mkono kwa sababu matatizo bado yapo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo, sasa naomba swali langu namba 92 lipatiwe majibu.

Na. 92

Maombi ya Fidia kwa Wananchi Waliopisha Mgodi wa Bulyanhulu

MHE. EZEKIEL M. MAIGE aliuliza:-

Wakati wa kuanzisha mgodi wa Bulyanhulu mwaka 1996 kaya 4,176 zilihamishwa bila fidia ikiwa ni pamoja na mali na mazao ya wananchi; na hata baada ya wananchi hao kufungua kesi Mahakamani hawajaweza kulipwa chochote zaidi ya kuwasilisha maombi ya kupewa japo kifuta jasho kwa Serikali mwaka 2009.

Je, Serikali imefikia hatua gani katika kufanya kazi maombi ya wananchi hao?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge wa Msalala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya mwaka 1996, Kampuni ya Kahama Mining Limited inayomiliki mgodi wa Bulyanhulu iliendesha shughuli za utafutaji mkubwa wa madini katika maeneo ikiwa inamiliki leseni ya utafutaji wa madini namba PL 216/94 ya tarehe 5/9/1994.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho kulikuwa na wachimbaji wadogo ambao walikuwa wakiendesha shughuli za uchimbaji madini ndani ya leseni ya utafutaji wa madini ya Kahama Mining Company Limited bila kuwa na leseni na baadhi yao walikuwa wameweka makazi ya muda katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, baada ya shughuli ya utafutaji mkubwa wa madini katika eneo hilo kubaini kuwepo kwa mashapo ya dhahabu yanayoweza kuchimbwa kibiashara mwaka 1996, wachimbaji wadogo walitakiwa kusitisha shughuli za uchimbaji madini katika eneo hili ili kupisha ujenzi wa mgodi. Wachimbaji hao walitii amri na kusitisha shughuli zao za kuendesha shughuli katika Kijiji cha Kakola ambako ni makazi rasmi ya wananchi hadi sasa. Aidha katika eneo hilo lililokuwa na wachimbaji wadogo hapakuwa na shughuli zozote za kilimo zaidi ya uchimbaji.

Mheshimiwa Spika, wakati mgodi wa Bulyanhulu unaanzishwa mwaka 1996, hakuna kaya yoyote iliyostahili kulipwa fidia kwa kuwa hakuna mtu aliyefukuzwa katika Kijiji cha Kakola ambacho ndipo kulikuwa na makazi rasmi ya wananchi. Iwapo mgodi ungehitaji kutumia eneo la Kijiji cha Kakola ungelazimika kufidia wananchi wote ambao wangetakiwa kupisha ujenzi wa mgodi kulingana na Sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, hivyo madai ya kuwepo kwa kaya 4,176 au wananchi wanaodai fidia hayana ushahidi kwa kuwa waliotakiwa kuondoka kwenye eneo linalomilikiwa na mgodi wa Bulyanhulu hivi sasa ni wachimbaji wadogo waliokuwemo ndani ya eneo hilo wakiendesha shughuli za uchimbaji bila kuwa na leseni.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niseme nimeshtushwa na majibu ya Waziri, sijui kama alikuwa anafuatilia vyombo vya habari mwaka 1994 vurugu zilizotokea pale na kuwepo tuhuma za watu kufukiwa wakiwa hai. Kwa hiyo anavyosema kwamba hapakuwepo watu na hapakuwepo malalamiko wala makazi, nashindwa kumwelewa.

Mheshimiwa Spika, naomba nipate majibu kwa maswali mawili yafuatayo ya nyongeza. Kwanza katika kuhamasisha wananchi waweze kupisha uwekezaji huo wenye mgodi pamoja na Serikali walihidi wananchi watapata manufaa mengi ikiwemo ujenzi wa barabara ya lami kutoka Kakola hadi Mji wa Kahama pamoja na hudjuma nyingine za kijaamii. Je, Serikali inasimamiae utekelezaji wa ahadi hiyo ambayo ilitolewa na Serikali mwaka 1996 pamoja na mwekezaji ambayo haijatekelezwa hadi sasa?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kinachoonekana ni kwamba, uwepo au kutokuwepo wa madai unatokana tu kutokuwepo ushahidi kwa upande wa Serikali na kwa sababu sisi tuna ushahidi wa kutosha wa mashamba yaliyokuwepo, makaburi yaliyokuwepo, mialo iliyokuwepo pamoja na vitu vingine vingi ambavyo viliharibiwa wakati huo. Je, Serikali iko tayari kupokea ushahidi huo na kulipa fidia inayostahili kwa sababu ushahidi upo na tatizo anasema ni ushahidi tu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, naomba iwe kwa kifupi kwa sababu muda umekwisha!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA): Mheshimiwa Spika, nimkumbushe tu Mheshimiwa Maige mimi mwaka 1983/1984 nilikuwa mchimbaji mdogo katika eneo hilo, kwa hiyo nalifahamu sana eneo hilo na ninafahamu mazingira ya namna ilivyokuwa wakati huo.

Mheshimiwa Spika, nipende tu kumhakikishia kwamba, wananchi katika eneo hilo ambaao anawataja, kama ana ushahidi atuletee, lakini usiwe ushahidi kama ambaao tumekuwa tukiletewa ambaao unaonesha sehemu nyingine kwa kuweka picha ambazo hazina uhakika kabisa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wananchi kupata huduma mbalimbali Kampuni ya Acacia ambayo sasa hivi inamiliki mgodi huo ambaao ni mgodi wa Bulyanhulu imeendelea kutoa huduma mbalimbali ikiwa pamoja na kulipa service levy ya 0.3, ikiwa ni pamoja na kuweka lami katika Mji wa Kahama, ikiwa ni pamoja na kutoa huduma mbalimbali katika maeneo ya shule na itaendelea kufanya hivyo kwa kushirikiana na Serikali.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tukae kwa pamoja, tushirikiane pamoja na Halmashauri yake ili tuweze kuwapatia huduma zilizo bora wananchi wa Kahama na sehemu nyingine ambako migodi inamilikiwa na wawekezaji kutoka nje ili waweze kupata faida kulingana na rasilimali zilizoko katika maeneo yao.

Na. 93

Ujenzi wa Barabara ya Mbalizi – Mkwajuni kwa Lami

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE aliuliza:-

Ahadi ya ujenzi wa barabara ya Mbalizi - Mkwajuni kwa kiwango cha lami imepita zaidi ya miaka mitano.

Je, ni lini kazi ya kujenga barabara hiyo itaanza?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Luckson Ndaga Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijijiini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mbalizi – Mkwajuni – Makongolosi yenyeye urefu wa kilomita 117 ni barabara ya Mkoa ambayo inahudumiwa na Wizara ya Ujenzi kuititia Wakala wa Barabara (TANROADS) sehemu ya barabara hii kati ya Mbalizi na Galula kilomita 56, imefanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kazi hiyo imefanywa na Mhandisi Mshauri aitwaye MAKCONSULT wa Dar es Salaam ambaye ameshawasilisha ripoti ya mwisho ya usanifu ambayo tunaipitia ili kujiridhisha. Hatua itakayofuata ni Serikali kutafuta fedha za ujenzi wa sehemu ya Mbalizi – Igulula kwa kiwango cha lami. Aidha, sehemu ya barabara iliyobakia kati ya Galula – Makongolosi itawekwa kwenye mipango ya kufanyia upembuzi yakini na usanifu kutegemeana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara ya Mbalizi – Mkwajuni hadi Makongolosi itafanya kwa awamu kuanzia sehemu ya Mbalizi – Galula kilomita 56 pindi fedha zitakapopatikana.

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu ya Serikali lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kazi ya kusanifu au kupitia ripoti ya msanifu wa barabara hiyo itakwisha lini maana ni ya muda mrefu sana?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, je, Serikali itakuwa tayari kutenga fedha ya kutengeneza barabara hiyo katika bajeti ya mwaka huu wa fedha? Ahsante sana.

SPIKA: Unamaanisha mwaka huu au mwaka ujao wa fedha?

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Mwaka ujao wa fedha.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze kwa namna ambavyo amekuwa anafuatilia sana ujenzi wa barabara hii kwa faida ya wananchi wa Mbeya Vijiji. Suala la kupitia ripoti ni kazi ambayo haitafanya kwa muda mrefu na kama nilivyo sema tu kwamba tumeahidi kwamba Serikali itaijenga, maana yake itabidi tuiweke kwenye bajeti itakayokuja, lakini tutajenga kwa awamu kulingana na kiwango cha pesa ambazo Bunge hili litaidhinisha kwa barabara hiyo.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda umekwisha sana na bahati nzuri na maswali yenyewe yamekwisha. Naomba nitambue baadhi ya wageni ambaa orodha yao nimeletewa. Tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambapo:-

Wapo wageni 40 wa Mheshimiwa Athuman Mfutakamba, ambaa ni Wenyeviti, Makatibu na Watendaji wa Kata 10 pamoja na Makatibu wawili wa Mbunge. Wako Viongozi wa Madhehebu ya Dini na Wazee Maarufu wakiongozwa na Mwenyekiti Juma Kanyanyato. Hawa wageni wote naomba wasimame walipo. Kumbe wapo hapo, karibuni sana, tunafurahi kuwaoneni. Ahsanteni sana. (Makofi)

Tuna wageni 30 wa Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, ambaa ni Mashehe wa Mkoaa wa Kilimanjaro wakiongozwa na Sheikh Hussein Chifupa Twairu Hussein. Waheshimiwa Mashehe walioko hapo wasimame tafadhali. Ahsanteni sana na karibuni sana. (Makofi)

Tuna wageni wa Mheshimiwa George Simbachawene, Waziri wa Nishati na Madini ambaa ni wanafunzi 36 kutoka Chuo cha Uhazili Dodoma na wanafunzi wetu wasimame walipo kama wamepata nafasi. Ahsante sana na mmevaa na sare kabisa, haya. (Makofi)

Tuna wageni sita wa Mheshimiwa James Daudi Lembeli, ambaa ni viongozi kutoka Jimbo la Kahama wakiongozwa na ndugu Yahaya Msafiri. Hawa viongozi wasimame walipo kama wamepata nafasi. Wako pale ahsanteni na karibuni sana. (Makofi)

Nakala ya Mlando (Online Document)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Sylvester Kasulumbayi, ambao ni ndugu Raphael Kasulumbayi, mtoto wake; Muhashi Mguku, dada yake; na ndugu Omar Abdallah mpwa wake. Naomba hawa nao wanafamilia wasimame mahali walipo, wapo pale nyuma. Karibuni sana. (Makofi)

Tuna wageni tisa wa Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wajumbe wa Baraza Kuu la UWT, Zanzibar kutoka Mkao wa Mjini Magharibi, wakiongozwa na ndugu Sania Mohamed, hawa nao wasimame walipo kama wana nafasi humu ndani. Ahsante, wako kule nyuma kabisa. Karibuni sana. (Makofi)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Moses Joseph Machali ambao ni Bi. Brigita Mptwa mke wake, huyo lazima aonwe peke yake, yuko wapi, yuko hapa na watoto, ana watoto Gloria Moses Machali na Victoria Moses Machali ni watoto wake. Hawa wajukuu wa Mheshimiwa Spika, karibuni sana. (Makofi)

Tuna wageni wanne wa Mheshimiwa Shaffin Sumar ambao ni Mheshimiwa Tanaeli Costa, Dwani Kata ya Mazama; yuko ndugu Swalehe Haruna Ibrahim, yuko ndugu Said Ramadhani Kiyao na ndugu Ismail Hussen Maganga. Naomba na Mheshimiwa Diwani wasimame walipo kama wameingia. Wapo kule nyuma, ahsante, karibuni sana Mheshimiwa Diwani na wenzio. (Makofi)

Nina wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo na ni Wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Vijana ambao ni wanafunzi 100 na Walimu 21 kutoka shule ya sekondari Rarya iliyopo Mwanza. Kwanza wasimame hao waliko hao 100 na Walimu 21 wasimame kama wapo. Ahsante sana karibu sana. (Makofi)

Halafu nina wanafunzi 39 ambao ni viongozi wa DARUSO kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, hawa ndiyo wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Habari, naomba wasimame hawa. Sasa katika hawa kuna Rais wao naomba huyo Rais aonekane maana yake inawezekana kesho, yuko na Waziri Mkuu tena na Mawaziri na wenyewe wasimame wanyoshe mikono yao, karibu wote ni Baraza na Wabunge. Kwa hiyo, hapa kuna Wabunge, Mawaziri Wakuu na nani karibu sana. Tunawaombeni kitabu ndiyo cha kwanza, mengine haya baadaye, karibuni sana. (Makofi)

Pia karibu na wageni wengine ambao hatujawataja. Katibu!

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Tume Kudhibiti UKIMWI Tanzania wa Mwaka 2014 (The Tanzania Commission for Aids (Amendment) Bill, 2014

(Kusomwa Mara ya Pili)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge nime-overlook kuna matangazo ya kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o anaomba niwatangazie kuwa Wajumbe wake leo saa saba watakuwa na kikao kwenye ukumbi wa Msekwa C.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Jasson Rweikiza, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba watakuwa na kikao chao chumba namba 231.

Halafu Mwenyekiti wa Jumuiya iliyopo hapa ya Mtakatifu Mo watakuwa na ibada yao leo. Mtoha hoja!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima naomba kutoa hoja kwa mujibu wa Kanuni ya 86(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013 kwamba Muswada wa Sheria ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI ya mwaka 2014 yaani The Commission for Aids Amendment Act, 2014, pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki katika Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Napenda kuchukua nafasi hii pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya masuala ya UKIMWI, Mheshimiwa Lediana Mafuru Mng'ong'o, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Makamu Mwenyekiti wa Kamati na Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa kuuchambua Muswada huu kwa kina na kutoa mapendekezo na ushauri uliosaidia sana kuboresha maudhui ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo na ushauri wa Kamati umewevesha kufanyika maboresho ya Muswada kama yanavyooneka katika Jedwali la Marekebisho lilitotolewa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kwa heshima kubwa kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada na kazi kubwa anayoifanya katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI nchini.

Mheshimiwa Spika, kitendo chake cha kujitokeza kupima na kuendelea kuhamasisha uwepo wa rasilimali na uratibu wa shughuli hizi zimempambanua Mheshimiwa Rais wetu kuwa mfano wa kiongozi kati ya viongozi wachache amba wanatamani Tanzania kufikia hatua ya kutokuwa na maambukizo mapya ya UKIMWI, kitu ambacho kinawezekana. Kitendo cha Mheshimiwa Rais kuamua kupima kulifungua kurasa mpya kuhusu mapambano dhidi ya UKIMWI na kuongeza chachu kwa wananchi wengi wa Tanzania kupima.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo imebadili taswira kubwa ya watu kuendelea kupima VVU kwa kasi kubwa na bila uwoga. Kabla ya kampeni hiyo watu milioni 2,200,000 ndiyo walikuwa wamepimwa, lakini hadi kufikia Desemba, 2014 watu zaidi ya milioni 25 wamepima.

Mheshimiwa Spika, kipekee pia napenda kutambua kazi kubwa ambayo inafanywa na Chama cha Wabunge cha Kupambana na UKIMWI yaani TAPAC chini ya Uongozi wa Mwenyekiti wake mahiri Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, ambaye ye ye binafsi pamoja na Wabunge wamekuwa mstari wa mbele bila kuchoka katika mapambano dhidi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba nimshukuru Mheshimiwa William Lukvi, Mbunge wa Ismani aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu na Bunge ambaye kwa muda mrefu ameshiriki kwa dhati na weledi mkubwa katika maandalizi ya Muswada huu. Pia nimshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa George Masaju na wataalam wa Ofisi yake kwa ushirikiano wao, wadau mbalimbali wa masuala ya UKIMWI na wananchi wote kwa ujumla kwa michango yao muhimu waliyoitoa ambayo imetumika kuboresha maudhui ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, aidha, namshukuru Katibu Mkuu na Naibu Katibu Ofisi ya Waziri wa Mkuu pamoja na wataalam wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI, Tanzania walioongozwa na Mwenyekiti Mtendaji kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kuhakikisha Muswada huu unafikia hatua hii.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwisha kusema hapo awali kwamba Muswada huu unawasilishwa katika Bunge lako Tukufu kwa mara ya pili. Sheria ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Sura 375 ilitungwa na kuanza kutumia mwaka 2001 kwa madhumuni ya kudhibiti na kuzuia maambukizi ya UKIMWI kwa kuweka muundo wa Tume, kazi, malengo na uratibu wa masuala ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha takribani miaka kumi na mbili cha utekelezaji wa sheria hii, kumekuwa na mafanikio mbalimbali. Sheria hii ndiyo iliyoanzisha Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania yaani TACAIDS ambayo tangu kuanzishwa kwake imetekeleza majukumu yake na kuchangia kuongezeka kwa uelewa wa masuala ya UKIMWI kwa kiwango kikubwa. Asilimia mia moja ya watu kati ya miaka 15 mpaka 45 wamesikia kuhusu VVU na UKIMWI na kati yao asilimia 73 wanauelewa wa kutosha kuhusu UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, pamoja na utoaji wa afua mbalimbali za UKIMWI, hali iliyochangia kupungua kwa kiwango cha maambukizo kutoka asilimia saba (7%) mwaka 2001 hadi asilimia tano (5%) mwaka 2012. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, kumekuwa na changamoto katika utekelezaji wa shughuli na majukumu ya Tume.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa katika utekelezaji wa shughuli na majukumu ya Tume kwa kiasi kikubwa umechangiwa na upungufu wa Sheria ya Tume ya mwaka 2001. Wakati sheria inatungwa ugonjwa wa UKIMWI ulichukuliwa kama tatizo la dharura na kwamba UKIMWI usingedumu kwa muda mrefu bila tiba kupatikana, lakini mpaka sasa sote ni mashahidi kwamba ni takriban miaka 30 sasa ugonjwa huu upo na bado tiba haijapatikana.

Mheshimiwa Spika, suala kubwa la chimbuko la Muswada huu ni sheria iliyopo kutotambua uwepo wa Mfuko wa Kudhibiti UKIMWI licha ya Sera ya Taifa ya UKIMWI ya mwaka 2001 kueleza uanzishwaji wa Mfuko huu. Mfuko huu, una umuhimu mkubwa kwani utawezesha kuwepo kwa uwiano wa mahitaji ya fedha na rasilimali zilizopo nchini kwa ajili ya udhibiti wa UKIMWI na kuendeleza uchangiaji wa wadau waliopo na wapya kwa kuwa na imani kutokana na ushiriki wa moja kwa moja na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kulingana na zoezi la kutathimini Mkakati wa Tatu wa Taifa wa kudhibiti UKIMWI, gharama ya kutekeleza mkakati wa Taifa wa kudhibiti UKIMWI kwa kipindi cha miaka mitano 2013/2014 hadi 2017/2018 ni shilingi bilioni 5.1 sawa na dola za Kimarekani milioni 2960. Kuna upungufu wa takribani shilingi bilioni 300 kwa mwaka na hivyo kusababisha afua nyingine kutofanyika. Serikali imetambua pengo hili ni kubwa na linahitaji kufanyiwa kazi kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, suala la kuanzisha Mfuko litaifanya Serikali kuanza kutumia rasilimali zake na kupunguza utegemezi. Vile vile kuwajengea uwezo wananchi wazalendo kuanza kuchangia masuala yanayohusu afya zao. Ili kuhakikisha Mfuko unaopendekezwa utawanufaisha wananchi, Serikali imezingatia mifano ya nchi nyingine kama Zimbabwe na Afrika ya Kusini ambazo zimefanikiwa katika kutekeleza suala hili.

Mheshimiwa Spika, hali ilivyo sasa utekelezaji wa sheria iliyoko sasa unakabiliwa na mazingira yafuatayo:-

Majukumu ya Tume, Tume imemelekezwa kutunga na kusimamia sera, mkakati wa utekelezaji kuhamasisha na kuwezesha upatikanaji wa rasilimali pamoja na kuratibu shughuli za udhibiti wa UKIMWI Tanzania Bara, lakini hata hivyo mfumo wa kiutendaji wa Menejimenti ya Tume, sheria iliyopo sasa inampa majukumu Mwenyekiti Mtendaji wa Tume kusimamia Tume na Sekretarieti kwa wakati mmoja, hivyo kwenda kinyume na taratibu za utawala bora.

Mheshimiwa Spika, ili kutimiza matakwa ya utawala bora, ni vyema sasa Mwenyekiti wa Tume abaki na jukumu la kusimamia vikao vya Tume na majukumu yote ya kiutendaji yawekwe chini ya Mkurugenzi Mtendaji. Hii ni pamoja na kiongoza sekretarieti ya Tume. Mfumo uliokuwepo sasa una upungufu wa kiutendaji kwa sababu inakuwa vigumu kwa kiongozi huyo huyo kutekeleza na kusimamia yeye mwenyewe.

Vikao vya Tume, mfumo uliopo sasa hauruhusu Tume kuunda Kamati za Kiutendaji, Tume inafanya vikao bila ya kuwa na Kamati ndogo, hali inayowezesha kusababisha kutojadili masuala ya kitaalam kwa undani ili kuboresha ufanisi wa Tume. Sheria iliyopo sasa haijatoa nafasi kwa Tume kuanzisha Kamati zake. Vigezo vya uteuzi wa Makamishina wa Tume, Kamishina huteuliwa na Waziri mwenye dhamana. Kigezo peke cha uteuzi ni utayari wa kujitoa kwa ajili ya kuitumikia Tume na shauku ya mtu binafsi katika kuongoza mapambano ya kuzuia na kudhibiti UKIMWI. Sheria inayotumika sasa haijatoa vigezo vya kutosha. Kwa mfano, kigezo cha uwakilishi elimu na uwezo wa mtu katika kuyaelewa masuala ya UKIMWI kwa kina.

Mheshimiwa Spika, vyanzo vya mapato, vyanzo vya mapato ya Tume ni bajeti ya Serikali, michango wa washirika wa maendeleo, mikopo nafuu pamoja na zawadi mbalimbali zinazotokana na utekelezaji wa shughuli za Tume kwa mujibu wa sheria. Kwa sasa vyanzo vya fedha kwa shughuli za UKIMWI nchini zinajumuisha bajeti ya Serikali ya Tanzania ambayo ni wastani wa shilingi bilioni 10 kwa mwaka. Sekta binafsi hutoa shilingi bilioni sita kwa mwaka na washirika wa maendeleo huchangia shilingi milioni 400 kwa mwaka. Wachangiaji wakuu wakiwa ni Serikali ya Marekani, Mfuko wa Dunia, Canada, Denmark, Ujeruman, Sweden, Ubeligiji, Benki ya Dunia na Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Spika, aidha, watu binafsi huchangia wastani wa shilingi milioni 60 kwa mwaka kama gharama ambazo kaya hutumia kumhudumia mgonjwa wa UKIMWI kwa kumpatia lishe, dawa za magonjwa nyemelezi na huduma nyingine zinazohitajika kwa mgonjwa. Kwa muda mrefu Tanzania imekuwa ikitegemea kwa kiasi kikubwa fedha za washirika wa maendeleo kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa shughuli za mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI nchini. Hali hii inaliweka Taifa katika utegemezi mkubwa na hivyo kuweza kusababisha athari kubwa ikiwa ni pamoja na vifo vingi iwapo washirika wa maendeleo watajitoa au kupunguza kusaidia shughuli za kudhibiti UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, madhumuni na sababu ya kuleta Muswada huu Bungeni, Muswada huu unakusudia kufanya marekebisho katika Sheria ya Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania, Sura namba 379. Marekebisho haya pamoja na mambo mengine yanakusudia kuweka na kuunda mfumo mzuri wa kisheria utakaoongoza Tume ya Kudhibiti UKIMWI kwa weledi na utaalam unaotakiwa huku nchi yetu ikiendana na hali halisi la tatizo la UKIMWI jinsi liliyuo sasa nchini.

Mheshimiwa Spika, aidha, Muswada huu pia unakusudia kuanzisha Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI, kwa lengo la kuhakikisha Serikali inazingatia upatikanaji wa rasilimali fedha na rasilimali nyingine katika kutekeleza shughuli zinazohusiana na VVU na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania; baada ya maelezo hayo ya jumla naomba sasa kwa ruhusa yako niwasilishe Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI ambao umegawanyika katika sehemu kuu mbili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza, sehemu hii inahusu jina la sheria inayopendekezwa ambayo itasomwa kwa pamoja na Sheria ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI, Sura ya 379.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili, sehemu hii ina masharti yanayopendekeza marekebisho katika vifungu mbalimbali vya sheria hii. Kifungu cha (2) na (3) kinapendekeza marekebisho ya misamiati na tafsiri ya maneno mbalimbali yanayohusiana na Tume VVU na UKIMWI kama yanavyosomeka kwenye sheria. Baadhi ya maneno ni mapya na yameongezwa ili kukidhi marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha (4) hadi (7) kinakusidia kurekebisha vifungu vya (6), (7) na (8) vya sheria. Marekebisho yanayopendekezwa yanaainisha masharti yanayohusu muundo wa Tume kwa kutengenanisha kofia na kutambua kwa kuwepo kwa Mweyekiti wa Tume.

Mheshimiwa Spika, uteuzi na sifa za Kamishina wa Tume umerekebisha kwa kuongeza sifa ya elimu na uwezo wa kushughulikia masuala ya VVU na UKIMWI. Hali kadhalika marekebisho haya yanaongeza sababu ambazo zitapelekea Kamishna kuondolewa katika nafasi yake, marekebisho pia yanaipa mamlaka Tume kuunda Kamati za Tume kwa adhima ya kuleta ufanisi wa utendaji wa Tume.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha (8) hadi 13 kinapendekeza marekebisho katika kifungo cha (9) hadi 13. Marekebisho hayo yana lengo la kuingiza kichwa cha habari kipywa cha Sehemu ya Tatu ambacho kitasomeka usimamizi wa shughuli za Tume. Hali kadhalika marekebisho haya yanaingiza nafasi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Tume, Uteuzi wa Majukumu yake na Mamlaka ya Nidhamu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo vifungu hivyo pia vinapendekeza kuanzishwa kwa Kamati ya VVU na UKIMWI katika sehemu za kazi ambazo zitakuwa chini ya usimamizi wa Mtendaji Mkuu wa Taasisi za Umma na Binafsi. Hii imetokana na baadhi ya Taasisi kutotekeleza kikamirifu program za UKIMWI mahali pa kazi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 14 kinaongeza Sehemu pia ya Nne ambayo inafanya marekebisho yanayolenga kuanzisha kwa Mfuko utakaojulika kama "Mfuko wa Udhamin wa UKIMWI". Sehemu hii inamaanisha Uteuzi wa Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi ya Udhamin ambayo itasimamia Mfuko wa UKIMWI na kazi zao. Sehemu hiyo pia inaonesha mjumuisho wa Wajumbe wa Bodi ambao watatoka katika sekta sita tofauti. Sehemu hii pia inaonyesha usimamizi wa Mfuko, vyanzo vya fedha za Mfuko, mgawanyo wa fedha na masuala mengine ya Mfuko. Sheria pia inaelekeza kuwa taarifa za ukaguzi wa Mfuko zitawekwa wazi na kuwasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 15 kinaongeza jedwali kwenye Sheria. Marekebisho hayo yanaingiza Bodi ya Mfuko wa Udhamin wa UKIMWI katika katika Sheria na kuainisha haya masuala ya kiutendaji ya Bodi ikiwemo idadi ya vikao vya Bodi na uendeshaji wake.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Muswada unapendekezwa kufanya marekebisho ya Sheria ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI ili kupata matokeo chanya na matokeo hayo yatakuwa kama ifuatavyo:-

Kuimarika kwa shughuli za uratibu wa muitikio wa Kitaifa dhidi ya UKIMWI; kuwepo na muongozo thabiti wa utaratibu wa wadau wote katika utekelezaji wa udhibiti wa UKIMWI nchini na Serikali kuanza kuchukua jukumu la kutafuta rasimali kwa ajili ya kudhibiti UKIMWI kwa kuanzisha Mfuko wa UKIMWI ambaa kwa kiasi kikubwa utasaidia kupunguza utegemezi.

Mheshimiwa Spika, endapo Bunge lako Tukufu litapitisha Muswada huu kuwa Sheria na Mheshimiwa Rais akaridhia Sheria hii itanza kutumika Tarehe 1 Julai, 2015.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kuchukua fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge ambaa wamekuwa mstari wa mbele kama viongozi wa jamii katika harakati za kupiga vita unyanyapaa na ubaguzi dhidi ya watu wanaoshi na VVU na UKIMWI, kuujadili na kuupitisha Muswada huu ili hatimaye uwe sheria. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu kwako kwa mara nyine kwa kusimamia kwa ukamirifu mchakato wa kufanya marekebisho ya Sheria ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI. Nina imani kwamba, kwa uongozi wako, Waheshimiwa Wabunge watujadili na hatimaye kuupitisha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofij*)

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Ahsante. Muswada umeungwa mkono.

Sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia Muswada huu.

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O - MWENYEKITI WA KAMATI YA MASUALA YA UKIMWI NA MADAWA YA KULEVYA: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, (*The Tanzania Commission for AIDS (Amendment) Act, 2014*).

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kupokea kazi ya kushughulikia Muswada huu, kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1) ilianza kuufanya kazi kwa kuainisha aina ya wadau na kuwaalika kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 84(2) na Kanuni ya 117(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Wabunge wote kwa kuniamini na kunichagua bila kipingwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge hili Tukufu. Naomba kuahidi kuwa nitaifanya kazi hii, kwa uadiifu mkubwa kwa mujibu wa Katiba na Kanuni za Bunge lako Tukufu. Pia nawashukuru Wanawake wote wa Mkoa wa Iringa na wananchi kwa ujumla kwa kuendelea kunipa ushirikiano na kuniamini, nawaahidi sitowaangusha.

Mheshimiwa Spika, Tarehe 15 Januari, 2015, Kamati ilikutana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge) katika Ukumbi wa Saadani uliopo katika Jengo la Mikutano ya Kimataifa la Mwalimu Julius Nyerere Dar es Salaam na kupokea maelezo kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, katika maelezo yake, Mheshimiwa Waziri alieleza Kamati kuhusu mapendekezo ya marekebisho yanayokusudiwa kufanya katika Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania. Muswada huo unapendekeza

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kurekebisha Sheria iliyopo ili kuondoa upungufu uliojitokeza wakati wa utekelezaji wake, kubadilisha muundo wa Tume ili kutenganisha majukumu ya Makamishna na Watendaji wa Tume.

Mheshimiwa Spika, hivyo, Muswada unaopendekezwa utaanzisha nafasi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ambaye atakuwa Mtendaji Mkuu wa Sekretarieti na Katibu wa Tume atakayeteuliwa na Mheshimiwa Rais chini ya utaratibu wa ajira katika Utumishi wa Umma. Pia Kutoa mamlaka kwa Tume kuunda Kamati zake na kuanzisha Mfuko wa Kudhibiti UKIMWI Tanzania Bara (*Tanzania AIDS Control Trust Fund*).

Mheshimiwa Spika, vile vile Kamati ilielezwa kuwa, Muswada huu ukipitishwa kuwa Sheria utasaidia kufanikisha mambo muhimu yafuatayo:-

Kuimarika kwa shughuli za uratibu na mwitikio wa Kitaifa dhidi ya mapambano ya UKIMWI; Kuwepo na mwongozo thabiti wa uratibu wa wadau wote katika utekelezaji na udhibiti UKIMWI nchini; na kuongezeka kwa rasilimali katika kudhibiti UKIMWI nchini baada ya kuanzisha Mfuko wa UKIMWI ambaa utasaidia kwa kiasi kikubwa katika kupunguza utegemezi mkubwa kwa wadau wa maendeleo uliopo sasa.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa Muswada huo unatendewa haki, Kamati ilikutana na Wadau kutoka katika Taasisi na Asasi mbalimbali zinazojihusisha na masuala ya UKIMWI ili kupata maoni yao kuhusu Muswada husika.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati yangu ilizingatia na kufanya kazi maoni ya Wadau wote kwa uzito unaostahili na kwamba, maoni yao yaliisaidia Kamati katika kutoa ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Muswada; ili kutoa maoni na ushauri wenyewe tija kwa Bunge lako Tukufu, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa Muswada huu. Katika kutekeleza jukumu hili, Kamati ilitaka kujiridhisha na mambo kadhaa muhimu katika mchakato wa utungaji wa Sheria bora. Mfano, Kamati ilitaka kujua asili ya wazo la mapendekezo ya marekebisho kwenye Sheria husika; Sababu na athari ya tatizo linalokusudiwa kutatuliwa kwa marekebisho yanayopendekezwa; Aina ya dosari inayosahihiswa kwa mapendekezo hayo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza hadi ya Nne. Sehemu ya Kwanza inahu Jina la Muswada unaofanyiwa marekebisho. Sehemu ya Pili hadi ya Tatu inahu mapendekezo ya marekebisho ya jumla kwenye Sheria iliyopo kama ifuatavyo:-

Moja, Ibara ya (3) inapendekeza marekebisho ya kifungu cha tatu kwa kutoa maana ya maneno yanayohusiana na masuala ya UKIMWI kama vile AIDS, HIV, ARV, Executive Director, HIV and AIDS focal person, recipient, thematic area na maana ya maneno Minister.

Ibara ya (4) inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha (6) cha Sheria iliyopo kuhusiana na muundo wa Tume, uteuzi na sifa za Makamishna. Ibara ya (5) inakusudia kufanya marekebisho katika kifungu cha (7) kinachohusu muda wa utumishi na jinsi ya kumwondoaa madarakani Kamishna. Ibara ya (6) inapendekeza kuongeza kifungu kipycha cha 7A katika Sheria iliyopo ambacho kinatoa mamlaka kwa Mheshimiwa Rais au Waziri mwenye dhamana kuwa ndiye chombo cha mamlaka ya nidhamu kwa Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume.

Ibara ya (7) inapendekeza marekebisho katika kifungu cha (8) cha Sheria kwa kufuta neno "Mtendaji" kabla ya neno "Mwenyekiti". Ibara ya (8) inapendekeza kuongeza kifungu kidogo cha (4) katika kifungu cha (9) cha Sheria ambacho kitaipa Tume mamlaka ya kuwa chombo cha nidhamu kwa Watumishi wa Tume. Ibara (9) inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 10 cha Sheria kwa kuongeza neno "Kamati" baada ya neno "Idara".

Ibara 10 inapendekeza marekebisho ya Sehemu Tatu kwa kufuta kichwa cha maneno "sekretarieti" na kuweka maneno "Menejimenti ya Tume". Ibara ya 11 inapendekeza marekebisho kwa kuingiza kifungu kipycha 11 kinachohusu uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Tume. Ibara ya 12 inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 11 cha Sheria kwa kufuta maneno "Executive Chairman" na badala yake kuweka maneno "Executive Director".

Ibara ya 13 inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 13 kwa kufuta maneno "guidelines issued by the Commission" na badala yake kuweka maneno "regulations issued by the Minister". Aidha, Ibara hii inapendekeza kuongeza vifungu vidogo vya (3) na (4) katika kifungu cha 13 cha Sheria.

Ibara ya 14 inapendekeza marekebisho kwa kuongeza sehemu mpya ya Trust Fund yenyevifungu 12A, 12B, 12C, 12D, 12E, 12F na 12G. Vifungu vyote kwa ujumla wake vinahusu uanzishwaji wa Mfuko wa UKIMWI, Bodi ya Mfuko; vyanzo vya mapato ya Mfuko na matumizi ya fedha za Mfuko. Ibara ya 15 inapendekeza marekebisho kwa kuongeza Jedwali.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati; kabla ya kutoa maoni ya Kamati, naomba kutambua na kuipongeza Serikali kwa juhudhi na utayari wake wa kuandaa na kuwasilisha Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI kwa wakati muafaka Bungeni ili Bunge liweze kuupitisha kuwa Sheria.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchambua Muswada kwa kuzingatia maoni yaliyotolewa na Wadau mbalimbali Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri kwa Serikali ili kuuboresha Muswada huu kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza ya Muswada. Katika Sehemu ya Kwanza ya Muswada inayohusu masharti ya awali na ina Ibara moja tu inayoelezea jina fupi la Muswada, Kamati ina maoni kuwa Ibara hiyo inajitosheleza, hivyo ibaki kama ilivyo kwenye Muswada.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada. Katika Sehemu hii inayohusu masharti ya jumla yenyevifungu 11 kuanzia Ibara ya (2) mpaka 12, Kamati ina maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Ibara ya (3) ya Muswada inahusu marekebisho ya kifungu cha (3) cha Sheria ya Tume ambapo inapendekeza kuongeza tafsiri ya baadhi ya maneno muhimu yaliyotumika katika Sheria ili kuifanya Sheria iweze kueleweka kiurahisi na watumiaji. Mfano, Muswada unapendekeza kuingiza tafsiri ya maneno, ARVs, Chairman, Executive Director, HIV and AIDS, Local Authority, recipient, thematic area na maneno mengine ambayo yanaonekana kwenye Muswada huo.

Mheshimiwa Spika, Kamati baada ya kupitia na kuchambua Ibara hii kwa ujumla wake, inaafiki mapendekezo ya tafsiri zilizotolewa kwani zimefafanua kwa mapana maneno husika na kuyafanya yaeleweke kwa ufasaha na watumiaji wa Sheria kuliko ilivyokuwa kwenye Sheria ya awali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya (4). katika Ibara hii Serikali inapendekeza kufanya marekebisho kwenye kifungu cha (6) cha Sheria mama kinachohusu Muundo wa Tume. Katika kifungu hicho Serikali inapendekeza kufuta na kuandika upya kifungu kidogo cha (1) na (2). Marekebisho hayo yanalenga kuongeza idadi ya Wajumbe wa Tume kutoka Wajumbe 10 wa awali hadi Wajumbe 11. Aidha, marekebisho hayo yanafuta dhana ya Mwenyekiti wa Tume kuwa na kofia ya utendaji. Marekebisho mengine katika Kifungu hiki yanalenga kuainisha vigezo vya kuzingatia wakati Waziri mwenye dhamana anapoteua Wajumbe wa Tume.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu baada ya kuchambua Ibara hii imebaini kuwa, Muswada huu haujaweka wazi utaratibu na masharti mengine kuhusu upatikanaji wa Makamu Mwenyekiti. Hivyo, Kamati inashauri kuwa Serikali iongeze kifungu kinachoweka masharti kuhusu nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa Tume na upatikanaji wake.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inashauri Serikali iweke kifungu kinachoweka utaratibu wa upatikanaji wa Wajumbe wa Tume. Mfano, Sheria itamke wazi kuhusu uwiano wa kijinsia, taasisi ambazo Wajumbe wa Tume watatoka badala ya kumwachia Waziri mwenye dhamana kuteua Wajumbe kwa kadiri inavyompendeza yeye kwa utashi wake.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya (5) inakusudia kufanya marekebisho katika kifungu cha (7) cha Sheria. Marekebisho hayo yanahusu muda wa utumishi na namna ya kumwondoa Kamishna wa Tume. Ibara hii pia, inapendekeza kufuta neno "reappointment" kwenye Ibara ya 5(a) na badala yake kuweka neno "one more term". Aidha, Ibara hii inapendekeza kuongeza sababu ambazo zinaweza kupelekea Kamishna kukoma kuwa Mjumbe wa Tume. Sababu hizo ni kifo, kushindwa kumudu majukumu kwa sababu za kiafya au kwa sababu nytingine yeyote ambayo Mamlaka ya Uteuzi itaona inafaa.

Mheshimiwa Spika, Kamati baada ya kupitia mapendekezo katika Ibara hii, inaunga mkono mapendekezo hayo kwa kuwa yanalenga kuondoa upungufu uliojitokeza wakati wa utekelezaji wa Sheria iliyopo.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya (6). Ibara hii ya Muswada inapendekeza kuongeza kifungu kipyä ambacho kinatoa mamlaka kwa Mheshimiwa Rais kuwa Mamlaka ya nidhamu kwa Mwenyekiti wa Tume. Aidha, Ibara hii inatoa mamlaka kwa Waziri mwenye dhamana kuwa Mamlaka ya nidhamu kwa Wajumbe wa Tume.

Mheshimiwa Spika, Kamati inayaunga mkono mapendekezo hayo kwani yanalenga kuboresha utendaji kazi wa Tume ili kuleta tija na ufanisi zaidi katika utekelezaji wa shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya (7) hadi ya 10. Ibara hizi za Muswada huu zinapendekeza kufanya marekebisho madogo madogo kwenye Sheria. Marekebisho hayo yanalenga kuondoa kasoro mbalimbali zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Sheria kama inavyoonekana katika Muswada husika.

Mheshimiwa Spika, kimsingi baada ya kupitia na kuchambua mapendekezo katika vifungu hivyo imeridhika nayo na kuyakubali kama yalivyopendekezwa kwenye Muswada.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 11. Ibara hii ya Muswada inapendekeza marekebisho kwa kuongeza kifungu kipyä cha 11 kinachohusu uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji, mchakato mzima wa uteuzi wake na utaratibu wa kuziba nafasi pale inapotokea kuwa wazi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono mapendekezo ya kifungu hiki kipyä kwani kinalenga kumpunguzia majukumu ya utendaji Mwenyekiti wa Tume ili aweze kubakia na jukumu la kusimamia Sera na Mipango ya Tume pekee. Aidha, Kamati inaona kwamba, kuanzishwa kwa nafasi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Tume itasaidia kuongeza tija na ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Tume.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 12. Ibara hii inapendekeza kufanya marekebisho madogo katika kifungu cha 11 cha Sheria kwa kukipa kifungu hicho namba nyingine ya 11B designating section 11 as section 11B. Aidha, Ibara hii, inapendekeza kufuta maneno "Executive Chairman" popote yanapoonekana katika Sehemu ya Tatu ya Sheria na badala yake kuweka maneno "Executive Director".

Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono mapendekezo hayo katika Ibara hii kwani Sehemu ya Tatu ya Sheria inahusu Sekretarieti ambayo kwa sasa ilikuwa ikifanya kazi chini ya Mwenyekiti Mtendaji. Hivyo, kwa kuwa Muswada huu unapendekeza kumwondolea Mwenyekiti wa Tume majukumu ya kiutendaji, Ibara hii ya Muswada inapendekeza kuwa Sekretarieti ya Tume iwe chini ya Mkurugenzi Mtendaji kwa kuwa ndiye kiongozi mkuu wa Tume kwenye masuala ya utendaji.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 13. Ibara hii ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 13(2) kwa kufuta maneno "guidelines issued by the Commission" na badala yake kuweka maneno "regulations issued by the Minister". Aidha, Ibara hii inapendekeza kuongeza vifungu vidogo vya (3) na (4) katika kifungu 13 cha Sheria. Vifungu hivi vinapendekeza kuanzishwa kwa Kamati za UKIMWI katika Wizara, Idara na Wakala za Serikali na katika kila taasisi binafsi na kwamba wakuu wa taasisi husika watasmamia uratibu wa utekelezaji wa mipango ya Kamati za UKIMWI na kuhakikisha kwamba mipango hiyo inatengewa na kupatiwa fedha.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo katika Ibara hii kwa kuwa yanalenga kuboresha na kuondoa upungufu uliojitekeza katika utekelezaji wa mipango ya UKIMWI iliyopo hivi sasa katika taasisi binafsi na taasisi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 14. Ibara hii ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria mama kwa kuongeza Sehemu mpya ya Nne (Part IV) yenyé vifungu saba kuanzia kifungu cha 12A mpaka 12G.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 12A kinapendekeza kuanzisha Mfuko wa UKIMWI ambao utaitwa "AIDS Trust Fund". Ibara hii pia inatoa masharti kuhusu uendeshaji wa Mfuko na majukumu ya Mkurugenzi Mtendaji wa Tume kuhusu uendeshaji wa Mfuko huo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Ibara hii kwa kuwa yanalenga kuondoa au kupunguza utegemezi kutoka kwa washirika wa maendeleo kwani kwa hali ilivyo sasa asilimia 97 ya fedha zote zinazotumika nchini kwa udhibiti wa UKIMWI zinatolewa na washirika wa maendeleo yaani development partners.

Mheshimiwa Spika, utegemezi huu unaliweka Taifa katika hatari kubwa ikiwa ni pamoja na vifo vingi iwapo Washirika wa Maendeleo wataacha kuchangia katika shughuli za kudhibiti UKIMWI ikizingatiwa kwamba ukianza kutumia dawa za ARV utatumia maisha yako yote.

Nakala ya Mlando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kuwa kuwepo kwa Mfuko wa UKIMWI kutaondoa utegemezi huo na itasaidia kuongeza uwezo wa kununua dawa mfano ARVs, vifaa tiba kama vile vitendanishi, CD4 Machines, dawa za magonjwa nyemelezi na kuwezesha Tume kuweza kuratibu vyema shughuli za mapambano dhidi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 12B kinapendekeza kuanzisha Bodi ya Mfuko wa UKIMWI yaani the Board of Trustee of the Trust Fund. Kifungu hiki pia kimeweka masharti kuhusu muundo wa Bodi, Uteuzi wa Wajumbe, Katibu wa Bodi na Majukumu ya Bodi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 12B (2) kinaainisha Wajumbe wa Bodi kama ifuatavyo:- Wajumbe wawili kutoka TACAIDS; Wajumbe watatu kutoka katika Wachangiaji wakubwa yaani major donors wa Mfuko na Mwakilishi mmoja kutoka taasisi zisizokuwa za Kiserikali (NGOs).

Mheshimiwa Spika, Kamati haikubaliani na mapendekezo kuhusu Muundo wa Bodi ya Mfuko, hivyo inaishauri Serikali kufanya marekebisho ya Muswada kuhusu Muundo wa Bodi na inapendekeza Bodi iwe na Muundo ufuatao:-

Wajumbe wawili kutoka katika Sekta binafsi; Mjumbe mmoja kutoka Wizara ya Afya; Mjumbe mmoja kutoka Wizara ya Fedha; Mjumbe mmoja mwakilishi wa Wachangiaji wa nje; Mjumbe mmoja mwakilishi wa wachangiaji wa ndani; na Mjumbe mmoja kutoka katika Taasisi Zisizo za Kiserikali.

Mheshimiwa Spika, aidha, baada ya kupitia maudhui ya Ibara hii, Kamati ilibaini kuwa, hakuna kifungu kinachohusu muda wa kukaa madarakani kwa Wajumbe wa Bodi, Maslahi ya Wajumbe wa Bodi pamoja utaratibu wa kumpata Makamu Mwenyekiti wa Bodi.

Mheshimiwa Spika, kufuatia hali hiyo, Kamati inaishauri Serikali kufanya marekebisho katika Muswada huu ili kuongeza vifungu vinavyoweka masharti kuhusu muda wa kukaa madarakani kwa Wajumbe, maslahi ya Wajumbe, pamoja na utaratibu wa kumpata Makamu Mwenyekiti wa Bodi ambaye anatajwa tu kwenye jedwali kuwa ataongoza vikao vya Bodi pale ambapo Mwenyekiti hayupo.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 12C kinapendekeza vyanzo vya mapato vya Mfuko wa UKIMWI. Vyanzo hivyo ni Fedha zitakazoidhinishwa na kupitishwa na Bunge; Fedha zitakazokusanywa na TACAIDS au zitakazolipwa kwa TACAIDS kwa mujibu wa Sheria hii; Fedha zitakazotokana na mikopo, michango na misaada; Fedha zingine zitakazotokana na uwekezaji utakaofanywa na Mfuko wa UKIMWI na Fedha au mali halali zitakazopatikana kutoka katika vyanzo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kifungu hiki kilivuta mjadala mkubwa sana baina ya Serikali na Kamati baada ya Wajumbe wa Kamati kutokubaliana na vyanzo vya mapato vilivyopendekezwa katika Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa kifungu hiki ndicho kinachobeba maudhui yote ya Muswada huu. Kamati ina maoni kuwa kama kweli Serikali imeamua kuondokana na utegemezi katika kupambana na janga la UKIMWI katika nchi yetu, basi ni vyema Mfuko unaoanzishwa uwekewe vyanzo vya mapato vya uhakika ili kuhakikisha fedha zitakazohitajika

kwa ajili ya masuala ya UKIMWI zinapatikana kwa uhakika na kwa wakati na Mfuko unakuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, kimsingi, Kamati haikubaliani na vyanzo vyatapato vilivyopendekezwa katika kifungu hiki, hivyo inaitaka Serikali kutafuta vyanzo vyatapato vyatapato ya uhakika na endelevu vitakavyosaidia katika kutunisha na kuendeleza Mfuko huu kwa ajili ya kutatua changamoto zitakazoikabili nchi katika mapambano dhidi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inaishauri Serikali kuongeza kifungu kidogo katika Ibara hii kitakachoelekeza kwamba fedha zote zitakazopatikana kutokana na Sheria hii zipelekwe kwenye Mfuko wa UKIMWI na zisitumike vinginevyo (*ring fencing provision for funds collected under this Act*).

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 12(d) kinahusu matumizi ya fedha za Mfuko. Kifungu hiki kinaweka masharti kwamba fedha zitakawekwa kwenye Mfuko zitatumika kwa ajili ya mapambano dhidi ya UKIMWI Kitaifa. Aidha, inapendekezwa kuwa asilimia isiyozidi mbili (*not more than two percent of the funds collected*) ya fedha hizo zitatumika kwa ajili ya shughuli za kuratibu mapambano dhidi ya Virusi vyatapato ya UKIMWI na UKIMWI Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, kimsingi Kamati inaafiki mapendekezo ya Ibara hii. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kupitia TACAIDS kuona ni namna gani inaweza kusaidia kifedha Mabaraza ya watu wanaoishi na virusi vyatapato ya UKIMWI kwa kuwa Mabaraza haya ni kiungo muhimu kati ya TACAIDS na watu wanaoishi na Virusi vyatapato ya UKIMWI kwa ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 12(a) cha Muswada kinahusu hesabu za kumbukumbu za mfuko, Kifungu cha 12(f) kinahusu Taarifa ya Mwaka ya Bodi, na Kifungu cha 12(g) kinahusu misamaha ya kodi na malipo yote yaliyolipwa kwa mfuko.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inaunga mkono mapendekezo yote katika vifungu hivyo vinavyopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 15, Muswada unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria kwa kuongeza jedwali kama ilivyoonekana katika Muswada huu. Kamati inaafiki na kuunga mkono pendekezo hili.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Jedwali la Marekebisho liilowasilishwa na mtoa hoja ni zao la maoni na ushauri wa Kamati uliotolewa kwa Serikali wakati wa uchambuzi wa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, napenda kutoa shukrani za pekee kwa Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, Mbunge, aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge) kwa namna ambavyo amekuwa akishirikiana na Kamati yangu wakati wote alipokuwa Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Wajumbe wote wa Kamati wanamtakia kila la kheri katika dhamana mpya aliopewa na Mheshimiwa Rais ya kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge, ambaye ameteuliwa hivi karibuni kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge). Kamati yangu inaahidi kumpa ushirikiano mkubwa katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia, inampongeza Mheshimiwa George Masaju, Mbunge kwa kuteuliwa kwake na Mheshimiwa Rais kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na tunashukuru kwa ushirikiano wa Ofisi yake wakati tunachambua Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru wataalamu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Mwenyekiti wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI (*TACAIDS*) na Watendaji wake wote kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wa kuchambua Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru wadau wote waliofika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao kwa kuongea kwa maandishi, naomba nikiri wazi kuwa, maoni yao yameisaidia Kamati yangu katika kutoa maoni haya ya Kamati kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa, nawashukuru Wajumbe wa Kamati yangu kwa ushirikiano mkubwa walionipa katika uchambuzi wa Muswada huu, hatimaye kukamilisha na kuanda maoni ya Kamati kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, naomba niwatambue Wajumbe wangu. Napenda pia kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wenzangu kwa namna wanavyotuongoza. Aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashilillah, Watendaji wa Ofisi ya Bunge pamoja na Katibu wa Kamati, Ndugu Abdallah Hancha, Mshauri wa Sheria wa Kamati Ndugu Mosi Lukuvi; Msaidizi wa Kamati, Ndugu Jesca Thadei kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Sasa namwita mse maji kutoka Kambi ya Upinzani kuhusu suala hili. Eeh, bado Mheshimiwa Rajab!

MHE. RAJAB MOHAMED MBAROUK – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI-OFIGI YA WAZIRI MKUU-SERA URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, ahsante nakushukuru. Kama ambavyo alimalizia mwenzangu jana, mdogo wangu, Mheshimiwa Mnyika kukwambia *goodnight*, nami niseme tu *good morning!*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania ya mwaka 2014 (*The Commission for AIDS Amendment Act, 2014*) chini ya Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(6) Toleo la mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uhai na kuweza kusimama mbele ya Bunge hili ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Tume ya kudhibiti UKIMWI ya mwaka 2014.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa shukrani zangu kwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbewe, kwa imani yake kwangu katika kusimamia Wizara hii nyeti, na pia kwa Viongozi wote wa UKAWA kwa kutuunganisha Watanzania wote katika kupigania haki na demokrasia ya kweli hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, lakini kwa umuhimu Mkubwa ni kutoa shukrani zangu za dhati kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Ole, Pemba kwa ushirikiano wanaonipatia katika

kuhakikisha tunaingia vizuri kwenye Uchaguzi Mkuu ujao na kuhakikisha Chama chetu kinashinda kwa kishindo kikubwa

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unakusudia kufanya marekebisho katika Sheria ya Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania, Sura namba 379. Marekebisho haya yanalenga, pamoja na mambo mengine, kutenganisha majukumu ya utendaji toka kwa Mwenyekiti wa Tume. Aidha, katika kuleta ufanisi katika utekelezaji wa Mwenyekiti na kuingiza nafasi ya Mkurugenzi Mtendaji katika muundo wa Tume.

Mheshimiwa Spika, pia marekebisho yanakusudia kuanzisha Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa fedha na rasilimali nyingine katika utekelezaji wa shughuli zinazohusiana na VVU na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, hali ya maambukizi ya UKIMWI yamepungua, ikiwemo maambukizi mapya. Kupungua huko siyo kwa kiwango kama ilivyotakiwa kuwa cha asilimia saba ya mwaka 2003/2004, asiliima 5.7 ya mwaka 2001 hadi 2008 na asilimia 5.3 ya mwaka 2011 mpaka 2012. Katika miaka yote hiyo, wanawake wamekuwa na maambukizi zaidi kuliko wanaume ambapo katika ya maeneo ya Mijini maambukizi ni zaidi kuliko maeneo yale ya nje ya Miji. Hata hivyo, kwa miaka ya karibuni maambukizi kwa wanawake yameshuka kwa kiwango kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutokomeza maambukizi ya UKIMWI kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, lengo lilikuwa ni kufikia kiwango cha chini ya asilimia tano ya maambukizi ya UKIMWI kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, kutoka kwenye kiwango cha asilimia 18. Wanawake wapatao asilimia 85 ya wajawazito wanapimwa na kupatikana na maambukizi hupatiwa dawa za kinga kwa watoto pamoja na wao kutumia dawa kupunguza makali ya maambukizo ya UKIMWI.

Inaonekana kuwa maambukizi yamepungua kutoka wastani wa watoto 26,000 walioambukizwa mwaka 2009 hadi kufikia 15,000 mwaka 2012. Hii haikuwa kazi ndogo. Huduma nyangi za Mama na Mtoto kwa asilimia 93 zinaunganisha pia huduma hii ya kuzuia maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupunguza vifo vitokanavyo na Kifua Kikuu (TB) kwenye watu waishio na virusi vya UKIMWI, lengo la Serikali ni kupunguza nusu ya vifo vitokanavyo na TB kwenye watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI ifikapo 2015. Huduma za TB na UKIMWI zimeunganishwa kwa zaidi ya asilimia 90 ya huduma za afya. Kwenye watu ambao UKIMWI umechanganyika na TB, nusu yao huenda wakapoteza maisha kama hawatibiwi ipasavyo. Inakadiriwa kwamba asilimia 26 ya watu walio na maambukizi yote mawili kwa wakati mmoja wanapatiwa tiba stahili.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu za Tume ya Kudhibiti UKIMWI, kuna wastani wa watu 710,000 wanaoishi na virusi vya UKIMWI ambao wamefikia kiwango cha kustahili kuanza kutumia ARVs. Idadi ya watu wanaofikiwa na kuanza kutumia ARV imekuwa ikiongezekwa kwa kasi, hasa kuanzia 2010, ambapo lengo ni kufikia watu 700,000 ifikapo mwaka 2015 hadi 2017. Aidha, kuboresha mazingira ya ufikiwaji wa watoto ambapo kwa sasa ni wa asilimia 25, lengo likiwa ni kufikia asilimia 70 ifikapo mwaka 2017. Tayari zaidi ya watu 663,911 wamefikiwa, ambapo idadi ya wanawake ni kubwa kuliko wanaume na pia imeokekana kwamba wanaume huchelea kuanza kutumia huduma za afya za UKIMWI ikiwemo kupima na pia kuanza tiba.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba kuongezeza kwa mahitaji ya matumizi ya madawa kwa waathirika wa UKIMWI ndivyo pia kunavyopungua kwa rasilimali fedha za kupambana na kutokomeza UKIMWI ndani ya nchi yetu. Mahitaji ya fedha ni mengi, kwa mwaka 2011/2012

kumekuwa na kupungua rasilimali fedha kwa kiwango cha asilimia tisa. Kutoka mwaka 2006/2007 hadi sasa, mgao kwa Sekta ya UKIMWI kwa nchi nzima umepungua.

Wahisani wanaendelea kuonesha nia ya kutoa msaada kwa sekta hii, Serikali ya Marekani ikiongoza na kufuatiwa na Mfuko Maalum wa UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu, Umoja wa Mataifa na Serikali za Canada na Denmark.

Wastani wa asilimia 30 ya Halmashauri zimeanza kutenga fedha za UKIMWI kutohaka na makusanyo ya ndani ya Halmashauri zao. Tume ya kudhibiti UKIMWI inapendekeza kuwa kila Halmashauri ifanye hivyo ili iweze kuhudumia mayatima, wagonjwa wa majumbani, kutoa huduma za kinga ili kuboresha lishe kwa wahusika na kuwezesha wajane na mayatima kuanzisha miradi ya kujiongeza kipato na kupunguza utegemezi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuainisha ukweli huo kama ulivyobainishwa na wataalam wa masuala ya UKIMWI na ambao umeendana kabisa na madhumuni ya marekebisho ya Muswada husika, hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatahadharisha kuhusu kilio ambacho kimekuwepo cha muda mrefu kwamba fedha nyingi za UKIMWI zinatumwa na Watendaji kwenye makongamano yahusuyo namna ya kujikinga kwa watu ambao tayari wana uelewa wa janga hilo badala ya fedha hizo kuelekezwa katika kuwapatia lishe wale ambao tayari wameshathirika.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli pia kuwa kila jambo jipya au marekebisho kwenye jambo fulani yanapotokea ni dhahiri kuwa patakuwepo na upungufu kadhaa wa kiutendaji katika mfumo au jambo liilopo.

Kambi Rasmi ya Upinzani, inapenda kupatiwa maelezo ni upungufu gani wa kiutendaji ambao umejitekeza na kuleta athari katika kukabiliana na AIDS na HIV katika nchi yetu? Kwani takwimu za Tume zinaonesha kwamba maambukizi yanapungua na udhibiti umekuwa wa hali ya juu katika nyanja zote za maambukizi. Pia dawa za ARV's watumiaji wake wamekuwa wakiongezeka kila uchwao.

Mheshimiwa Spika, hii ni karne mpya ya utendaji kazi. Kama Mwenyekiti anaweza kufanya kazi ya utendaji na matokeo yake kuwa mazuri, ni kwa nini asifanye hivyo? Ni muda sasa kwa Serikali kuanza kutumia concept/dhana ya New Public Management. Kwa maana ya kuwa dhana nzima ya jinsi sekta binafsi inavyotoa huduma na Sekta ya Umma ifanye vivyo hivyo. Kama mtu anaweza kufanya kazi ya watu wawili na tija ikaonekana, ni kwanini asifanye hivyo?

Mheshimiwa Spika, baada ya Kambi Rasmi ya Upinzani kutoa maelezo ya jumla, sasa tupitie baadhi ya vifungu.

Kifungu kipyga cha 11(1) cha Muswada kinachohusu Uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Tume; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa hapa kunaweza kutokea mgogoro kwani Mwenyekiti wa Tume ni Mteule wa Rais na Wajumbe wa Tume ni Wateule wa Waziri na Mtendaji Mkuu ambaye anatakiwa awajibike kwa Bodi ya Tume naye ni Mteule wa Rais.

Aidha, Kifungu cha (6) kinachoongeza Kifungu kipyga cha 7(a) kinachohusu Mamlaka ya Nidhamu, kinasema wazi kuwa Mamlaka ya Nidhamu ya Mwenyekiti wa Tume ni Rais na kwa Wajumbe wa Tume ni Waziri. Vivyo hivyo kwa Mkurugenzi Mtendaji, Mamlaka ya Nidhamu kwake yeche ni Mamlaka ya Uteuzi wake ambayo ni Rais.

Mheshimiwa Spika, Mkurugenzi Mtendaji sio nafasi ya kisiasa, bali ni ya Utumishi wa Umma. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri nafasi hii ipitie kwenye taratibu na kanuni

za kawaida za kuwapata Watendaji au Watumishi wa Serikali na Mtendaji awajibike moja kwa moja kwa Bodi ya TACAIDS.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli pia kuwa HIV na AIDS ni suala mtambuka na linajulikana hivyo, ndio sababu kila sekta inatenga fedha kwa ajili ya masuala mtambuka likiwemo suala hili la UKIMWI.

Kifungu cha 13(b) kinachoongeza Kifungu kipy Cha (3) na (4) kinachosema kwamba, "each Ministry, Department and Agency and every private institution shall establish an HIV and AIDS Committee under this Act, and shall designate one senior officer to be an HIV and AIDS Focal person."

Kambi Rasmi ya Upinzani inaona sharti hili la lazima linaweza kuleta mtafaruku amba siyo wa lazima hasa kwenye taasisi binafsi. Huyo Afisa Mwandamizi anapatikana vipi? Je, majukumu ya ajira yake anayaacha na kupewa hayo majukumu mapya? Aidha, huyo Afisa Mwandamizi atakuwa na taaluma ya UKIMWI?

Kama tulivyosema, suala hili kuwa mtambuka inatosha na utaratibu unaotumika hivi sasa pahali pa kazi uendelee kutumika. Aidha, kifungu cha (4) kinasema kwamba, "the duties shall be to coordinate the implementation of the Institution's HIV and AIDS Committees Plans and Interventions which shall be internally funded."

Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kifungu hiki ni kuwa Tume yenyewe haitahitaji bajeti zaidi ya kulipana mishahara na posho, kwani mipango yake yote itakuwa inatekelezwa na taasisi mbalimbali za Umma na za binafsi. Kwa maana hiyo, haina maana kuanzisha taasisi hiyo ambayo itakuwa inatumia fedha za walipa kodi bure.

Mheshimiwa Spika, Sehemu mpya ya Nne inayoanzisha mfuko, Kifungu cha 12(a) (3) (b), Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuwa, kwa kuwa masuala ya UKIMWI ni masuala yanayolindwa na mikataba mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa, hivyo basi, ni muhimu kuongezwa kwa neno "and International" na hivyo kifungu kisomeke kama ifuatavyo: "Promote prevention of new infection according to the agreed priorities in the HIV and AIDS National and International response."

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 12(a)(d) kinachohusu utayarishaji wa sera na jinsi ya matumizi ya mfuko, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuwa Mkurugenzi Mtendaji atayarishie mpango wa kufanya ufuatiliaji na tathmini ya fedha za mfuko.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 12(b)(2) kinachohusu uundwaji wa Bodi ya Wadhamini wa Mfuko wa UKIMWI, Kifungu kidogo cha (c) kinasema kuwa Bodi itahusisha pia Mjumbe mmoja kutoka asasi zisizo za Kiserikali. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema ni muhimu Wajumbe kutoka asasi za kiraia wakaongezwa na kuwa wawili na kuwa katika uwiano wa jinsia ya mwanaume na mwanamke ama kiime na kike.

Kifungu cha 12(b)(3) kinachohusu uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko, kuwa Waziri ndiye atalazimika kufanya uteuzi huo kutoka mionganoni mwa Wajumbe; Kambi Rasmi ya Upinzani inaona itakuwa ni vyema kama Wajumbe yenyewe watakaa na kuteua Mwenyekiti wao badala ya jukumu hilo kuwa ni lazima kufanywa na Waziri.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 12(c) kinahusu fedha za Mfuko wa Wadhamini, kifungu kidogo cha (a) kinasema kuwa, "such sum of moneys as may be appropriated by Parliament."

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Ukiangalia kifungu cha 15(a) cha sheria mama, kinasema kuwa Tume itapata mgawo kama utakavyokuwa umeotishwa na Bunge. Kwa mujibu wa Muswada huu wa Sheria, msimamizi mkuu wa fedha hizo za Tume na Mfuko, ni Mtendaji Mkuu wa Tume.

Aidha, kwa kuwa suala la UKIMWI ni suala mtambuka na hivyo kila Wizara inatenga bajeti kwa ajili ya UKIMWI, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka ufanuzi kuhusiana na fedha hizo ambazo kwa mujibu wa sheria zinatakiwa kupelekwa kwenye Tume ambayo kwayo imeunda taasisi nyingine ndani yake kwa mujibu wa Sehemu ya Nne ya Muswada huu wa marekebisho ya sheria.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 12(e) (1)(c) kinachosema kuwa Bodi ya Wadhamini itafungua akaunti moja au zaidi katika Benki kwa ajili ya malipo; nakinukuu. Establish one or more separate accounts in a Bank into which all moneys received by the Trust Fund shall be paid.

Kambi Rasmi ya Upinzani ina wasiwasi, kwani kwa mujibu wa Muswada huu fedha zinazoweza kuwa zinapatikana zaweza kuwa nyingi. Hivyo kuwa na akaunti za Benki nyingi inaweza kupelekea wizi au ubadhirifu. Tahadhari hii ni kutokana na ushauri wa CAG (Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali) kuhusiana na Halmashauri za Wilaya kutokuwa na akaunti za Benki nyingi, jambo ambalo lilikuwa ni kitovu cha wizi na ujisadi.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 12(g) kinachohusu msamaha kwa ushuru wa bidhaa na kodi mbalimbali zinahusu utendaji kazi wa Mfuko, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa tahadhari au angalizo kuhusiana na wahusika kutumia fursa hiyo ya misamaha ya kodi kwa maslahi yao binafsi kama ambavyo imekuwa ikifanyika.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani katika kupitia Muswada huu hasa katika jedwali linalotoa utaratibu wa jinsi Bodi hii ya wadhamini itakavyokaa na kuendesha shughuli zake, hakuna kifungu chochote kinachoeleza uhai wa Bodi hii ya wadhamini ni muda gani. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kipindi cha uhai wa Bodi kiwe ni kile ambacho Mtendaji Mkuu wa Tume atatakiwa kukaa kabla ya kuongezewa kama sheria inavyotaja.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kwa dhati inavipongeza vyombo vya habari vya ndani kwa namna ambayo hutoa elimu na kuhabarisha Umma juu ya madhara yatokanayo na maradhi haya, njia za kujikinga na pia namna ya kuzuia maambukizi mapya.

Mheshimiwa Spika, kipekee tunawapongeza walio tayarisha na kutoa tangazo lisemalo, "Tanzania Bila UKIMWI, Inawezekana," bila ya kusahau wadau wote ambao hupiga vita maambukizi ya maradhi haya.

Mheshimiwa Spika, pia nachukua nafasi hii kukupongeza wewe binafsi, lakini nampongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Mhagama, mama wa kazi mama wa nguvu, kwa namna ambavyo kwa kweli ameshughulikia na amesimamia misaada hii. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (Kicheko/Makofij)

SPIKA: Ama kweli! Ahsante sana. Yote hii ni kwa sababu ya UKIMWI! (Kicheko)

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyojua, hii shughuli ilikuwa ya jana, lakini kutokana na uzito wa kazi iliyokuwepo jana, hatukufanya. Kwa hiyo, tunaifanya leo na mkiangalia Order Paper bado tuna kazi nyingine. Kwa hiyo, nitakaowataja wanaweza kuwa wachache zaidi kuliko tulivyotegemea.

Namwita kwanza Mheshimiwa Diana Chilolo, atafuatiwa na Mheshimiwa Maria Hewa, halafu Mchungaji Mwanjale.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kukupongeza wewe binafsi kwa kazi nzuri unayoifanya hapa Bungeni.

Pili, nichukue nafasi hii niungane na mchangiaji aliyemaliza kuzungumza, kweli Mheshimiwa Waziri tuliyempata kwenye Wizara hii, ni Mama wa kazi na ni Mama wa nguvu. Sisi wanawake wenzako tunapata faraja, tunajivunia na tunashukuru kwamba umekuja wakati muafaka. Tunaamini haya tunayoyajadili sasa utayatekeleza kwa nguvu zako zote na yatazaa matunda yanayotarajiwa na Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watanzania. (Makofii)

Vilevile nichukue nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI pamoja na Mwanasheria wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI na sio mwingine ni Betty Kaghanda; Mwenyekiti Mtendaji mnafahamu ni Dkt. Fatma Mrisho. Kwa kweli Dkt. Fatma Mrisho pamoja na Mwanasheria, wanafanya kazi nzuri sana. Katika Muswada huu wametoa mchango mkubwa sana, naamini ndani ya Serikali na pia ndani ya Kamati. Mwenyezi Mungu awajaalie sana. Ninaamini mtaendelea kufanya hivyo kwa maslahi ya Watanzania. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, nitumie nafasi hii sasa nijikite kwenye Muswada ulio mbele yetu. Kwanza kabisa, naomba nizungumzie suala ambalo lipo ndani ya Muswada nalo ni suala la kutenganisha cheo cha Mwenyekiti Mtendaji.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika, Mwenyekiti Mtendaji kuwa na kofia mbili ni tatizo. Mwenyekiti ni mtu anayeongoza Tume na kuongoza Makamishna. Lakini unapokuwa na Mwenyekiti ambaye ni Mtendaji pia anawaongoza ninyi Makamishna, ni kazi sana kumhoji mtu kama huyo kwa sababu tayari ameshakuwa Kiongozi wako. Ni bahati ya pekee mpango wa Mwenyezi Mungu tumepata Mwenyekiti Mtendaji Mama mwenye busara, Mama makini na ambaye siku zote amekuwa tayari kushauriwa. La sivyo tungeweza kufanya kazi kwa taabu katika Tume hiyo. Tumshukuru Mungu sana Mama huyu amekuwa tayari siku zote kushauriwa na kufanya yale anayoshauriwa, ndiyo maana mpaka sasa hivi Tume inafanya kazi vizuri...

SPIKA: Nawe ni Mjumbe wa Bodi.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunikumbusha, kweli naomba ku-declare interest kwamba mimi ni Kamishna wa Tume ya kudhibiti UKIMWI. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni wakati muafaka kabisa wa kutenganisha kofia hizi kwa sababu hatutegemei kuwa na Dkt. Fatma Mrisho siku zote, kuna siku atastaafu. Anaweza kuja mtu ambaye ni mbabe, Makamishna watamshauri vipi mtu wa namna hiyo, wakati ni Mtendaji na ndiye Mwenyekiti anayeongoza Makamishna? Itakuwa ni taabu kweli kweli!

Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba sasa imefika mahali tukubali kabisa kwa moyo mkunjufu, cheo hiki kitengenishwe kiwe na watu wawili. Mtendaji wa Tume awe mwingine na Mwenyekiti awe mwingine; Mwenyekiti ateuliwe na Mtendaji ni Mtumishi wa kuajiriwa. Tukifanya hivyo, tutakuwa tumeisaidia Tume hii kufanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana, ninaamini Mheshimiwa Waziri ameshasifiwa, Upinzani wamemkubali kabisa; hili ninalosema na wao wameliona, kwa hiyo naamiini kabisa baada ya Muswada huu kuitishwa hili litachukuliwa kwa uzito wa pekee na Muswada huu utanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, naomba niongelee suala la pili, nalo ni kuanzisha Mfuko wa Taifa wa UKIMWI. Ni ukweli usiopingika kwamba Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, inafanya kazi kwenye mazingira magumu kweli kweli! Sasa hivi Tume haina fedha, mambo mengi yamekwama kwa sababu tu ya kutegemea wahisani. Hivi ndugu zangu, Serikali ya Tanzania tutategemea Wahisani mpaka lini? Mpaka hapa tulipo Serikali yetu imekuwa ikichangia 3% tu katika kuendesha Tume ya Kudhibiti UKIMWI, 97% inatokana na wahisani. Hivi kweli ndugu zangu hapa kuna seriousness ya Serikali? Hivi kweli Serikali imedhamiria kabisa kupambana na janga la UKIMWI kwa 3%?

Mheshimiwa Spika, umefika wakati sasa tuanzishe Mfuko wa Kudhibiti UKIMWI. Mfuko huu utakuwa ni Mwarobaini wa kuonyesha nia thabiti ya Serikali yetu kupambana na janga la UKIMWI, kwa sababu Sekretarieti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI itaainisha na kupeleka mapendekezo kwamba inahitaji kiwango kiasi gani cha pesa, nasi Makamishna tutapitia kuangalia fedha hizo kama ni kweli zitatosha kuendesha suala zima la UKIMWI. Ikienda Serikalini, Mama yetu hapa Mheshimiwa Jenista atasimamia kwa uwezo wake wote kuhakikisha kile ambacho sisi tumependekeza, makisio yetu yametekelizwa kwa asilimia mia moja. (Makof)

Mheshimiwa Spika, tukifanya hivyo, tutakwenda sambamba na Mataifa ya wenzetu kwamba sasa ifike mahali tuhakikishe tunatoa dawa hata kwa wagonjwa wenye CD₄ 500 kwa sababu mpaka sasa tunatoa dawa kwa wagonjwa wenye CD₄ 350. Hivi kweli tunasubiri mtu mpaka azidiwe ndiyo tuenze kumpa dawa? Ni vizuri tukianza kutoa dawa kwa watu ambao wana maambukizi lakini wana bado nguvu zao. Tukifanya hivyo tutakuwa tumesaidia nguvukazi ya Taifa, watu hawatadhoofu, wala kufa mapema.

Mheshimiwa Spika, nawaomba sana suala hili tulipitishe, Serikali ianzishe mfuko ambao utatusaidia sana Watanzania katika kuhakikisha kwamba suala la kupambana na UKIMWI linaendeshwa vizuri, kwa sababu tutakuwa tumetoa wigo mpana, Serikali itachangia lakini bado pia wahisani, siyo kwamba tutakuwa tumewakataza, watachangia, tena watachangia kwa sababu watakuwa wameona na sisi tumekuwa na nia thabiti ya kuhakikisha kwamba sasa tunapambana na UKIMWI na tunatafuta fedha. (Makof)

Mheshimiwa Spika, vilevile tutakuwa na kikapu ambacho hata Watanzania wenye mapenzi na Watanzania wenzao wenye matatizo ya maambuziki ya UKIMWI, watachangia kwa sababu wanajua wakichangia fedha hizo zinakwenda kwenye chombo gani. Vilevile tutalisaidia Bunge hili litapata namna bora ya kuhojii zile fedha zinatumikaje, kwa sababu ni lazima matumizi yatapitiwa na Kamati za Bunge na baadaye Bunge litakuwa linapitisha matumizi yao.

Vilevile, itasaidia sana kuhakikisha kwamba Serikali imetengeneza namna bora ya kutumia zile fedha. Hazitatumwi kiholela kama inavyokwenda. Fedha zinakwenda kwenye Halmahauri zetu lakini kama alivyosema mzungumzaji aliyejita, unakuta fedha nydingi zinatumika kwenye semina, vikao, warsha na kadhalika, lakini zitakuwa na namna bora ya kutumia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nashukuru sana, naunga mkono hoja. (Makof)

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mchungaji Mwanjale na baadaye Mheshimiwa Maria Hewa.

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu katika hoja hii ya Udhibiti wa Masuala ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, kwanza nakupongeza kwa kazi nzuri ambayo umeifanya hasa kuanzisha Kamati ya UKIMWI. Suala la UKIMWI ni suala ambalo limezoleka sana mionganoni mwa watu wengi lakini wewe ukaona umuhimu kabisa wa kuanzisha Kamati ili suala hili liwe zinazungumzwa kwa upana wake na liweze kueleweka vizuri kwa Taifa. Kwa hiyo, nakupongeza sana. Lakini nawashukuru wote ambao wameshughulika sana kuleta Muswada huu hasa Waziri kwa kazi nzuri ambayo anaifanya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, nataka niwaambie ndugu zangu Watanzania kwamba UKIMWI ni ugonjwa ambao upo nchini na hatuwezi kupuuza. Ni ugonjwa mkubwa na watu wengi ambao wanakosa huduma na hasa katika maeneo ya vijijini wanakufa. Naipongeza Serikali kwa mpango wake wa kujenga Zahanati kila Kijiji ambapo kwa kweli inasaidia kwa mahali ambapo kuna Zahanati, wagonjwa wanakwenda kupata huduma kule. Naomba waendelee kufanya hivyo.

Kwa hiyo, ugonjwa huu ni mkubwa na watu wanakufa, lakini sensa au data tulizonazo ni kwamba 5% ya watu wa Tanzania wana shida hii. Kwa hiyo ni watu wengi na maeneo mengine yamezidi hata hiyo ya Kitaifa, yaani 10%, 9% au 15%. Kwa hiyo, nafikiri sheria hii imekuja kwa wakati muafaka hasa katika suala la kuanzisha mfuko. Mfuko huu utasaidia sana kuokoa maisha ya watu wengi walipo Vijijini na Mijini. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa uzoefu wa nchi nydingine kama Zimbabwe, tulielezwa kwamba wanatenga 3% ya VAT kwa ajili ya kushughulikia suala la UKIMWI. Lakini South Africa wako over 90% ya fedha zao zinatumika kwa ajili ya tatizo la UKIMWI. Sisi kwetu tupo pabaya, ni 3% tu. Kwa hiyo, ina maana kuanzisha mfuko huu kutatuweka mahali pazuri. Hata kama tunapata misaada, lakini hii misaada itasaidia tu kupunguza hilo pengo ambalo sisi tunalo.

Mheshimiwa Spika, tulipokuwa Australia, Rais Mstaafu wa Marekani alizungumzia sana suala la nchi kujitegemea katika suala hili. Maana itafika mahali watu watakoma kuleta misaada hii: Je, watu wetu wafe kwa sababu ya kukosa fedha na sisi tupo na Serikali ipo? Kwa hiyo, naishukuru na kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu wa sheria hii ambayo tunaizungumzia leo. Kwa kweli ni muhimu sana kwa wakati huu kwa sababu ni kweli kabisa tatizo hilo lipo na siyo tatizo la Watanzania peke yake, lakini ni tatizo ambalo limezagaa kila mahali, yaani lipo nchi zote duniani. Lakini sisi tupo zaidi. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu ambao utasaidia sana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kusema ni seriousness ya Serikali katika Idara mbalimbali; na siyo Serikali tu, lakini idara mbalimbali na sekta mbalimbali. Tulipokuwa tukitembelea na kupita kila maeneo tuliona kuna watu wengine wapo serious kweli kweli, wanashughulikia kweli suala la UKIMWI, lakini wengine ni basi tu. Tulikuwa tunaombaa hata hii fedha kidogo ambayo inapatikana iende ifanye kazi iliyokusudiwa na siyo vinginevyo. Kwa sababu suala la UKIMWI limezoleka, watu hawaoni kama kuna umuhimu zaidi. Lakini tukumbuke kwamba watu wanakufa, sasa kifo hakina kuzoea!

Kwa hiyo, naomba kwa kweli sekta zote na Serikali ihakikishe kwamba inasimamia vizuri suala hili la fedha zote za UKIMWI kwamba zinafanya kazi ambayo imekusudiwa kwa sehemu

zote. Tuanzie hapa katika Bunge, halafu twende katika Idara zote za Serikali. Naomba tuhakikishe kwamba kazi hiyo inafanyika.

Suala lingine naipongeza Kamati kwa maoni yake ambayo iliyatoa kwa Serikali na yamekubalina. Nashukuru sana kwamba yalikuwa ni maoni, ilikuwa ni mchakato mkali sana, lakini nashukuru kwamba maoni hayo Serikali imeyachukua na imeona kuna umuhimu wa kuyaweka katika Muswada huu. Kwa hiyo, Tanzania bila UKIMWI inawezekana.

Mheshimiwa Spika, nilichotaka kusema ni kwamba tarehe 14 Julai, ambapo ndiyo siku ambayo Mheshimiwa Rais mwenyewe alikubali kuanzisha kampeni ya watu waende wakapime, hii siku naomba iwekwe maanani kabisa, kila mwaka ifanywe hivyo hivyo ili watu wakapime katika tarehe hiyo. Maana ilikuwa siyo rahisi, Mkuu wa Nchi anaweka kampeni kama hiyo halafu sisi tukaiacha hivyo hivyo tu.

Mheshimiwa Spika, naomba tarehe 14 Julai, kila mwaka na tuanzie mwaka huu huu iwe ni wakati wa watu kwenda kupima. Kama nilivyosema, watu wameshazoea, hawana shida tena ya kupima, wanaona kama ni kitu cha kawaida tu, lakini kumbe kuna umuhimu wa kwenda tena kupima tujue status zetu ziko vipi na ziko namna gani ili tuweze kukabiliana na gonjwa hili ambalo ni baya.

Kwa hiyo, Tanzania bila UKIMWI inawezekana. Naomba Serikali ihakikishe kwamba inaweka mipango mikakati ya uhakikisha ya kuhakikisha kwamba kwa kweli tarehe hiyo ambayo Rais wetu alianzisha, tunakwenda kupima. Watu kwa hiari yao waende wakapime. Nimeona katika Idara na Sekta nyingi watu wanakwenda kupima, wengine hawataki, lakini angalau wale wachache ambao wanaweza kujitokeza kwenda kupima, ni muhimu na inasaidia kuliko kuwa hivi hivi kimya. Kwa hiyo, naomba suala hilo lizingatiwe sana.

Kwa hiyo, sheria hii kwa ujumla wake, naipongeza ninaiunga mkono kwa asilimia mia moja kwamba Waheshimiwa Wabunge wote tuiunge mkono kwa sababu ni muhimu kabisa kwa wakati huu ambao kwa kweli watu wanakabiliwa na matatizo haya. Naomba kila Mbunge hapa aiunge mkono kwa sababu ni sheria muhimu kabisa kwa wakatu huu, bila kusita, itatusaidia kupunguza tatizo hili ambalo ni kubwa sana kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naunga mkono kwa asilimia mia moja Muswada huu upite. Ahsante sana. (Makofii)

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Maria Hewa, atafuatiwa na Mheshimiwa Menrad Lugola.

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii finyu na adimu ili nami nizungumze machache tu kuhusu suala zima la UKIMWI nchini, katika kuboresha sheria ambayo imeletwa mbele yetu leo.

Mheshimiwa Spika, nami ni kama mama nisije nikasahau kumpongeza mtoto, Mheshimiwa Jenista kwa speed aliyonayo ya utendaji wake katika nchi, sasa akiwa Waziri full wa Nchi, Uratibu, Sera, Uratibu na Bunge. Ona ilivyo tamu! Ninachoomba tu ni wana-Peramiko kuwa naye katika kumuunga na kumshika mkono ili speed zake zisije zikaishia njiani. Ni mtoto mzuri huyu! (Makofii)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, napenda tu kusema kwamba naunga mkono hotuba ya Mwenyekiti wetu ambaye ameisoma hapa, Mwenyekiti ambaye ni mahiri, kwa

umahiri wake, ameweza kupanda na yeye akawa Mwenyekiti wetu ndani ya Bunge humu kтуongoza. Hongera pia Mheshimiwa Mng'ong'o. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo kama mama nilisema, sasa nirudi kwenye mada ya leo ambayo tunatunga sheria kuhusu masuala ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi huwa nakwenda moja kwa moja ingawa huwa ina maumivu kidogo kusema wazi tu kwamba UKIMWI upo na unaua. Sasa turufika mahali tu pazuri sasa tufanye nini ili suala zima hili la UKIMWI tuwe nalo katika utendaji mzuri endelevu.

Mheshimiwa Spika, kipindi kilichopita nilizungumzia kwa kirefu kidogo kuhusu suala la uundaji wa mfuko na leo suala zima la mfuko limezungumzwa katika uundani wa Sheria. Ombi langu, ili mradi limezungumzwa katika uundaji wa Sheria hii, yasije yakawa maneno tu ya kuzungumza, maana kipindi kilichopita tulikuwa wategemezi wakubwa wa wafadhili kutoka nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, narudia tena, hawa watu, baadhi wameanza kujitoa. Sasa katika Sheria hii nadhani tumeona umuhimu na kwa vyovyothe vile ni lazima tuunge mkono Bunge zima hili umuhimu wa kuwa na mfuko wetu. Mfuko huu sasa ni lazima uwe ni endelevu, siyo wa kufungua tu. Uwe ni mfuko wenye pesa na uwe endelevu. Kwasababu tunaweza tukatamka tu hapa, halafu ukawa una hela za ajabu tu, legelege, hapana. Wenye pesa na uwe ni endelevu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, vile vile mfuko huu uanzishwe na bajeti yetu ya ndani. Uanzishwe ukiwa na fedha zetu ndani ya bajeti ya kipindi kijacho. Kwa maana ya mwaka 2015 /2016 kuwe na kitu kama hicho, hata bajeti yetu ya Tume nadhani tutabanana tu huko tutakapokaa kwenye Kamati tuweze kuona kwamba mifuko hii inapoanzishwa, inaananzishwa kwanza na sisi wenyewe ikiwa na fedha ili tuweze kuwa na mifuko ambayo inatia matumaini na iwe endelevu.

Mheshimiwa Spika, hilo ndilo ombi langu la kwanza kwa Mheshimiwa Waziri, naamini utarudi tu na hata kama hautakuwa katika eneo hili, lakini utakuwa mahali. Utarudi tu mwanangu! (Kicheko)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema, juu ya Mfuko huo, napenda kuongelea pia suala la Halmashauri zetu. Sisi tunapokuwa na mfuko kwetu hapa kama ngazi ya Taifa, ni vyema basi na Halmashauri, nimeisikia katika hotuba ya Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, ni wazo zuri kwamba Halmashauri zetu nazo ziwe na mifuko iwekwe katika Sheria hii. Tubanane tu tujue kujitegemea. Hamashauri zetu hizi nazo ziwe na mifuko ambayo inaweza kushughulika na masuala ya UKIMWI katika ngazi zetu za Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, fedha hizi kama alivyozungumza msomaji wetu wa Kamati, unajua kwa kawaida, mimi natoka kwenye Halmashauri pia, na ninaingia kwenye Kamati ya UKIMWI, unakuta fedha hizi zinadharaulika hata kama Serikali inatoa fedha kwenda kwenye matumizi ya UKIMWI, zinatumika tu ovyo ovyo tu, yaani kwa lolote litakalojitokeza la dharura ndiyo wanachukua humo. Sijui ni kwa nini! Ambapo wanajua kabisa kwamba wanachukua uhai wa mtu wanapositumia hizo fedha. Hapana! Kuanzia sasa, sheria ibane kabisa na itamke wazi kabisa kwamba hizi fedha ni za matumizi ya UKIMWI tu. zitoke na zibanwe kwa ajili ya matumizi hayo. Halmashauri yoyote itakayodiriki kuzigusa, awajibishwe. Iwajibishwe kabisa hiyo Halmashauri. Zibaki katika matumizi ambayo yanalenga uhai wa watu hawa tukijua kabisa kwamba sasa tunajitegema na kwa hiyo matumizi yasiwe ya ovyo ovyo, sheria iseme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, hawa tunaowaita wadau wa masuala ya UKIMWI, naomba tu Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa sasa kuweka vizuri suala zima la sheria hii, hawa wadau tunawabanaje; wenye shughuli za briefcase za mifukoni hawa, tunawabana namna gani? Watasema mimi hapa nashughulika na UKIMWI. Ukimfuatilia kwa karibu hawapo. Walio wengi hawapo.

Mheshimiwa Spika, sheria inawazungumzaje hawa watu ili twende nao pamoja? waelewekeje katika maeneo yao ili letu liwe moja kutokomeza UKIMWI? Ili msemo wa Tanzania bila UKIMWI inawezekana, tukashambulia pote katika angles zote, kweli iwe katika hali ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hayo mafupi, nakushukuru. naomba Waheshimiwa Wabunge wote, kama ilivyokuwa jana, hebu Muswada huu tuunge mkono kwa manufaa ya wenzetu, manufaa yetu sisi wengine humu ni watarajija tu watupu katika suala zima la UKIMWI. Hakuna aliyetulia duniani, wote ni waswampaji, ili mbele ya safari, sheria hii iweze kuwalinda.

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunisikiliza.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mendrad Kigola, atafuatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Spika, nami nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja hii muhimu. Vilevile napenda kutoa pongezi kubwa kwa dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa kazi nzuri anayoifanya na hii inaonekana kwa kila mtu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, Suala la UKIMWI ni suala ambalo linagusa maisha ya kila mtu na ni maisha ya binadamu. Ninachokijua ni kwamba afya ni muhimu kuliko mambo yote na kama huna afya maana yake huwezi kufanya kitu chochote. Tunaona kwamba maambukizi ya UKIMWI yanasaababisha hata uchumi wetu kudorora kwasababu Watendaji wengi wanakuwa wameathirika na haya masuala ya UKIMWI, kwa hiyo, hata uzalishaji mali unapungua.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naipongeza Tume ya Udhibiti UKIMWI Tanzania kwasababu ilikuwa inafanya kazi kubwa na tumeona *impact* yake ya kazi inayofanya. Lakini kuna sehemu moja ambayo inabidi kufanya marekebisho. Kwa mfano, Mbunge mmoja alisema Mwenyekiti na Kamishna cheo hicho amechukua mtu mmoja. Hii inadhoofisha hata utendaji wa kazi. Nami nashauri kwamba Mwenyekiti awe ni Mwenyekiti na Kamishna awe ni Kamishna ili wafanye kazi vizuri

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni suala la mfuko. Kwanza Mfuko tumechelewa kwasababu hata mimi nilikuwa nikiangalia ile Bajeti Kuu ambayo huwa tunajadili sisi Wabunge utakuta kwenye upande wa UKIMWI hakuna bajeti ambayo tunasema tunategemea wafadhili. Hili ni kosa, huwezi ukategemea mfadhili kwenye afya yako. Afya yako inabidi ujitegemee wewe mwenyewe. Kwa hiyo, nami naungana kwamba Mfuko huu ni wa muhimu sana na utasaiadia sana ili tuweze kujitegemea hasa kwa masuala ya kupata dawa za kuongeza maisha kwa waathirika.

Mheshimiwa Spika, vilevile nataka kutoa ushauri kwenye hii Tume katika uendaji wa kazi. Tumeona Tume inafanya kazi lakini bado haijashuka kule chini kwenye Vijiji; nimeona kwamba kuna Kamati za UKIMWI; nataka kushauri kwamba kwenye Kamati za UKIMWI hasa Vijijini ziwepo

kila Kijiji na Kata kuwe na Kamati ya UKIMWI pale kwasababu hizi Kamati zitasaidia sana kubaini matatizo ya watu walioathirika pale.

Mheshimiwa Spika, tumeona kwamba hata hizi dawa zinazopelekwa kwenye Vituo vyetu vya Afya, lakini lakini kuna watu wanaishi zaidi ya kilomita 50 hawawezi kufikia Kituo cha Afya.

Mheshimiwa Spika, mimi nataka kushauri, hizi dawa zishuke mpaka kwenye Zahanati. Lakini pamoa na kwamba zinatashuka kwenye Zahanati zetu, lakini bado kuna Vitongoji vingine viko mbali na Zahanati. Nataka kutoa mfano mdogo, kwamba Zahanati ya Idete na Kitongoji cha Holo au Itika ni Kilomita 60. Sitegemei mtu aliyeathirika aende Idete akapate dawa ya kuongeza maisha, hii itakuwa ni shida.

Mheshimiwa Spika, nataka nishauri kwamba dawa za kuongeza maisha zishuke mpaka kwenye Zahanati na kama kuna uwezekano, Tume itaangalia, ianzishe Kamati ambayo inaweza ikafungua vile Vituo vya Ushauri Nasaha hata kwenye Vitongoji. Siyo lazima iwe kwenye Kijiji tu, unaweza kufungua Kituo cha Ushauri Nasaha hata kwenye Kitongoji. Kuna Vitongoji vingine vina watu wengi sana, lakini hawawezi kufika kwenye Zahanati. Hilo naomba lizingatiwe.

Suala lingine Sheria iangalie vizuri sana ni masuala ya unyanyapaa. Tunaona kuna watu wananyanyapaa. Hata katika makazi, utaona watu wanaajiriwa kufanya kazi katika makampuni, eti mtu anaachishwa kazi kwasababu ameathirika. Hili ni kosa kubwa sana. Lazima sheria lazima iangalie hili suala na mtu yoyote kama anafukuzwa kazi eti kwasababu ameathirika, anashindwa kufanya kazi, wewe ukamfukuza, huyu mwajiri achukuliwe hatua na hili ni lazima liwekwe kwenye sheria likae vizuri. (Makof)

Mheshimiwa Spika, siyo kwamba hawa wanaojiri wanaanza kuwanyanyasa watu walioathirika au hawawatunzi. Mimi nataka kushauri kwamba mtu aliyeathirika inatakiwa aongezewe mshahara ili aweze kuishi vizuri. Huwezi kutoa ushauri nasaha kwa mtu ambaye hana hela, kwasababu kuishi sasa hivi inategemea fedha. Sasa utakuata makampuni yakiona mtu ameathirika, yanamwachisha kazi. Sasa hili nataka lizingatiwe. Waajiri wenyе tabia ya kuwanyanyapaa watu walioathirika, wanachukuliwa hatua na sheria iwekwe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nimeliona, watu wengi wanaoomba misaada wanasema wanaomba misaada kwa ajili ya Uelimisha Rika, yaani upite unaelimisha rika tu! Unaelimisha watu ambao tayari wameshaathirika! Sasa nataka kusema hivi, tuombe misaada ambayo inaleta *impact* kubwa kwa watu walioathirika. Kwa mfano, vituo vingi sana havina magari. Kwa mfano, magari yanatakiwa kwenye vituo vya afya; ni kwa nini tusiombé magari kwenye Vituo vya Afya kwa ajili ya kuwasaidia hawa watu kuwapelekea dawa kule wanakokaa kwenye vijiji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafadhili sisi tukiwaandikia, kwa mfano ukiandika proposal yako ukaweka gari pale, ukasema kwamba kila kijiji kiwe na gari, kimeombea mradi; mradi ule ile gari itakuwa ina-supply madawa kwenye vijiji kule, hiyo gari itasaidia sana. Kuliko wewe unaandika proposal unapewa intensive billion lakini ya kujifurahisha tu, ya kula tu, wakati yule mwathirika kule hata chakula hana, hana hata dawa. Unaenda kumwelimisha rika nani huyo?

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba tuombe fedha kwa wafadhili na sisi wenywewe katika fedha zetu za ndani ambazo sasa hivi tumeshasema kwenye bajeti hii nadhani tutaiona, wala hili siyo ombi; hili ni lazima tuliombe kwenye bajeti yetu. Lakini nataka kushauri kwamba zile fedha zitumike hata kununulia magari ya kutoa huduma ya kwanza kwenye vijiji. Hayo magari yatasaidia.

Kwa mfano, tukiwa na mobile service; nikisema mobile service maana yake zile gari zitakuwa zinapeleka dawa vijiji. Zikipeleka dawa vijiji na upimaji vijiji unakuwepo. Sasa hivi watu hawapimi kwasababu wanashindwa kwenye vituo vyta upimaji, ni mbali. Wewe mtu aende kwenye Halmashauri, aende kwenye Hospitali ya Wilaya, atembee kilomita karibu 200 au kilomita 160, atafika saa ngapi, na huyu mtu hana hela? Ni kwa nini tusianzisha mobile services katika vijiji vyetu? Hii itatusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, nadhani wale wataalamu, hata Kamishna wa UKIMWI atakuwa ananielewa vizuri ninaposema mobile services iende vijiji, upimaji vijiji ni lazima uwepo. Hili litakuwa limesaidia sana kwa watu wa vijiji.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo naomba ni la msingi sana kwenye upimaji, sasa hivi tukitaka kuangalia kuna watoto yatima wengi sana, lakini wale watoto yatima wanapewa huduma ya upimaji hata mashulen. Kule mashulen hakuna upimaji wa UKIMWI, kuna watu wanaishi kule wanashindwa hata kuanzishiwa dawa kwasababu hakuna upimaji. Kwa hiyo, tukianzisha upimaji hata mashulen watoto wale itabidi hata diet yao, kwasababu sasa hivi tumeanzisha hata chakula mashulen. Mwathirika huwezi kumpa kila chakula tu, kila siku unampa chakula chochote, ni lazima upate special diet ambayo anaweza kuandaliwa. Sasa watoto mashulen hawapimi.

Mheshimiwa Spika, nataka kushauri kwamba Sheria hii iwepo kwamba upimaji katika Shule za Msingi na Sekondari ni lazima uwepo. Haya magari yatasaidia kuwasafirisha hawa wataalamu waende kupita katika mashule ili kutoa huduma ya upimaji. Vile Vituo vyta Ushauri Nasaha viwepo hata mashulen, siyo lazima Zahanati tu, unaweza kuweka hata kwenye mashule yetu kwasababu kule kuna wataalamu, tunaweza kusema kila Mwalimu akasomea Ushauri Nasaha katika masuala ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Walimu wafundishe haya mambo! Tukisema tutegemee Manesi peke yao, hatutafanikiwa, kwasababu nchi hii haina Manesi wengi, hata Zahanati hatuna Manesi. Lakini tukisema waelimisha rika wa upimaji, tukawaelimisha hata Walimu kwa ajili ya kuwapima watoto pale shulen, hii itasaidia. Nimeona kuna watoto wengi sana hata mashulen wanaanguka. Utasikia watoto shule nzima wanaanguka, watu wanasema labda kuna majini au nini, hapana! Hebu tufuatilie hata afya za watoto hawa, unaweza kuona kuna mambo kama haya yapo, lakini kwasababu hawajapimwa,

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, dakika 15. Simama hapo hapo.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. KIGOMA A. MALIMA): Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni ya Wizara ya Fedha katika Muswada wa jana na huu. Muswada wa UKIMWI una umuhimu wa kipekee kwa hali halisi ya tunakokwenda mbele kwa mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwanza ili Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Watanzania mnaonisikia, tuelewe *the magnitude of the problem*, ule upana wa tatizo lenyewe. Pamoja na yote yanayozungumzwa na jitihada zote hizi, lakini wagonjwa wanaohudumiwa ni wagonjwa wapatao kama 600,000. Lakini kwa ujumla wake wagonjwa wanaokadiriwa ni milioni

1,400,000. Kwa hiyo, ndiyo maana nataka sana kumshukuru Mheshimiwa Mama Hewa aliposema hapa kwamba tunajiangalia lakini humu humu sisi na Watanzania wengine ambao bado hawaingia kwenye kundi hili la wagonjwa 600,000 wanaweza wakawemo kwenye wale wagonjwa 800,000.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo kwa jitihada hii kubwa iliyofanyika pia, ni kwamba kasi ya maambukizi Tanzania imepungua sana. Mwaka 2010 maambukizi kwa mwaka ule yalikuwa ni Watanzania 140,000; miaka minne baadaye 2013, maambukizi yalikuwa ni Watanzania 78,000, ndiyo ilikuwa new infected cases. Yote hii imekuja kwa ambalo wataalamu wanaita financing HIV.

Mheshimiwa Spika, kila nchi ina mkakati wake ama wa ku-finance kupitia madawa au ku-finance support programmes. Sasa lile zoezi zima la ku-finance hili zoezi, financing HIV and AIDS kwa Tanzania dawa na supporting programmes. Programu zile za kusaidia, maana kwenye suala la kupambana na UKIMWI hatuzungumzii suala la dawa tu, dawa ni section moja, bado kuna maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, mahitaji yetu yakadiriwa ili tuweze kupambana na tatizo hili kwa upana wake, ni Shilingi bilioni 800. Tunachopata kwa ujumla wetu wote ni Shilingi bilioni 400. So we are doing about on 50% to 55% ya mahitaji. Sasa kwenye hiyo Shilingi bilioni 400 na kitu tunayocheza nayo hapo, tunachopata kutoka vyanzo vyetu wenyewe ni 10% ya hii Shilingi bilioni 400 na kitu, vyanzo vingine vyote vinatokana na vyanzo vyta wahisani wa nje. Hali ya wahisani wa nje ikoje?

Tuna wahisani kwenye ile Presidential Fund ya Rais wa Marekani, alianzisha George Bush inatoa hela nyingi lakini yenewe inapeleka hela moja kwa moja kwenye Asasi hizi na shughuli zao, hazingii kwenye mtandao wa Serikali. Halafu kuna programu ambazo ni siyo za dawa. Kwa mfano, kuna kitu tunaita kwenye theory ya fighting AIDS inaitwa demand creation. Demand creation au positive behavior change, ni uwezo wa kuwa na ufadhilli wa kuwafanya watu wengi zaidi watamani kuangalia afya zao na kadhalika na nini. Sasa hiyo demand creation, kadri unapopeleka fedha nyingi zaidi kwenye programu hizo, ndiyo unapata wagonjwa wengi zaidi ambao wanaingia kwenye programu kwa mfano lishe. Kuna wagonjwa wengi wanapambana na tatizo la lishe. Kalisema Mjomba pale Mheshimiwa Kigola; kuna suala la kufiwa akina mama, kuna suala la yatima, kuna suala la uratibu na ufuatiliaji wa zoezi zima hili.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tunapata kama Shilingi bilioni 16 ama 17 kila mwaka, zilikuwa zinachangiwa na Canada na Denmark. Canada wamejitoa mwaka 2014 kwenye programs hizi, Denmark wanajitoa mwakani, 2016. Kwa hiyo, tukifika mwakani, tutakuwa na gap ya hizo Shilingi bilioni 16 ambazo zinaenda kwa ajili ya watu wengine ambao wanakaa mbali na huduma ya afya kama alivyosema Mheshimiwa Kigola. Kwa hiyo, inabidi tuwatafutie msaada wa kuwawezesha wao kwenda ku-access hizo dawa.

Mheshimiwa Spika, what is the problem if we fail? When we fail, maana yake ni kwamba dawa wanazotumia wagonjwa kwa hatua ya kwanza, zinaitwa first line drugs, ndiyo zile dawa za kwanza. Lakini ukitumia dawa halafu ukiacha kutumia hizo dawa, unaporudi dawa zile sasa mwili wako unakuwa resistant, yaani unakuwa sug. Kwa hiyo, inabidi uingie kwenye second line drugs.

Mheshimiwa Spika, zile second line drugs watalaam walikuwa wananiambia kwamba ni Marekani tu ambao wanaweza ku-afford kwenye system yao ya Umma kwa sababu dawa hizo ghamama yake ni mara name ya dawa za first line drugs. Kwa hiyo, hizi pesa ambazo zimo kwenye kuhamasisha hizi program ni zile za kuhamasisha waathirika ili wasiache kutumia dawa

at any stage. Maana wengine wanatumia dawa, wakiona miili imerudi, wamekuwa na afya nzuri, wanaacha. Wakiacha, wakirudi tena baada ya *infection* yoyote huwezi kutumia *first line drug*; na hatuna *second line drugs* kwa sababu *they are just too expensive, no one can afford them.*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, ndiyo nilitaka Waheshimiwa Wabunge wenzangu mnielewe kwamba katika mazingira haya ya sasa, suala la kuwa na Mfuko wa Taifa wa kupambana na UKIMWI, siyo suala la hiari, ni suala la lazima. Nilikuwa nataka kusema kwamba na Serikali imeridhia kuwa na mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi suala kubwa kuhusiana na mfuko huu ni vyanzo vyake. Tunafanyaje? *How do we move forward?* Kwa sababu kama mahitaji ya mfuko ni haya, amesema Mheshimiwa Kigola, wakati tunategemea vyanzo vya nje, nasi wenywewe lazima tuingize mikono yetu humo ndani. Mahitaji ya mfuko huu ni makubwa kweli. Sasa mpaka dakika hii hatujaweza kuafikiana. Tunaendelea na mazungumzo na watalaam, Ofisi ya Waziri Mkuu, kuhusu vyanzo vya mfuko huu, vinatokana na nini?

Mheshimiwa Spika, vyanzo vya mfuko huu tungefikiria labda twende kwenye VAT ili kwenye kipande cha VAT pale pawe na pesa zinazotoka asilimia ndogo pale kwenda kwenye Mfuko wa Taifa wa UKIMWI au tozo mbalimbali labda tozo kwenye mafuta au tozo kwenye nini. Lakini *all in all*, vitu hivyo vyote kwanza vina aspect ya *inflation* kwenye uchumi lakini la pili ni kwamba vinalindwa na sheria.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi tukaingia mle ndani tunasema tuweke tozo kwenye umeme, walipaji wa umeme au tozo kwenye mafuta au tozo kwenye nini bila kuingia kwenye sheria husika na kuziwekea utaratibu amba unaridhiwa na Bunge hili. Hili ndiyo maana nasema katika upande huu, vyanzo hivi hatujaafikiana, tunaendelea kuvifanyi kazi pamoja na Mheshimiwa Jenista na watu wake wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Watalaam na Kamati ya Mheshimiwa Mama Lediana Mng'ong'o ili tufike sehemu tuafikiane, tutakapovileta hapa Bungeni kwa ajili ya kupata *figure* hizo ambazo nimezitaja, mahitaji hayo makubwa Waheshimiwa Wabunge turidhie na tupime uzito wake, tuone kama tutaridhia kuweka hizi tozo kwenye maeneo mbalimbali ili mfuko huu update *financing* ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine lililokuwa limefikiriwa ni mishahara. Tulikuwa tumefikiria labda tukate asilimia kidogo kwenye mishahara ya wafanyakazi wote kwenye Sekta ya Umma. Tukasema *fine, it is a good thing, it is noble thing, jambo tukufu, zuri*. Lakini ni jambo ambalo linaonekana lina ubaguzi kwa sababu waathirika wa HIV na mahitaji ya HIV hayaendi kwenye Sekta ya Umma tu, au hayaendi kwa wafanyakazi wa Sekta ya Umma, *yana-cut across*, watu wote tunahitaji. Kwa hiyo, hilo likaonekana lina ubaguzi na badala yake sasa, ndiyo maana tukalipeleka kwenye vyanzo vingine.

Mheshimiwa Spika, lingine tulikuwa tumefikiria vyanzo vya Halmashari. Katika Halmashauri zaidi ya 150, ni Halmashauri 30 tu zinazochukua own source, pesa kidogo kwa ajili ya kupambana na janga la UKIMWI. Hata hizo bado ni ndogo kweli!

Mheshimiwa Spika, sasa tutakapokuja na mapendekezo kwamba tunakwendaje na mkakati huu, kwanza ni kutambua kwamba tuna watu wa *global fund* amba tulikutana nao. Mimi mwenywewe niliongoza ujumbe wa Wizara mwaka 2014 Oktoba na mwaka huu mwezi wa Nne wanakuja tena na katika mambo ambayo tulikuwa tunafikiria ni muhimu yawepo, ni suala la kupitisha hii sheria. Ndiyo maana hii sheria leo ina umuhimu wa kipekee. Inaonesha *commitment* ya Bunge na *commitment* ya Taifa letu kwa ajili ya kupambana na ugonjwa wa UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, *global fund wame-commit* kutoa hela kwa sura mbili; dola milioni 280 kwa kipindi cha miezi 18 ijayo kwa ajili ya HIV, dola milioni 32 kwa ajili ya Tuberculosis (TB) kwa miezi ya 24. Hii pesa dola 280 kwa asilimia kubwa zaidi ya asilimia 80 zinakwenda kwa ajili ya kununua dawa, asilimia 20 inakwenda kwenye vitendanishi; vitendea kazi, kits na kdhalika na program support na hela nyingine inaenda kwenye asasi za kiraia.

Mheshimiwa Spika, masharti yake ni nini? Kwamba hizi dola 280 kwa mwaka, hii miezi 18 nchi zote zinategemea *global fund* kupata pesa hizi; sasa Tanzania tunapata dola milioni 280 lakini ili tuzipate, lazima tuwe tume-abide kwenye concept inayoitwa *willingness to pay*.

Mheshimiwa Spika, hiyo *willingness to pay* maana yake ni kwamba kama program yote inagharimu milioni 280, sisi tutoe asilimia 15 ya zile dola 280. Asilimia 15 ni dola milioni 42. Sasa ndio tunakwenda tukijipanga kwenye bajeti yetu tuone kwamba kwa sababu ni *incremental* inakwenda inapanda, tunaweza tukaamua sasa tutoe labda ngapi. Labda tutoe dola milioni 10 kama bajeti inaruhusu, hatutafika asilimia 15 lakini tutafikia asilimia fulani ambazo zinawapa wao sababu ya kusema, basi kwa mwaka huu wa kwanza tutoe pesa hizi.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wake wa kipekee wa kupata hizi pesa za kutoka ni kwa sababu wagonjwa wapya wanaoingia hawajafanyiwa utaratibu wa kibajeti au kwa pesa hizi za *global fund* hazizingatii wagonjwa wapya wala pesa nyingine nyingine zozote. Kwa hiyo, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Kigola na wengine wote waliosema kwamba kuna umuhimu wa kipekee wa kuangalia hili tatizo na kuangalia sisi wenyewe tunajipangaje, tutakuja na mapendekezo Bungeni ya kusema namna tutakavyokabiliana kwa kiwango gani, kwa kuangalia matumizi haya na mahitaji ya fedha hizi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba uniruhusu niseme hili la *dynamics* za *pharmaceutical industry*. Hakuna nchi Sub Saharan Africa inayotengeneza ARVs. Tumekubaliana kwenye Mkutano wa SADC juzi tulipokuwa Zimbabwe kwamba tuangalie local ya capacity ya kuwa na kiwanda ndani kinachotengeneza ARVs.

Arusha wamejaribu, walikuwa wanakwenda wana-export dawa kwenda Rwanda, Burundi kile kiwanda cha Arusha na kulikuwa na pesa wamepata kutoka European Union, hatuelewi; mpaka sasa hivi Wizara ya Afya wanalifanya kazi; hatujui ni kwanini zile dawa zimesimamishwa na kadhalika. Lakini ukipata kiwanda chako mwenyewe ndani kinachotengeneza ARVs inaweza ikawa ni ukombozi fulani. Tatizo, inaweza isiwe hizo ARVs zikawa na bei rahisi zaidi au zikawa zimepungukiwa gharama kwa sababu zile re-agency na mambo mengine ya kuchanganya, bado yanatoka maeneo hayo hayo. Moja.

Kwa hiyo, kwa sasa hivi dawa hizi kwa kiasi kikubwa, hawa wanazinunua kupitia utaratibu wa PPM, hizi dola 280 zitakuja kama dawa asilimia 80 na asilimia 20 zitakuja kwa ajili ya uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, tuko kwenye hiyo *proposal* ya *regional strategy* ya kuangalia mkakati wa kikanda kama tunaweza tukawa na utengenezaji wa ARVs kwa gharama ndogo kwa nchi za Uganda, Kenya, Tanzania, Rwanda na nchi nyingine na kadhalika. Lakini bado hiyo kwa sasa hivi ni mkakati ambao upo mbali na lazima tujue kwamba kwenye mambo ya ushindani na biashara, hayo makampuni makubwa yanayotengeneza ARVs, wakikuona wewe kikampuni unanyemelea ulaji wao, pia hiyo inaweza ikawa ni issue. Kwa hiyo, kwa sasa hivi, bado jambo lote hili linazungukwa na *dynamics* hizi za wafadhili wakubwa na makampuni makubwa yanayotengeneza dawa.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Waheshimiwa Wabunge walielewe tatizo hili kwa upana wake ikiwa ni matatizo pia ya kuyapatia fedha za kupambana na tatizo hili. Naomba nahakikishieni kwamba Serikali inaendelea kufanya kazi kwa karibu na Kamati ya Bunge pamoja na wadau wengine ili tupate ufumbuzi wa haraka hasa kwenye suala hili la vyanzo vya Mfuko wa Taifa wa kupambana na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naunga mkono hoja. (Makofii)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mtoa hoja!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuhitimisha hoja hii muhimu sana ambayo iko hapa mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nadhani nianze kwa kukushukuru wewe binafsi kupitia Kamati ya Uongozi ikiongozwa na wewe mwenyewe. Uliridhia Muswada huu kwa mujibu wa ratiba ya kikao hiki cha Bunge, uingizwe hapa Bungeni na kupatiwa mjadala na hatimaye tuweze kuhitimisha kwa makubaliano ya Bunge kuwa sheria. Nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe shukrani nyingine za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati kama nilivyosema mwanzo na baada ya hotuba yangu amesoma maoni ya Kamati, ameweka msisitizo wa kutosha juu ya masuala mengi tu ambayo Serikali inatakiwa kuyazingatia ama katika utungaji wa kanuni, ama katika kuboresha jedwali, ama katika utendaji wetu wa kazi wa kila siku kwenye tatizo hili. Naomba nimshukuru sana Mwenyekiti na Wajumbe walioanda taarifa ile ya Kamati. Kuna Wajumbe mle mahiri kabisa tumefanya nao kazi kwa kiasi cha kutosha. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, namshukuru Makamu Mwenyekiti na wachangiaji wengine wote waliochangia kwa maneno, wamesema hapa. Wachangiaji wengi waliochangia hoja hii leo ni Wajumbe wa Kamati hiyo na wametoa ushauri mzuri sana. Vile vile wameshirikiana na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ambao sio Wajumbe, wametusaidia kuboresha Muswada huu na kutupa ushauri sisi kama Serikali ni namna gani nzuri ya kwenda kutekeleza majukumu yetu katika mapambano dhidi ya tatizo hili la UKIMWI kwenye nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Msemaji wa Kambi ya Upinzani, ndugu yangu Mheshimiwa Rajab. Amewasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani. Ni lazima niseme maoni yaliyosemwa na Kambi ya Upinzani kwa kiasi kikubwa yanetoa ushauri mzuri sana kwa Serikali. Ni maoni ambayo unaona kabisa ni namna gani Kambi ya Upinzani imedhamiria kuunga mkono juhudii hizi za Serikali za kupambana na tatizo hili la UKIMWI, lakini wamechukua nafasi ya kukumbusha maeneo ambayo yanatakiwa yafanyiwe kazi pia kwa haraka ili kuhakikisha kwamba mbio hizi za kupambana na tatizo hili la UKIMWI zinaweza kupelekea kuwa ni mbio za kutufikisha mahali tunapotarajia. Lakini kipekee namshukuru sana Mheshimiwa Rajab kwa pongezi alizonipa na kunitia moyo katika kazi hii mpya. Inshallah Mwenyezi Mungu na wewe akuangazie na kukuongzeza yale unayoyafikiria na ikiwezekana wote turudi tena tuweze kushauriana katika Bunge hili. Mheshimiwa Rajabu nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia na Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa maneno, kwa kweli wamenipongeza na wameipongeza pia Serikali kwa namna ya kutosha kwa jinsi tulivyojitalidi na hasa kufanya kazi kwenye eneo hili ambalo tunaliletea Muswada. Kwa niaba pia ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI naomba kuzipokea pongezi hizo na tunawahakikishia kwamba tutafanya kazi kwa pamoja na tunaomba Mwenyezi Mungu aendelee kutuongoza ili

kwa kweli tatizo hili la UKIMWI katika nchi yetu liweze kupatiwa ufumbuzi kama siyo kuliondoa kabisa, lakini tuweze kulipunguza kwa kadri tutakavyoweza.

Mheshimiwa Spika, hoja hii imechangiwa kwa maneno na Waheshimiwa Wabunge takribani nane, lakini pia imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wawili waliochangia hoja hii kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, kipindi cha takribani miaka 12, nchi yetu imekuwa ikiendelea kupambana na tatizo hili la maambukizi ya UKIMWI ama tatizo hili la UKIMWI katika nchi yetu kwa kutumia sheria ya awali. Lakini unaona kabisa kwamba sheria iliyokuwepo mwanzo imetusaidia kwa kiasi cha kutosha; na hapa ni lazima niseme, nawapongeza sana Watendaji wote wa Tume wakiongozwa na Mwenyekiti wetu Mtendaji wa Tume. Pamoja na sheria ile kuwa na upungufu ama kuwa na mwelekeo wa namna ambayo inatakiwa ifanyiwe mabadiliko, lakini imeweza kusaidia kwa kiasi kikubwa sana mapambano haya dhidi ya UKIMWI na unaona kwamba maambukizi yameweza kupungua kutoka asilimia saba mwaka 2003 mpaka kufikia asilimia tano mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, ni shida kubwa. Tatizo hili la UKIMWI hakuna ambaye hajaguswa nalo kwa namna moja ama nyine. Ni tatizo ambalo linatugusa wote. Karibu kila Mtanzania ameguswa kwa namna moja ama nyine. Sasa ni wakati muafaka wa kuona tunatakiwa kwa namna gani kukusanya nguvu zetu kwa pamoja na hasa kama sheria hii mpya itapitishwa leo.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha kama yangu Adam Malima, ametoa ufanuzi wa kutosha ni kwanini Serikali tumeamua kuleta huu Muswada ili tuanzishe mfuko ambaa utatusaidia sasa kuzuia upungufu wa upatikanaji wa rasilimali katika kuhakikisha nchi yetu inajitegemea yenye ndani na siyo kuwategemea wafadhili katika mapambano haya dhidi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, watu laki sita wapo kwenye dawa, lakini inasemekana kwa misingi ya tafiti tulizonazo ni zaidi ya watu milioni moja na kitu ambaa wanatakiwa kuingia kwenye dawa. Sasa kama hawa watu hawataingia kwenye dawa kwa muda unaotakiwa, athari zake ni kubwa sana katika afya za Watanzania. Ukishaona hiyo picha, nasi kama Serikali tusipochukua wajibu wetu wa kijiandaa mapema, hapa taarifa tulizonazo ni kwamba wafadhili watajitoa mwaka 2017.

Mheshimiwa Spika, wafadhili wanapojitoa mwaka 2017 sisi hatujajiandaa, namna gani tutafanya wafadhili wakishajitoa? Itakuwa ni kazi kubwa! Ina maana wagonjwa walioko kwenye dawa watashindwa kuendelea kupata tiba, wagonjwa wapya wanaohitaji kuingizwa kwenye dawa hawataweza kupata dawa na matokeo yake itakuwa ni janga lingine kubwa, kama siyo maafa kwenye Taifa letu, ingawa Muswada wa Maafa hauzungumzi pia tatizo hili la UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hizi ni juhudzi za Serikali kuchukua tahadhari mapema. Leo Waheshimiwa Wabunge, nawapongeza kwa sababu kila siku wamekuwa wakituagiza kama Serikali, ni kwanini hatuchukui tahadhari tunasubiri mpaka majanga yatokee? Sasa Muswada huu unakwenda kuchukua tahadhari ya kuandaa miundombinu ambayo inatusaidia kuchukua tahadhari ya kuendelea kufanya maisha ya Watanzania wanaotumia dawa hizi yaendelee kuwa ni maisha bora kwa sababu Serikali itakuwa imeshachukua tahadhari ya kuijandaa kirasilimali.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina heshima kubwa sana katika mapambano haya dhidi ya UKIMWI. Tarehe moja Desemba, 2014, Kitabu cha Guinness cha records kiliendesha

mashindano ya nchi mbalimbali kuona ni namna gani nchi hizo zimeweza kuanza kuwa na mwamko wa kupima kwa hiari.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu, katika mashindano haya katika maadhimisho ya siku ya UKIMWI Duniani Tanzania ilichukua ushindi wa kwanza. Ushindi huu ni lazima tujivunie kwa sababu unapoona Watanzania sasa wamehabarika na wako tayari kupima afya zao ili kuweza kupatiwa matibabu yanayohusiana na magonjwa nyemelezi ama kuanza kutumia dawa zitakazoweza kurefusha maisha yao ni hatua kubwa sana katika nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ziko nchi wananchi wake hawapimi na wala hawajitokezi kupata dawa. Kwa hiyo, mimi niwapongeze sana Tume, lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kuwa mfano katika suala hili la upimaji. Waheshimiwa Wabunge nakumbuka tumepima mara kadhaa, kwa hiyo, kwa pamoja tumekuwa mfano mzuri kwa Tanzania na kwa Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, lakini sisi tunaamini kabisa sheria hii itasaidia sana kuimarisha miongozo mbalimbali na taratibu mbalimbali ambazo zitatupelekea katika kuratibu shughuli za mapambano haya dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, basi mambo muhimu ambayo yamezingatiwa katika sheria hii ambayo leo tunaijadili hapa Bungeni; kubwa la kwanza ni kubadilisha muundo wa Tume kwa ajili ya kutenganisha majukumu ya Kamishina na watendaji wa Tume.

Mheshimiwa Spika, sheria hii inaenda kuweka nafasi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ambaye atabaki kuwa tu Mtendaji Mkuu. Lakini sheria hii itaweka utaratibu pia wa namna gani watumishi wa Tume hii watapatikana wakiongozwa na Mtendaji Mkuu wa Tume ili kuweza kufanya kazi za uratibu kwenye Tume yenyewe na kutengeneza pia utaratibu wa uteuzi wa Mwenyekiti wa Tume, nafasi ambayo inamtenganisha Mtendaji Mkuu wa Tume na Mwenyekiti ili kuleta utawala bora na ufanisi wa kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, lakini eneo la pili, tutakwenda kutoa mamlaka kwa Tume kuunda Kamati zake. Kwa mfumo wa zamani, uendeshaji wa vikao ndani ya Tume havikuwa na nafasi ya kuunda Kamati ndogondogo za kufanya mijadala ya kina kuhusiana na tatizo hili la udhibiti wa UKIMWI katika nchi yetu. Kwa hiyo, sheria hii sasa inaenda kutengeneza provision itakayoisaidia Tume kuunda Kamati wakati wa utendaji wa kazi na kuhakikisha kwamba, Kamati zitapata nafasi nzuri ya kujadili.

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa ni hili la kuanzisha Mfuko wa Kudhibiti UKIMWI Tanzania Bara. Mfuko huu ndio sasa utakaokwenda kusaidia shughuli nyingi sana, zikiwemo pamoja na hizo tulizosisema za kuhakikisha kwamba, Watanzania hawatakosa dawa. Na niseme tu mpaka sasa niendelee kuwatoa hofu Watanzania, dawa zipo na zitaendelea kugawiwa. Kwa hiyo, tatizo la dawa lisije kuwa ni hofu kwetu, zipo na ndio maana tunakimbizana; wafadhili watakapojitoa, tuendelee kuwa na uwezekano wa kuweza kuwa na dawa na wagonjwa wakaendelea kupata dawa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, marekebisho yatawezesha pia kuimarisha shughuli za muitikio wa kitaifa katika kufanya shughuli mbalimbali kupambana na tatizo hili la UKIMWI katika nchi yetu. Lakini tutaweka pia, miongozo thabiti na taratibu za wadau wote katika kujishughulisha na mapambano dhidi ya UKIMWI nchini.

Mheshimiwa Spika, lakini sheria hii itatusaidia kuongeza rasilimali katika kudhibiti UKIMWI nchini kwa sababu, mfuko huo si tu kwamba, utachagiwa na Serikali, lakini ni *interest* pia ya wachangiaji mbalimbali na wadau mbalimbali kuchangia katika mfuko huu na kuhakikisha kwamba, nchi yetu inaendelea kubaki kuwa salama na mapambano dhidi ya ugonjwa huu wa UKIMWI katika watu wa rika tofauti, makundi tofauti na malengo tofauti wanaendelea kupatiwa huduma zinazotakiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, nitajibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, lakini kama nitashindwa kuzijibu hoja zote, basi nyingine tutaweza kuzijibu kwa maandishi, na hivyo, jedwali hilo ambalo litakuwa na majibu ya hoja zetu, tutaliwasilisha kwenye Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikuwa inashauri kuongeza masharti kuhusu nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa Tume. Hii hoja ililetwa na Kamati na Mheshimiwa Mwenyekiti ameisoma tena hapa pia.

Mheshimiwa Spika, sasa Kifungu cha 6(3) cha Sheria Mama ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI, Namba 22 ya mwaka 2001 kinenelekeza utaratibu wa kuhusiana na nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa Tume. Kwa hiyo, kifungu hicho kimeeleza vizuri sana, *the Commissioners appointed under this paragraph ambayo nimeisema na (b) yake inasema Sub Section (a) above shall nominate from their number a Vice Chairman of the Commission.* Kwa hiyo, Kifungu hiki kwenye sheria ile ya mwaka 2001 kimezingatia pendekezo hilo la Kamati na tunaishukuru Kamati.

Mheshimiwa Spika, lakini Kamati inashauri kuongeza kifungu kitakachoweka utaratibu wa upatikanaji wa Wajumbe wa Tume. Mfano, sheria itamke wazi kuhusiana na uwiano wa kijinsia na mambo mengine yanayoendana na hayo, dhamana ya kuteua na utashi wa kuteua wajumbe hao.

Mheshimiwa Spika, ushauri huu umezingatiwa na tunasema kwamba, uwiano huo pia ni lazima utatajwa na kuanishwa katika Kanuni ambazo tutazitunga ili kuhakikisha jinsia zote ziweze kuwakilishwa wakati wa kufanya uteuzi wa group lile zima kama ilivyoinishwa kwenye marekebisho ya sheria yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini Kamati inashauri muundo wa Bodi ya Mfuko uliopendekezwa na Serikali ubadilishwe ili kukidhi mahitaji kadhaa ambayo Kamati imefikiria.

Mheshimiwa Spika, tumekubaliana na hoja hiyo ya Kamati na tumeweka mapendekezo kupitia Jedwali la Marekebisho kuonesha ni namna gani tumebadilisha muundo huo wa Bodi uwakilishi wake utakavyokuwa, na muda utakapofika basi, marekebisho yetu haya yatawekwa wazi mbele ya Bunge na Kamati itaona jinsi tulivyoafikiana na ushauri wao na jinsi tulivyofanya.

Mheshimiwa Spika, Serikali itafute vyanzo vingine vya mapato: Tumezungumza hapa na Naibu Waziri wa Fedha ameeleza. Ni kweli ni nia na azma ya Serikali kufanya hivyo na tutajitahidi sana kuona vyanzo hivyo vinapatikana, ili kwa kweli mfuko huu uwe na fedha.

Mheshimiwa Spika, jambo hili hakuna mtu anayetakiwa kulifumba macho kwa sababu, ni jambo la hatari na kama halitafanyiwa kazi, linaweza kuangamiza Watanzania wengi na hasa wale Watanzania ambao tayari wameishaanza kutumia dawa na watahitaji kuendelea kupata huduma, kama sio za dawa na huduma nyingine.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilizungumzia sana umuhimu wa taasisi zetu zote za Serikali na zisizo za Serikali kuhakikisha kwamba, zinatengeneza kamati ndani ya Taasisi zao zitakazoshughulikia masuala haya ya wagonjwa ndani ya ofisi zao.

Mheshimiwa Spika, hilo tumelizingatia sana. Ni kweli kabisa, ziko taasisi nyingine katika nchi yetu ya Tanzania na hasa taasisi binafsi, hazikuwa zikiunda kamati za kushughulikia tatizo hili ndani ya taasisi zao. Kwa hiyo, sheria hii sasa haitakuwa tena na mwanya wa kukwepa jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, taasisi hizo ni lazima zianzishwe katika kila eneo la kazi kwenye Taasisi za Serikali na Taasisi Zisizokuwa za Serikali na lengo ni kuhakikisha kwamba, Watanzania wote tunakuwa kitu kimoja katika kushughulikia tatizo hili la ugonjwa wa UKIMWI katika nchi yetu ya Tanzania, wagonjwa wapewe huduma wanazostahili, wafanyakazi waendelee kufanya kazi wakiwa na moyo wa utumishi katika maeneo yetu kwenye nchi yetu ya Tanzania na Kamati hizo zikiongozwa katika utaratibu ambao umeainishwa kwenye sheria tulioileta mbele ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani nayo ilikuwa na hoja kadhaa. Hoja kubwa ya kwanza, ilikuwa, Msemaji Mkoo wa Kambi ya Upinzani humu Bungeni alifikiri kwamba, na alisema kwamba, anadhani kutenganisha madaraka haya ya Mtendaji Mkoo na Uenyekiti wake sio sahihi sana kama Mtendaji huyo pia ni Mwenyekiti na anafanya kazi vizuri ni kwa nini tutenganishe madaraka yake?

Mheshimiwa Spika, tunachotaka kusema tu hapa ni kwamba, tunajaribu kuangalia dhana ya msingi wa utawala bora. Leo unaweza ukawa na Mtendaji ambaye ni Mwenyekiti ambaye ni muadilifu, lakini kesho unaweza ukapata Mwenyekiti na Mtendaji ambaye utendaji wake hautakuwa na vigezo hivi vya uadilifu. Kwa hiyo, ili kufanya kazi hizi zitendeke kwa uadilifu na kwa misingi ya utawala bora, sisi kama Serikali tumeona kuna umuhimu kwa kweli kabisa tutenganishe hizo nyadhifa, ili kuweka utawala bora wa kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile Mkurugenzi Mtendaji atayariske mpango wa kufanya ufuatiliaji wa tathmini ya fedha za Mfuko.

Mheshimiwa Spika, tumesema kwenye sheria hii mfuko huu kwanza utakuwa unatolewa taarifa Bungeni na utakaguliwa kama inavyokaguliwa mifuko mingine. Kwa hiyo, kwa namna hiyo basi unaona kabisa mfuko huu umepewa udhibiti wa hali ya juu na hivyo, utendaji kazi wa mfuko, ukaguzi wake na namna nzuri ya mipango ya uratibu wa mfuko itafanyiwa kazi vizuri tu kwa sababu, pia, uta-comply na sheria nyingine za fedha za nchi na hapo watendaji na wasimamizi wote wa mfuko hawatakuwa na ujanja wa kufanya jambo lingine lolote na vinginevyo sheria zitachukua hatua na mkondo wake endapo kutatokea tukio la namna hiyo la uvunjifu wa maadili katika matumizi ya mfuko.

Mheshimiwa Spika, Msemaji Mkoo wa Kambi ya Upinzani amesema pia kufungua akaunti zaidi ya moja kunaweza kusababisha wizi na ubadhirifu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Serikali tunasema kwamba, ni kweli hiyo inaweza ikatokea, lakini katika mifumo ya uratibu wa fedha katika nchi yetu ya Tanzania, huu mfuko hautakuwa wa kwanza kufungua akaunti mbalimbali kulingana na mahitaji na matumizi. Ni utaratibu ambao sasa hivi upo na unaendelea na maeneo mbalimbali ya utendaji wa kazi Serikalini kwa kuzingatia sheria za fedha ambazo tunazo. Kwa hiyo, sisi tunachoamini akaunti hizo zitadhibitiwa

kwa kulingana na taratibu na kanuni za fedha kama zinavyodhibiti na kusimamia akaunti nyingine katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge pia, wengi wamechangia na wamechangia michango mizuri tu. Mheshimiwa Diana Chilolo, Makamu Mwenyekiti, ameshukuru pamoja na ku-declare *interest* yake kama Mjumbe wa Tume, lakini ameleezea umuhimu wa Mfuko huu, amepongeza juhudzi za Tume, lakini pia juhudzi za Serikali. Tunaomba kumthibitishia yale yote aliyoysesma tutayazingatia, kama sio kwenye Kanuni lakini tutayazingatia kwa nafasi moja ama nyingine.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mchungaji Mwanjale, amesema sana umuhimu wa huu mfuko, ameipongeza Serikali kufikia hatua hii. Ameomba uimarishaji wa kamati zote mpaka kwenye kamati zile zilizoko huko kwenye Halmashauri zetu na kwingineko, uadilifu wa kufanya kazi. Haya yote ni mambo ya kimsingi kabisa. Tunaomba, sisi kama Serikali tunakubali tutayachukua na tutayafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mnyika amechangia kwa maandishi amesema sekta binafsi nayo iachangie pamoja na jamii kwenye huduma za UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, sekta binafsi inashirikishwa kwenye uchangiaji na nia ya Serikali kwa kweli ni kuendelea kufanya hivyo. Kwa mfano, Geita Gold Mine ambayo kila mwaka wanatangaza na kupanda Mlima Kilimanjaro, wamekuwa wakichangia sana.

Sasa huu ni mfano mmoja mzuri. *Inshallah* Mwenyezi Mungu akiturudisha Bungeni mwakani, nadhani tuombe tu na sisi Wabunge tukiongozwa na wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, labda na Mheshimiwa Mnyika aliyetoa hoja hii labda na sisi tukapande Mlima Kilimanjaro ili tuweze kuchangia tatizo hili. Kwa hiyo, hizo tu ni hamasa ambazo wenzetu kama Geita Gold Mine wameonesha. Kwa hiyo, Watanzania wengi wanachangia na sisi huwa tunashukuru na tunakubaliananao kwa sababu ni jambo la nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, ametoa *proposal* ya kuongezwa kwa majedwali; tutaona namna majedwali ya Serikali yalivyorekebisha maeneo hayo na kuona tunaweza kufanya nini.

Mheshimiwa Spika, Kamati za UKIMWI ziko katika ngazi zote mpaka kwenye ngazi za Wilaya, na kwenye ngazi za Wilaya Sheria Mama inatoa miongozo ya namna Kamati zile za UKIMWI zitakavyofanya kazi na kujumuisha watu wa aina mbalimbali ili kuweza kujadili na kuona namna tunavyoweza kushughulikia tatizo hili la UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, kwa sababu, ya muda, wachangiaji waliochangia kwa kusema wako wengi kama niliviyowataja pale mwanzo, na kwa kweli, wamechangia michango mizuri. Naomba niwashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, nirudie kusema kwamba, tutajibu michango yote kwa maandishi na sisi kama Serikali, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa sababu wote mmeunga mkono juhudzi hizi za kuanzishwa kwa huu Mfuko na mmekubaliana na Serikali kwamba ni wakati muafaka na mmesema kwamba, Serikali lazima isimamie jambo hili kwa dhamira ya dhati.

Mheshimiwa Spika, naomba kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hoja hii. Na baada ya kusema haya, basi naomba kutoa hoja, ili hatua inayofuata ya kuendelea kuhitimisha Muswada huu iweze kuendelea.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa Hoja.

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba kutumia Kanuni ya 28(5), tuongeze nusu saa tuweze kuhitimisha hii shughuli, jioni tuingie kwenye Muswada mwingine. Katibu!

KAMATI YA BUNGE ZIMA

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Tume
ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania wa Mwaka 2014
(The Tanzania Commission for AIDS [Amendment] Bill, 2014)**

MWENYEKITI: Waheshimiwa naomba tukae. Katibu?

(Hapa, yalitamkwa Marekebisho ya Jumla ya Neno TACAIDS yaliyofanywa na Serikali katika Ukurasa wa 3 wa Muswada kuwa Isomeke COMMISSION)

(Mabadiliko ya Neno yaliyotajwa hapo juu katika
Ukurasa wa 3 wa Muswada, yalikubaliwa na
kupitishwa na Kamati ya Bunge Zima)

Ibara ya 1

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge zima, bila ya mabadiliko yoyote)

Ibara ya 2

Ibara ya 3 iliyokuwa ya 2

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Ibara Mpya ya 3

Ibara Mpya ya 4

Ibara Mpya ya 5

(Ibara ziliyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge zima bila ya mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tundu Lissu, vipi, naona kama unashangaa kitu, nini?

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia kwenye Ukumbi wa Bunge lako Tukufu, sina hakika kama tuna Quorum!

Ibara Mpya ya 6

Ibara Mpya ya 7

Ibara Mpya ya 8

(Ibara ziliyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima, bila ya mabadiliko yoyote)

Ibara Mpya ya 9

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sina tatizo la pendekezo lililoko Mezani, lakini katika mchango wangu niliomba ufanuzi kutoka kwa Waziri, baada ya maamuzi ya kuingiza suala la uundaji wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini katika kuleta Muswada huu hawakuleta vilevile pendekezo la marekebisho kwenye Muundo wa Kamati za Wilaya za UKIMWI ambapo pamoja na kuwa na wawakilishi wa Taasisi zilizo za Kiserikali na watu wanaoishi na virusi vyta UKIMWI ni wajumbe wasiokuwa na kura ndani ya vikao hivyo; na watu wanaoishi na virusi vyta UKIMWI wamekuwa wakitoa rai kwamba, wawekwe kama wajumbe wenyewe kura, ili wawe sehemu ya maamuzi ili waweze kuongeza msukumo.

Ningependa kupata ufanuzi tu kwamba, kwa nini hili halikuletwala na pengine ni lini litatafakariwa kuletwa? Nashukuru.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Mnyika ametuletea jambo hilo. Kwa mujibu wa Sheria Mama, utaratibu wa uendeshaji wa Kamati zile za UKIMWI ambazo ziko kwenye ngazi ile ya chini unaratibiwa kwa mujibu wa sheria ya zamani. Lakini, baada ya marekebisho haya tunayoyafanya, haituzuui pia sasa haimzuii Waziri baada ya sheria hii kupita, kuendelea kutengeneza kanuni sasa ambazo zitaendelea kutoa miongozo ya utendaji wa kazi za kamati ambazo zitafanya kazi kwenye hayo maeneo ambayo Mheshimiwa Mnyika anayasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni pendekezo zuri lakini sasa kwa kuwa tayari Sheria Mama ilikuwa imeishaweka utaratibu wa kutoa miongozo, lakini kanuni sasa zinaweza zikatoa maelekezo ya namna sasa ya watu anaowasema Mheshimiwa Mnyika, wakashiriki kiukamilifu katika kamati hizo.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara Mpya ya 10

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hiki nilikuwa napendekeza kuondoa neno President na badala yake kuweka neno Minister.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba Mwenyekiti wa Kamati hii atachaguliwa na Rais; na wakati huo huo huyu Mkurugenzi Mtendaji (*Executive Director*) naye vilevile atakuwa appointed na Rais. Hapa kunaweza kukaleta mgongano, kwamba, Mwenyekiti anateuliwa na Rais wakati huo huo na Mkurugenzi Mtendaji naye anateuliwa na Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilishauri kwamba hii nafasi ya Mkurugenzi Mtendaji, huyu ateuliwe na Waziri ili kusije kukatokea mgongano kwamba Mkurugenzi anajiona yeye ni mteule wa Rais na Mwenyekiti ni mteule wa Rais, kwa hiyo, wakajikuta kwamba power zao ni sawa kwa sababu wote ni wateule wa Rais. Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza kwamba huyu Mkurugenzi Mtendaji ateuliwe na Waziri na asiteuliwe na Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya hivyo, ukienda kifungu cha pili yake pale, utakuta kwamba iwapo nafasi hii ya Mkurugenzi Mtendaji itakuwa wazi, basi Mwenyekiti katika muda wa siku 30 atam-notify Wazirji; na Waziri atachukua hatua za kumu-appoint Executive Director. Kwa hiyo moja kwa moja inaonekana kwamba Waziri bado ana nafasi ya kumu-appoint huyu Mkurugenzi Mtendaji badala ya huyu Mkurugenzi Mtendaji kuteuliwa vilevile au kuwa appointed na Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu yalikuwa ni hayo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, practice ambayo tuko nayo katika Serikali kwa mujibu wa sheria nydingi ambazo tumeishazitunga, Wenyeviti wote wanateuliwa na Mheshimiwa Rais; na tayari tunazo sheria ambazo zimepitishwa kwa mfano Sheria ya Bodi ya Mfuko wa Elimu Nchini, Sheria ya Bodi ya Manunuzi na nyiningine. Sasa unakuta kwamba practice tuliyonayo Wenyeviti hawa wanateuliwa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgongano huo wa kimadaraka anaousema Mheshimiwa Mbunge, ni kwamba, Rais ye ye anateua kwa mujibu wa madaraka yake, Waziri kwa mfano, Waziri mwenye dhamana ya udhibiti wa UKIMWI nchini ni Ofisi ya Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu ndiyo yenyehi dhamana ya udhibiti wa UKIMWI haina maana na yenye wewe ikifanya uteuzi, kwa hiyo, aliyyeteuliwa na Rais atakuwa na mgongano wa kiteuzi na huyu aliyyeteuliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa maana ya Instrument ya Waziri Mkuu katika kusimamia tatizo hili la UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri tutakuwa tume-harmonize tu utaratibu mzuri wa kazi, kwa sababu hawa wote kwanza wakiteuliwa na mtu mmoja wanaweza waka-gang-up wakajiona hawa wote ni wateuliwa wa mtu mmoja na basi wakaamua kuona kama vile ni watu ambao ni very exceptional katika taasisi ile ambayo wanaiongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani kama ilivyo hivi ni vizuri tungeiacha hivyo hivyo kwa sababu practice inaonesha migongano hiyo haipo na utendaji huu wa kazi kwa utaratibu huu nadhani utatusaidia tu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa, labda ungesoma vizuri, anachouiza Mheshimiwa Rajab ile 11(1) ambayo sasa ni 10 mpya, inasema; “*there shall be an Executive Director of TACAIDS who shall be appointed by the President on such terms and conditions as shall be specified in the appointment letter*”.

Sasa lakini, ukisoma kile cha pili yake inasema kama hiyo nafasi ya “Executive Director falls vacant then the Chairman shall within 30 days notify the Minister who shall take appropriate measures towards appointment of an Executive Director”. Ni kwamba, huyu Mwenyekiti naye anakuwa appointed na President na Executive Director kwa mara ya kwanza anakuwa appointed by President, isipokuwa ya pili ndiyo Minister. Ndiyo hiyo confusion na tunauliza maana yake nini?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwanza naunga mkono mapendekezo ambayo Mheshimiwa Rajab amewasilisha. Kwenye kifungu cha 12(2) kimsingi haina confusion sana kwa sababu kimewekwa kwa ajili ya kuwezesha mchakato tu wa Waziri kwenda kutoa taarifa za uteuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kifungu ambacho kinahitaji marekebisho ni 11(1) ambapo inasema; "...there shall be an Executive Director of TACAIDS who shall be appointed by the President."

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Rajab kwamba Mwenyekiti ameteuliwa na Rais, basi ni vyema Mkurugenzi Mtendaji akateuliwa na Mamlaka nyingine. Sasa, Mheshimiwa Waziri katika majibu amerudia rudia neno moja kwamba *practice*, hii ni *practice*, hii ni *practice*. Ni kweli kumekuwepo na *practice* ya namna hiyo, lakini ni ukweli vilevile tumekuwa tukiwambia kwamba hiyo *practice* ni *bad practice*.

Sasa ifike hatua, ni kweli ukitizama mlolongo wa sheria zetu za miaka ya nyuma, zimeweka mfumo wa namna hiyo ambapo Rais anateua Mwenyekiti, wakati huo huo anateua iwe ni Mkurugenzi Mtendaji au Mkurugenzi na kadhalika. Sasa ili tufungue ukurasa mpya, tuanze na sheria hii, tunafanya marekebisho ya sheria ya zamani, sheria mpya iweke separate mamlaka za uteuzi kwenye ngazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kukubaliana na pendekezo la Mheshimiwa Rajabu, mimi ningesema twende mbele zaidi. Tunapoondoa neno President na kuweka neno Minister, tuongeze na maneno "...upon receiving recommendations from the Commission".

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo kubwa sana katika Taifa letu; unaunda chombo, tume au bodi, unaipa Mwenyekiti, halafu hicho chombo, mtendaji anayesimamia utendaji wa hicho chombo kama Katibu wa chombo, utendaji wa kila siku, hicho chombo hakihusiki katika kumteua hata kutoa mapendekezo wakati mwagine kwenye maamuzi ya uteuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imefika wakati tuache hiyo *bad practice* na badala yake tuwe na *best practice*, tutumie misingi ya utawala bora, corporate governance, public governance katika taasisi za namna hii, zinataka uteuzi wa namna hii ili kuongeza uwajibikaji na kupunguza madaraka makubwa sana ya Rais ambayo wengine wanayatumia vibaya kumpendekezea watu ambaa mwisho wa siku unakosekana uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono pendekezo la Mheshimiwa Rajabu.

MWENYEKITI: Naomba na muangalie hizi tofauti kati ya moja na mbili ndogo.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na hilo ambalo umeligusia sasa hivi la tofauti. Ukiangalia katika kifungu cha 11(1) ambacho sasa ndio kifungu cha 10 kimeeleza bayana kwamba Mkurugenzi Mtendaji atateuliwa na Mheshimiwa Rais. Katika kifungu cha 11(2) kimeeleza kwamba itakapotokea nafasi ya Mkurugenzi Mtendaji iko wazi, ndani ya siku 30 Mwenyekiti atapaswa kumuarifu Mheshimiwa Waziri ambaye atachukua hatua stahiki. Sasa katika hatua hizi stahiki ni michakato mbalimbali ya kiserikali ya kupokea mapendekezo ya watu ambaa wanaweza kufaa kushika nyazifa ya Mkurugenzi Mtendaji.

Mheshimiwa mwenyekiti, lakini nikijibu hoja ya Mheshimiwa Mnyika kwamba ifikie wakati sasa tuondokane na taratibu za nafasi mbalimbali za utumishi kuteuliwa na Mheshimiwa Rais. Kifungu cha 5 cha Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2002 kimebainisha bayana na kimetoa mamlaka kwa Mheshimiwa Rais kuteua watumishi wakuu au wakuu wa taasisi mbalimbali Serikalini na idara nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nahisi hoja yangu ina mashiko kwa sababu tayari kuna mifano mingi ambayo imeshawahi kutokea ya mgongano huu wa kimadaraka ndani ya ofisi moja watu ambao wamechaguliwa au wameteuliwa na mtu mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niiombe sana Serikali, ili kuondoa mgongano huu wa kimadaraka na kwa sababu kifungu cha (2) tayari kimempa nafasi Waziri ku-appoint japokuwa Naibu Waziri hapa amesema kuchukua hatua stahiki, lakini akumbuke kuna neno lingine limekwenda hapo mbele appointment, kumu-appoint mtu. Sawa toa appointment, ni hayo hayo kumu-appoint mtu kwa ajili ya kuchukua hii nafasi. Kwa hiyo, bado Waziri atakuwa na nafasi ambayo anaweza kuifanya badala ya kufanywa na Rais kama ambavyo imependekezwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado niko katika msimamo huo huo pamoja na maelezo ambayo Mheshimiwa Mnyika vilevile aliyapendekeza.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mapendekezo ambayo Mheshimiwa Rajab amekuwa akiyatoa, lakini na jambo lingine ambalo hakulizingatia. Huyo Waziri ambaye anasema kwamba ndiye awe na mamlaka ya kuteua ni mteule wa Rais vilevile. Sasa madaraka haya unayahamisha wapi?

Mimi nadhani kwamba tuzungumzie vile ambavyo sheria imetamka. Tusije tukajifunga katika vitu ambavyo tunasema tunaokoa, lakini ule mpira unaelekea kule kule upande wa ushambuliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hapa imejainishia; na uteuzi wa Rais mara nyangi watu wanaaamini kwamba Rais ye ye ndiye anayeteua. Rais siyo mtu binafsi, Rais ni taasisi ambayo inazingatia mapendekezo yaliyotolewa na vyombo mbalimbali ambavyo vinahusika na uteuzi wa hawa. Taasisi zote za Serikali utaratibu ni huo, Mwenyekiti wa Bodi na Mtendaji Mkuu wanateuliwa na Rais, Rais ni uteuzi tu.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nichangie hili hapa. Pengine ni kwa sababu tu hatuangalii sana Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni sharti la kikatiba. Ibara ya 36(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema hivi; "Rais atakuwa na madaraka ya kuteua watu wa kushika nafasi za madaraka ya viongozi wanaowajibika kuweka sera za idara na taasisi za Serikali na watendaji wakuu wanaowajibika kusimamia utendaji wa sera za idara na taasisi hizo katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano nafasi ambazo zimetajwa katika Katiba hii au katika sheria mbalimbali zilizotungwa na Bunge kwamba zitajazwa kwa uteuzi unaofanywa na Rais.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lediane!

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo,...

MWENYEKITI: Bado hujamaliza! Endeleda!

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huyu anayedaiwa hapa Mtendaji Mkuu, hawa ndiyo watu wanaoenda kusimamia hizi sera ndani ya hizi taasisi. Kwa hiyo, naomba kushauri hili suala nadhani kwa sababu hatukuwa tumesoma vizuri hii Katiba, tukishalimaliza hili, maana naona kama linajitokeza mara kwa mara, jana lilijitokeza hapa,

mwongozo huu wa Katiba wote tunawajibika kuufuata. Naomba ibara hii kwa jinsi ilivyo kama ilivoletwa na Serikali ibaki hivyo hivyo.

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwarudishe nyuma Wabunge wenzangu kwamba tunachofanya hapo tunabaadilisha jina la cheo. Hicho cheo kilikuwepo, alikuwa anaitwa Mwenyekiti Mtendaji, ilikuwepo kwenye sheria. Sasa hivi tunachofanya, tunaondoa ule Uenyekiti, anakuwa Mkurugenzi Mtendaji na alipokuwa toka mwanzo alikuwa anateuliwa na Rais kama alivyosema Mwanasheria Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naomba niwashawishi Wabunge wenzangu kwamba, uteuzi ule ubaki vilevile chini ya Mheshimiwa Rais. Lakini naomba pia msione hii Tume kama ni ndogo. Waheshimiwa Wabunge, ndugu zangu, wote tukubali kwamba tumefika hapa kuona maambukizi ya virusi vya UKIMWI yanapungua kwa sababu ya kazi kubwa iliyofanya chini ya hii Tume. Kwa hiyo, tusiishushe tukafikiri kwamba ni Tume ya kawaida, kazi iliyo fanya ni ya vita, hii ni vita ya ugonjwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaombe kwamba tukubaliane na hivyo ilivyo.

TAARIFA

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

MWENYEKITI: Taarifa! Mbona tunajadiliana, taarifa ya nini tena?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo ambalo limepotoshwa, juu ya tafsiri ya Katiba. Ibara ya 36(2) imepotoshwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Inasema yafuatayo:-

"Rais atakuwa na madaraka ya kuteua watu wa kushika nafasi za madaraka ya viongozi wanaowajibika kuweka sera za idara na taasisi za Serikali na watendaji wakuu wanaowajibika kusimamia utekelezaji wa sera za idara na taasisi hizo katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Nafasi ambazo zimetajwa katika Katiba hii au katika sheria mbalimbali zilizotungwa na Bunge kwamba zitajazwa kwa uteuzi unaofanya na Rais." Tafsiri yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho ni lazima kwa Rais kuteua ni nafasi ambazo zimetajwa kwenye Katiba. Nafasi nydingine zozote, Rais anateua kama tu sheria imesema Rais ndiye atue. Maana yake ni nini, ukiitunga sheria ukamuondoa Rais kwenye uteuzi kwa nafasi ambayo Katiba haijasema anateua, mtu mwingine yeyote iwe ni Waziri, iwe ni yeyote atakayetajwa na sheria anateua, ndiyo maana katika hili Mheshimiwa Rajab anapendekeza kwa yule Mtendaji ambaye hajatajwa humu katika Katiba tuirekebishe sheria sasa ateuilie na Waziri ili wasiteuliwe na mamlaka moja kati ya Mwenyekiti na Mkurugenzi mwenyewe wa Tume. Tuanze sasa good practice tuanzie na sheria hii siyo tu turudie rudie bad practice kila wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

MWENYEKITI: Sasa jamani tusidanganyane hapa, wote tunasoma na kuelewa! Mwanasheria Mkuu, jiteteetee!

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, na afadhali umelisema hili. Moja, mapendekezo ya Serikali hapa ni kuendelea kuwa na utaratibu huu, sheria hii hii kwa sehemu ya mwisho iendelee kutaja hivyo kwamba Rais aendelee kuteua, lakini pia kuna sehemu hao wakuu wanaowajibika kusimamia utekelezaji wa sera zilizowekwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani hili Bunge limelifahamu. Mimi naomba kushauri hivi, wakati wa kutunga sheria tujielekeze kwenye kutunga sheria, kwa sababu maneno haya tunayoyasema hayaingii kwenye vifungu vya sheria. Haya tunaweza kuyasema wakati wa mjadala wa kwanza, lakini tunapoingia hapa sasa tunakaa kama Kamati ya Bunge Zima kutunga sheria kifungu kwa kifungu, tujielekeza kuboresha vifungu, siyo siasa, kwa sababu siasa hizi haziingii kwenye kifungu cha sheria.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rajab, pale na mwenyewe amedanganya!

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema, kwanza nimuambie Mwanasheria kwamba hapa hatuzungumzi siasa, tunafanya kazi ambayo tumetumwa na wananchi.

MWENYEKITI: Bwana wewe jibu tuachane na haya maneno.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na wewe. Tayari kuna mifano mingi ambayo iko ndani ya nchi yetu baina ya Mawaziri na Manaibu wao, kwa sababu wote ni wateule wa Rais, wanagongana na wanasababisha baadhi ya Wizara kutokufanya vizuri, hiyo mifani ipo mingi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama Bunge nalo lina nafasi ya kutunga sheria na sheria hii ikakubalika ni lazima au kwa vyovvoste vile Rais naye ataifuata matakwa ya Bunge. Rais ni Sehemu ya Bunge, hata kama Katiba imesema hivyo, lakini Rais ni sehemu ya Bunge. Kwa hiyo, kitachokutungwa na Bunge, sheria itakayopitishwa na Bunge ndiyo hiyo ambayo Rais naye ataifuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo bado mimi niko katika msimamo wangu wa kwamba nafasi hii ya kumteua *Executive Director* iende kwa Waziri wa Wizara husika badala ya kwenda kwa Rais, Rais abaki tu na nafasi ile ya kumteua Mwenyekiti wa hii Tume. Ahsante.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja ilihamuliwa na kukataliwa)

Ibara Mpya ya 11

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara Mpya ya 12 iliyokuwa Ibara ya 13

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hiki cha 13 cha zamani ambacho sasa ni 12 katika, ibara ile ya (b)(iii) inasema kwamba; “Each Minister, department and agency and every private institution shall establish an HIV and Aids Committee under this Act and shall design one senior officer to be an HIV...”

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka baada ya neno senior officer huyu ambaye atateuliwa au atachaguliwa na Wizara ama idara, ama taasisi binafsi, pale tuongeze maneno yanayosema kwamba who has knowledge and experience on HIV and Aids.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nafasi hii ambayo inatolewa katika kila Wizara ama idara ama taasisi za mtu binafsi kwa mujibu wa sheria hii tunayotaka kuipitisha, ni kwamba, ni vyema mtu huyu ambaye atateuliwa kushughulikia masuala haya ya UKIMWI, *at least* awe na uelewa wa mambo haya ya UKIMWI, awe na imani vilevile katika masuala mazima ya kuhudumia hawa watu ambao wameathirika na matatizo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo *target* yangu.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri huu wa Mheshimiwa Rajab, Mbunge, ni mzuri, huu hauna matatizo. Nashauri Bunge likubaliane na ushauri wa Mheshimiwa kwa sababu unaongeza tu *experience* kwa watu wanaoenda kusimamia hii.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mwanasheria, lakini tunaomba ushauri huu uzingatiwe wakati wa kutengeneza kanuni zitakazokwenda kusimamia Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ni hii unaposema kwamba huyu mtu lazima awe na knowledge na experience on HIV and AIDS, unaweza ukakuta kuna taasisi haina mtu mwenye experience wala knowledge inayohusiana na masuala haya ya HIV.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa kwenye kanuni ni lazima tuweke utaratibu, taasisi zile zote tuweze ku-train watu katika kila taasisi ambao watapata hiyo knowledge na watapata hiyo experience na hao sasa ndiyo watakuwa wasimamizi na waratibu wa shughuli hizo kwenye zile taasisi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ukisema tu sasa hapa tuiweke tu toka mwanzo iwe mtu apatikane mwenye hiyo knowledge kwenye ile taasisi, tunaweza tukajikuta kwamba kwenye private sector labda hakuna mtu ambaye ana experience na knowledge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama alivyosema AG, ni wazo nzuri sana na sisi tunalikubali. Lakini nilikuwa nafikiri tukaliweke kwenye kanuni kusudi watu hawa wawe *trained* kwanza halafu ndipo waweze kuteuliwa. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, nadhani argument ya ku-train na hapa havina nguvu sana. Kwa hiyo, nahoji kufuatana na amendment iliyoletwa na Mheshimiwa Rajab.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara Mpya ya 13 ambayo ilikuwa Ibara ya 14

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi naomba niishukuru Serikali kwa marekebisho kwa sababu marekebisho ambayo nilikuwa nimeyaweka mengi yamekubaliwa na hasa kwenye Wajumbe wale wa Tume, nilikuwa nimependekeza kwamba mmoja atoke Wizara ya Afya, hilo wamelikubali, mmoja atoke Wizara ya Fedha, wamelikubali na tulipendekeza kwamba wawili watoke sekta binafsi na lenyewe limekubalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ila ambalo halijakubalika ni kwamba niliomba tumuondoe Mjumbe kutoka kwenye Tume ya Kudhibiti UKIMWI badala yake tuitoe kwa watu wengine. Sasa hoja yangu ni kwamba huu mfuko utakuwa chini ya uangalizi wa Tume hawa ni Board of Trustees, huu mfuko uko ndani ya Tume na mfuko huu pia Katibu wake atakuwa ni Mkurugenzi

Mtendaji wa Tume. Sasa, hapo hapo hao hao wamerudi tena kuja kuwa Wajumbe wa Bodi (Trustees).

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikaona kwamba labda wenyewe wangebaki na nafasi ya usimamizi badala ya kurudi tena wakaingia kwenye Board of Trustees. Sasa, nilikuwa naomba Serikali ikubaliane na mapendekezo yangu. Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nimependekeza kwamba hiyo nafasi, nilisema two members from private sector, one member from Foreign Development Partners, one member from Ministry of Finance, one representative from Local Development Partners, one member from Ministry of Health, one member from Non-Governmental Organizations.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweka wale wachangiaji wakubwa wa ndani badala ya kuacha tukasema private sector, tulipenda wale wachangiaji wakubwa wa ndani pia waende kwenye mfuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu nyiningine ni kwamba hapa tunatafuta fedha, tunaleta Wajumbe kwenye Bodi ili kuja kusaidia kupata vyanzo vya mapato ili tuweze kupata fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sisi wenyewe wale wale ndiyo tatarudi tena kukaa humo ndani, badala ya kuleta mawazo mapya yanayotoka nje ili tupate kupata fedha kutosheleza; na tumezungumza kwamba huu mfuko lazima uwe mfuko endelevu. Kama ni mfuko endelevu lazima tulete mawazo mengine kutoka nje ili tujue kwamba tuna vyanzo vya mapato vya kutosha ambavyo labda yule mwingine ambaye yuko kwenye Tume anaweza asivifahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo ilikuwa ni hoja yangu; na hoja nyiningine ilikuwa pia wakati wa kuangalia wakati wa kugawa hizi fedha, maana yake tumesema sisi kama Kamati tumesema kwamba...

MWENYEKITI: Ngoja kwanza, tunatunga sheria, tunaenda moja kwa moja.

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatunga, sasa basi hoja yangu ndiyo hiyo.

MWENYEKITI: Maliza kwanza hiyo ya kwanza.

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O: Basi, hoja yangu ndiyo hiyo ya wajumbe kwamba tumuondoe mjumbe kutoka kwenye Tume, tuweke mjumbe mwingine wa kutoka nje, wachangiaji wakubwa wa ndani.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa concern ya Mheshimwia Mng'ong'o na kwa kweli amefanya kazi kubwa juu ya kuwepo kwa sheria hii na ameendelea kufanya kazi kubwa sana juu ya kupigania maslahi ya afya za watu ambao ni waathirika wa ugonjwa huu wa UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ila nilikuwa naomba kushauri kwamba katika uendeshaji wa Serikali hatuwezi kuruhusu watu wa nje wakaingia kwenye Bodi za Serikali. Tukifanya hivyo tutakuwa kwanza, tuna-compromise our sovereignty, lakini pia tutawakaribisha watuingilie sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hawa wamekuwa wakitoa hizi fedha bila kuwa hata Wajumbe wa Bodi, kama nia yao ni kuendelea kutoa hizi fedha, wataendelea kuzitoa bila ya kuwa lazima washinikizwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tulikuwa na mapendekezo kwamba badala ya hawa, tuwaweke sasa wajumbe kutoka kwenye... tumeleta mapendekezo kwenye hili jedwali, tuweke Mjumbe kutoka kwenye organization ya watu wanaoishi na HIV/AIDS kusudi sasa na wao hawa ndiyo wahusika wakubwa kama ni uzoefu, hawa ndiyo watakuja kutusaidia. Lakini hawa wanaotaka kuingia mle ama kutoka Local Development Partners, kwanza, hawapo mara nyingi ni hao Foreign Development Partners, hao tunashauri kwamba kama tulivyoweka kwenye mapendekezo ya Serikali kwenye marekebisho, wasiwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono pendekezo la Serikali na kwenye mchango wangu wa maandishi nilipendekeza vilevile umuhimu wa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI kuingizwa katika huu mfuko kwa sababu nyingi ambazo nisichukue muda kuzieleza. Lakini ningependa vilevile katika majumuisho, Serikali ieleze tu; kumekuwepo na mapendekezo kwamba huu mfuko katika moja ya vyanzo vyake ni kufikiria kuhusu vyanzo vya kutoka kwenye Halmahsauri.

MWENYEKITI: Hii hapa hatujaingia kwenye vyanzo, ilikuwa ni membership.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Ndiyo, nataka kusema kitu hapo kwenye hii hii muundo, najenga hoja tu kwamba, itoke kwenye Halmashauri. Na tufikirie vilevile kuwa na mifuko kwa ajili ya miradi ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI haya masuala ya kupambana na UKIMWI mpaka kwenye Halmashauri.

Sasa kama tunafikiri hivyo ni muhimu sana, katika muundo wa hii *fund representative from Ministry responsible for Local Government* kama nyongeza, itatusaidia sana. Moja, kwa sababu watakuwa vyanzo vya mapato na nini, pili, mifumo mifumo mazima ya migawanyo ya fedha wana nafasi yao, tatu, tumekubaliana kwamba kimsingi mambo mengi tunataka kupeleka madaraka, kugatua madaraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kiungo kati ya masuala mazima ya Halmashauri ni huyo mwakilishi wa *Ministry responsible for Local government* (Mwakilishi wa Wizara inayohusika na Serikali za Mitaa) kweye chombo hiki. Nadhani Serikali katika majumuisho wafikirie hili ombi na kulizigatia vilevile, pamoja na kuunga mkono pendekezo la Serikali.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ni kweli, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mnyika, kwenye mchango wake wa maandishi alionilettea hapa, alipendekeza sana kufanya marekebisho kwenye lile jedwali na kuhakikisha kwamba mmoja wa wawakilishi ni lazima atokane na watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Namshukuru Mheshimiwa AG amelielea vizuri hilo, tunalikubali. Lakini naona logic hiyo ya kuongeza mjumbe kutoka kwenye Wizara ya Local nadhani ni jambo hilo pia ni la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa jambo hili ni kwamba kazi hizi za Tume hazitakuwa zinaelea hewani tu ni lazima zishuke na kule chini ndiko ambako waliko wadau wakubwa kwa maana ya Watanzania wenywewe. Kwa hiyo, kuongeza mtu wa Local Government nadhani ni ushauri muhimu sana, sisi kama Serikali nadhani hauna tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba niendelee kufikiri kwamba Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Lediane Mng'ong'o nadhani tukubaliane tu umuhimu wa mjumbe mmoja wa Tume kubaki kwenye ile bodi. Kwa sababu Mkurugenzi ata-serve kama Sekretari, na aki-

serve kama Sekretari hana nafasi ya kupiga kura wala kuchangia. Lakini tutatakiwa pia maagizo mengine yatakayojadiliwa ile bodi yarudishwe kufanyiwa kazi kule. Kwa hiyo, kuna haja ya kuwa na mwakilishi ambaye atakwenda kutoa ufanuzi na kutoa taarifa na kuleta pia taarifa katika Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukiweka composition ya watu hawa na ukialingalia pale tumeongeza private sector kwa maana ya uwakilishi wa private sector, composition hiyo nadhani itakuwa vizuri.

Mheshimiwa Mng'ong'o aliisitiza sana private sector lazima wawepo kwenye Bodi hiyo. Naomba kukubaliana kwamba wale ni watu pia wa msingi. Kwa hiyo, composition ikiwa hivyo nadhani itatusaidia.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lediana tufike mwisho.

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekubaliana kabisa hasa hilo la kuingiza watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI, nakubali asilimia mia moja na naipongeza Serikali, kwa sababu hata kwenye Kamati tulijadili. Lakini hilo la Commission pia nimekubali awe ni mmoja wa ma-commissioners, nimekubali.

MWENYEKITI: Kwa hiyo, tunaongeza mwathirika mwenyewe na Local Government.

(Ilara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

MWENYEKITI: Kuna 12(c), Mheshimiwa Lediana!

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekubaliana na imeishaleta marekebisho naipongeza kwa sababu tulisema hizi fedha zisitumike kwa kitu chochote na Serikali imekubaliana na mapendekezo yangu, nashukuru.

(Ilara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbarouk, unakubaliana na ya Mheshimiwa Lediana na Serikali?

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu kile cha 12A kwanza nilileta marekebisho (3)(a)(b) kwa kuongeza maneno; "...in and Internationally."

Naomba nkinukuu hapa; kinasema kwamba promote prevention of new infection according to the agreed priorities in HIV and AIDS nationally response. Baada ya neno nationally tuongeze maneno mengine ambayo yatakuwa ni; "in and Internationally response."

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni yangu ni kwamba, suala hili la HIV ni suala la kimataifa na hata fedha ambazo tunazitegemea nydingi kwa ajili ya kunusuru hawa watu wetu basi zinatokana na mifuko hii ya kimataifa. Sasa, nilitaka tu niongeze hili neno "Internationally" ili iwe moja kati ya mambo ambayo yanahitajika kuzingatiwa.

MWENYEKITI: Kuna tatizo nalo hilo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui tunaitafsirije hiyo, kwa sababu tunapoandaa kazi zitakazofanywa na hii Tume,

sisi tunataka kufanya mapambano dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI kwa kufuata sera na mikakati iliyomo ndani ya nchi yetu ya Tanzania.

Sasa tunaposema mikakati inayofanyika ndani ya nchi of course ni mikakati ile ambayo tuna-adopt makubaliana ya kimataifa na nini, lakini sisi tunapokuja humu ndani tunatengeneza mkakati wetu wa kinchi, wa ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sijui ni kwa nini Mheshimiwa anafikiri mpaka tukiongeza hiyo *International* ndiyo ataona kama vile tume-comply na hayo mengine ya kimataifa. Lakini tunapotafsiri sisi mkakati wa nchi, unabakia kuwa ni mkakati wa kwetu wa kitaifa, ambapo sasa mkakati huo unakuwa na component zote, kama kuna makubaliano ya kimataifa sijui haki nini, hayo yote sasa tunakuja kuyatafsiri katika mkakati wa kitaifa wa hali ya UKIMWI ndani ya nchi yetu. Kwa hiyo, nilikuwa namuomba tu Mheshimiwa Rajab, katika hili tukubaliane kwamba ya Serikali ipo vizuri.

MWENYEKITI: Dunia kote kuna ya kwao.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo ambayo Mheshimiwa Waziri ameyatoa, basi niseme nakubaliana nayo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante endelea na inayofuata.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Katika Ibara ya 12B(3) ambayo nilitaka iondolewe neno Minister na badala yake libaki neno Members.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ni kwamba inasema *the Minister shall appoint one of the members to be a Chairman*. Sasa mimi nilikuwa nafikiri kwamba hii nafasi ya kuteua Mwenyekiti huyu wa hii Bodi, basi waachiwe wale Members wenye kazi ya Bodi wateue yule mtu wao. Kwa hiyo, nipayendekeze tu kwamba hii ni vyema sasa ba isomeke “*the members shall appoint their own member to be the a Chairman*.”

MWENYEKITI: Muandike vizuri hata na ninyi pia. Haya itakuwa kama Kamati za Bunge hivi. Fujo hapana, hapana, haya. Mheshimiwa Waziri! (*Kicheko*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa dhamira ya Mheshimiwa Rajab anadhani kwamba labda ukifanya hivyo, ukiwatumia wajumbe wenye kazi ya Bodi wanaweza wakam-own Mwenyekiti. Kuongoza kitu kama hiki ni tofauti na Kamati nyingine zile ambazo zinatoa loophole wajumbe wachaguane wao wenye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo mwanzo mapambano dhidi ya UKIMWI yako chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Waziri Mkuu ndiye anayeongoza mapambano hayo kwa mujibu wa *Instrument* ambayo amepewa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hati idhini ile inampa hayo madaraka pia ya kujiridhisha hata huyo Mwenyekiti anayeteuliwa ni wa namna gani na atafanya kazi hizo kweli kwa uadilifu na kwa kutekeleza majukumu kama vile ambavyo tunafikiri atafanya. Kwa kweli hii haiwezekani kwa kweli Mwenyekiti huyo yaani wakutane wale halafu waanze, kampeni zifanywe kwa wajumbe. Sheria inawaruhusu kwa Makamu, lakini kwa Mwenyekiti kwa kweli abaki ateuliwe.

MWENYEKITI: Haya Mheshimiwa Rajab, itakuwa kama vile ninyi mnavyofanya mambo.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa umetia na mdomo wako, basi nikubaliane nayo tu.

MWENYEKITI: Ahsante. Naomba uendelee ile inayofuata tafadhalii.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilileta jedwali la marekebisho katika kifungu *Part IV* Clause 12B kwa kutaka niongeze kifungu kipyaa na zile nyingine ziwe numbered. Kifungu hicho kiwe 12B(5) na kisomeke *The members of the Board of Trustee will hold office for a period of five years and shall be eligible for reappointment.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, hii Bodi haikuwekewa muda wake, hakuna muda wa mwisho wa Bodi hii. Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza kwamba Bodi hii iwekewe muda na muda wake uwe ni miaka mitano kama vile ambavyo huyu Mkurugenzi Mtendaji muda wake amewekewa wa miaka mitano.

Kwa hiyo, Mkurugenzi Mtendaji atakapomaliza muda wake wa miaka mtano, basi na ile bodi nayo iwe imemaliza muda wake. Kwa hiyo, iainishwe katika sheria kwamba hii Bodi muda wake itakuwa uhai wake ni wa miaka mitano. Ni hilo tu.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, anachosema Mheshimiwa Mbarouk ni kweli, tunakubaliana naye kwa sehemu kwamba katika kuandaa Muswada huu ilisahaulika kuweka ule muda wa Bodi. Lakini, na Serikali imeleta pia mabadiliko kwenye hii.

Sisi tunapendekeza kwenye mabadiliko yetu kwamba hawa Wajumbe wa Bodi ikiwa ni pamoja na Mwenyekiti washike madaraka kwa muda wa miaka mitatu, lakini wakiwa pia na fursa nyingine ya kuchaguliwa kwa mwaka mmoja halafu tunavipanga tena vile vifungu vingine upya accordingly, yaani kipindi kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani nilimaanisha kipindi siyo mwaka. Halafu baada ya hapo vifungu vile sasa vinapangwa tena maana tulicho-introduce kilikuwa cha 7, halafu baadaye kilichokuwa cha 7 sasa kinakuwa cha 8 na kuendelea.

MWENYEKITI: Kwa maana kwamba mnakubaliana na Mheshimiwa Rajab, isipokuwa muda tu?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Eee ndiyo!

MHE. RAJAB MBOROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na hiyo miaka mitatu, kwa sababu mimi nilipendekeza miaka mitano, lakini kwa ajili ya kuleta ufanisi, lakini miaka mitatu naamini kwamba itakuwa ni nzuri zaidi.

MWENYEKITI: Malizia kile cha mwisho!

MHE. RAJAB MBOROUK MIHAMMED: Amendment katika part 4 clause 12(E) kwa kuondoa maneno “more” na ili niweke neno “three”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba katika huu Muswada au pendekezo hili la Muswada ambalo limetolewa ni kwamba Bodi hii itakuwa na uwezo wa kufungua akaunti au kuwa na akaunti zaidi ya moja katika mabenki yetu kwa sababu ya fedha zile ambazo zitakuwa zinapokelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na wingi wa fedha na matatizo ambayo tulishaya-practice hasa katika Halmashauri zetu wakati unapokuwa na akaunti nyingi, tukafikia wakati tukaona kwamba akaunti hizi kuwa nyingi basi zinaleta tatizo. Ni bora kuwa na akaunti kidogo ambazo tutaweza kuzi-monitor vizuri, tukatoka karibu kwenye akaunti 12/13 tukaja katika akaunti sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa mujibu wa Muswada huu ni kwamba, umetoa room kwa hii Bodi kuweza kufungua akaunti wanazotaka, kama 10, 15, 20, 100, wanawenza kufungua tu. Nafikiri tufike pahala tuwawekee kikomo cha ufunguaji wa hizi akaunti. Kwa hiyo, mimi nimependekeza kwamba wafungue akaunti zisizozidi tatu hapo ili tuweze ku-monitor vizuri hizi fedha ambazo zinainginzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA – MHE. ADAM KIGOMA MALIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo la Mheshimiwa Rajab ni zuri. Lakini nataka nimwambie Mheshimiwa Rajab kwamba, tatizo hapa tumesema ni *one or more*, tunatarajia kwamba hii *Board of Trustees* itatumia busara yake, kwa sababu hapa hizi pesa zinatumiwa kwa malengo, expenditure purposes mbalimbali.

Kwa hiyo, kuna pesa zingine labda ziliwuwa zinatoka nje za *foreign assistant* lakini zinakwenda kwenye prevention, kuna nyingine zinakwenda kwenye coordination and monitoring support. Sasa wale wanasema bwana mimi natoa pesa, lakini nataka iende kwenye coordination and monitoring, kwa hiyo mnaitengenezea akaunti yake, zingine wanasema bwana zinaenda kwa ajili ya kuchangia lishe au nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunacho assume, assumption kubwa hapa ni kwamba ndiyo maana tunateua *Board of Trustees* kwa uangalifu sana ili waweze pia kubeba dhamana hii ya kusimamia pesa hizi. Tunasema hatuamini kwamba watatengeneza akaunti 100, hiyo itakuwa ni fujo, lakini tunaamini tunasema one or more, tukijua kwamba kima cha chini cha akaunti ni *at least* ile moja, lakini watasema hii akaunti ya operations, hii akaunti ya hivi na watazipatia maelezo wakati wanazitengeneza.

MWENYEKITI: Mnasahau kwamba huyu ni Mwenyekiti wa LAAC, kwa hiyo akakuta zile akaunti nyingi.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini akumbuke kwamba, hawa pia ni binadamu na binadamu ndiyo ambao wanafanya makosa. Wewe ni muumini, kila siku ya Ijumaa tunapewa mawaidha yale yale, yale yale kila Ijumaa, ni kwa sababu ya kukumbushana, kwa sababu sisi ni binadamu ambao tunatenda makosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi ambazo tunazungumza, Mheshimiwa Naibu Waziri alizungumza vizuri sana na masharti yake ameyataja vizuri sana, lazima Serikali izi-ring-fence pesa hizi, hata Mwenyekiti wa Kamati alisisitiza sana hili, kuhakikisha kwamba fedha hizi za mfuko zitakazoingizwa tunazi ring-fence ili zisiwe zinatumika tu hovyo hovyo. Sasa tutakapoanza kuruhusu kutumia ama kuweka katika akaunti nyingi zaidi kwa kweli hapa tutafanya kosa.

Mimi nishauri tena tu kwamba hili neno “more” liondoke, badala yake tuweke idadi kamili kama ambavyo nimependekeza mimi ya kuwa na akaunti.

MWENYEKITI: Mimi nafikiria kwamba kwa sababu fedha zenyewe source yake sio moja, source ni severally, na kwa faida development partners huwa wanataka wawekewe akaunti zao ili waweze ku-audit. Hizi sio hela za Serikali peke yake na halafu chombo chenyewe ni kimoja tu wala sio zaidi kama zile Halmashauri zako. Mheshimiwa Mnyaa! Ala nimesema Mnyaa, siyo bwana! Mheshimiwa Rajabu! (Kicheko)

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakubaliana na wewe na mifano kama hii imeishatokeza. Nitoe mfano kule Mwanza tulikuta mfano kama huu. Halmashauri ya Mwanza ilifungua akaunti pale bila hata ya idhini ya Waziri kwa sababu ya fedha hizi tu zinazotoka nje, wakaamua tu wenyewe kufungua akaunti bila hata idhini ya Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuogopa haya ndiyo hapo tunaposema ni kweli fedha zinatoka kutoka nje, wafadhili tunawajua kawataja hapa maeneo mawili ambayo yatatoa fedha katika mwaka huu. Kwa hiyo, tunajua kwamba fedha hizi....

Mimi ninachokitaka ni kwamba hili neno “more” liondoke, tuweke idadi ili tuhakikishe kwamba hizi fedha hazitakuja kuingizwa katika akaunti za kinyemela.

MWENYEKITI: Jamani na muda wenyewe kwangu hauniruhusu! Mheshimiwa Esther!

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, nimeelewa dhamira yake, lakini hoja ya Mheshimiwa Rajab bado ina mashiko, kwa sababu kati ya hizo akaunti ambazo tunasema tunaziwekea *limit*, wenyewe watajua fedha gani za wafadhili zitaingia huko na wao watakuwa na uwezo wa kuzi-monitor, kuliko tukiacha huu mwanya mpana ambao wengi wanautumia vibaya. Mimi nadhani bado hoja ya Mheshimiwa Rajab ina mashiko ili hizi fedha zisitengenezewa mazingira ya kuchakachuliwa na hawa waathirika wa ugonjwa wa UKIMWI waweze kunufaika nazo kwa madhumuni yale yale ya Serikali ambayo walikuwa nayo. Ahsante. (Makofsi)

MWENYEKITI: Jamani kuna a lot of experience, donor's wako tofauti, they don't want to mix their stories. Mheshimiwa Lediane Mng'ong'o!

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O: Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi naomba niwasaidie Wabunge wenzangu, sio kwamba zitafanya kila kazi. Hata mkisoma report ya Kamati tumeleeza, hayo masuala ya akaunti mimi nilikuwa naomba kwamba yaingizwe kwenye Kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama ulivyosema uzoefu wa wafadhili uko tofauti, kuna wafadhili watakubali kwamba wanatoa fedha, lakini hawatapenda hela zao ziwekwe kwenye kapu, watasema kwamba ndiyo ni Trust Fund, lakini tunataka fedha zetu ziwe na akaunti maalum ambayo na sisi wenyewe tutaikagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa sisi tukiji-*limit* kwamba tumeishasema mbili/tatu tena kwenye sheria, halafu turudi humu ndani tuje turekebishe sheria, tutaandika wataweka kwenye kanuni watasema lakini matakwa mengine yategemeana na wale wanaotuchangia. Kwa hiyo, mimi nakubaliana na hilo unalosema, namwomba Mwenyekiti mwenzangu wa LAAC akubali hilo, ameishasema Mwenyekiti, tuko hapa tutasaidiana fedha hizi zitatumika kama iliyotakiwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa, seriously practice iko hivyo.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutakubaliana kwamba katika Kanuni itaelezwa kiufasaha kabisa kuhusiana na hizi akaunti, sina tatizo nakubaliana nayo.

(Ibara iliyotajwa hapo juu imepitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara Mpya ya 14 ambayo ilikuwa Ibara ya 15

(Ibara iliyotajwa hapo juu imepitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Jedwali

(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

(Bunge lilitrudia)

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania wa
Mwaka 2014**
(The Tanzania Commission for Aids (Amendment) Bill, 2014)

(Kusomwa Mara ya Tatu)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ibara kwa ibara na imekubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika. Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania wa mwaka 2014 (*The Tanzania Commission for Aids (Amendment) Bill, 2014*) kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Muswada wa Sheria wa Serikali ulisomwa
Mara ya Tatu na Kupitishwa)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naona safari ya Muswada imefika, kwa hiyo tuna hakika kwamba Watanzania wamepata moyo zaidi wa kuendelea kupima afya zao kwa sababu ni muhimu kufanya hivyo.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Nawashukuru wote mlifanya kazi na Mheshimiwa Rajab naona umefanya kazi kubwa sana katika Miswada hii. Tuwashukuruni wote, Wizara, Wafanyakazi wa TACAIDS na Wizara kwa kazi nzuri na ninyi Waheshimiwa Wabunge. (Makofi)

Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka Saa Kumi na Moja.

(Saa 7. 50 Mchana Bunge *lilisitishwa hadi Saa 11.00 jioni*)

(Saa 11.00 jioni Bunge *lilirudia*)

Mwenyekiti (Mhe. Lediane M. Mng'ong'o) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Katibu, hatua inayofuata!

HOJA ZA SERIKALI

M A A Z I M I O

**Azimio la Kuridhia Mkataba wa Msingi na Kanuni za Utumishi wa Umma na Utawala Barani Afrika
la Mwaka 2011 (The African Charter on Values and Principles
of Public Service and Administration, 2011)**

MWENYEKITI: Sasa nitamwita Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma), Mheshimiwa Celina Kombani!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA): Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Msingi na Kanuni za Utumishi wa Umma na Utawala Barani Afrika la Mwaka 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio hili lilipo mbele yako, linapendekeza kuridhia Mkataba wa Msingi na Kanuni za Utumishi wa Umma na Utawala Barani Afrika (*The African Charter on Values and Principles of Public Service and Administration*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio hili ni matokeo ya Mkutano wa 16 wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika (AU), uliofanyika Addis Ababa Ethiopia tarehe 31 Januari, 2011 ambapo waliazimia kila Nchi Wanachama kuridhia Mkataba wa Msingi na Kanuni za Utumishi wa Umma na Utawala Barani Afrika ili kuuvezesha Mkataba huu kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi Wanachama zinatambua kuwa, Mkataba wa Msingi na Kanuni za Utumishi wa Umma na Utawala Barani Afrika ni nyenzo muhimu katika kujenga utumishi wa umma na wa kisasa wenye uadilifu na weledi, utakaowezesha Bara la Afrika kukabiliana na changamoto mbalimbali zikiwepo za kiuchumi, kisasa na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa Msingi na Kanuni za Utumishi wa Umma na Utawala Barani Afrika, pamoja na mambo mengine, unalenga katika yafuatayo:-

Moja, kuimarisha Msingi na Kanuni za Utumishi wa Umma zilizomo ndani ya Mkataba.

Mbili, kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa na Utumishi wa Umma ni za ubora na ubunifu kulingana na mahitaji ya Wananchi.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Tatu, kuhamasisha jitihada za Nchi Wanachama kuubadilisha Utumishi wa Umma kuwa wa kisasa na kuimarisha uwezo wa kutoa huduma kwa Wananchi.

Nne, kuhamasisha Wananchi kushiriki katika usimamizi wa Utumishi wa Umma.

Tano, kuimarisha misingi ya uadilifu katika kuendesha shughuli za Utumishi wa Umma na Taasisi zake ili kuwa na uwazi katika kutoa huduma kwa Wananchi.

Sita, kuboresha mazingira ya utendaji kazi katika Utumishi wa Umma na Taasisi zake ili kuhakikisha haki za Watumishi wa Umma zinalindwa.

Saba, kuwianisha Sera, Kanuni na Taratibu zinazotawala Utumishi wa Umma mionganini mwa Nchi Wanachama kwa lengo la kuwa na mtangamano wa Kikanda na Kibara.

Nane, kuongeza usawa kati ya Wanawake na Wanaume na baina ya Taasisi za Umma.

Tisa, kuimarisha ushirikiano baina ya Nchi Wanachama, Jumuia za Kiuchumi za Kikanda na Jamii ya Kimataifa kwa nia ya kuboresha Utumishi wa Umma.

Kumi, kubadilishana uzoefu na utaalam baina ya Nchi Wanachama na kuweka kanzidata (*database*) ya taarifa hiyo mionganini mwa Nchi Wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuridhiwa kwa Mkataba wa Misingi na Kanuni za Utumishi Umma na Utawala Barani Afrika ni fursa ya Tanzania kuwa:-

Moja, kuweka viwango katika kuendesha Utumishi wa Umma na kujipima kwa kuangalia wenzetu wanachokifanya katika kuboresha Utumishi wa Umma.

Mbili, kupata misaada ya kimaendeleo kutoka washirika wa maendeleo ambao watafadhilii Miradi itakayotokana na utekelezaji wa Mkataba huu.

Tatu, kupata tuzo za ubunifu katika Utumishi wa Umma zitakazokuwa zinatolewa kutokana na masuala mengi yaliyopo katika Mkataba na tayari nchi yetu inayatekeleza masuala hayo kupitia Sera, Kanuni na Taratibu mbalimbali za Utumishi wa Umma hapa nchini.

Nne, kujenga uwezo wa Utumishi wa Umma na Taasisi zake, kupambana na changamoto mbalimbali za ukuaji wa mahitaji ya huduma za jamii zikiwemo umaskini, majanga asilia kama vile njaa na ukame, uharibifu wa mazingira, ukuaji wa haki za binadamu na rushwa.

Namba tano, kuimarisha Utumishi wa Umma katika nchi yetu kwa kuongeza ujuzi, maarifa, ubunifu, tija, ufanisi na uwezo wa kiutendaji kazi.

NA KWA KUWA Jamhuri ya Muungano ni Nchi Mwachama wa Nchi za Umoja wa Afrika (AU);

NA KWA KUWA uchambuzi wa kina ulifanyika umebaini kuwa Mkataba wa Misingi na Kanuni za Utumishi wa Umma na Utawala Barani Afrika haukinzani na Sheria, Kanuni na Taratibu zinazotawala Utumishi wa Umma katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

HIVYO BASI, kwa kuzingatia umuhimu wa Mkataba wa Misingi na Kanuni za Utumishi wa Umma na Utawala Barani Afrika na manufaa ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itapata na kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, ninaomba Bunge lako Tukufu liridhie Mkataba wa Misingi na Kanuni za

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Utumishi wa Umma na Utawala Barani Afrika (*The African Charter on Values and Principles of Public Service and Administration*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MWENYEKITI: Ahsante. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati.

KUHUSU UTARATIBU

MWENYEKITI: Kuhusu Utaratibu!

MJUMBE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja kuhusu utaratibu inatakiwa iungwe mkono na Wajumbe wasiopungua kumi na hawajatimia hawa. Kwa hiyo, hoja haikubaliki kwa mujibu wa Kanuni za Bunge. (*Kicheko/Makofi*)

MWENYEKITI: Naomba nihoji tena, naomba tuheshimu Kiti. Mheshimiwa Waziri ameshatoa hoja, sasa ameomba hoja hiyo iungwe mkono. (*Kicheko*)

(*Hapa Mawaziri waliokuwepo Bungeni walismama kuunga mkono hoja*)

MWENYEKITI: Hoja imeungwa mkono, tuendelee Mwenyekiti.

MHE. JASSON S. RWEIKIZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Kuridhia Mkataba wa Misingi na Kanuni za Utumishi wa Umma na Utawala Barani Afrika (*The African Charter on Values and Principles of Public Service and Administration*, 2011).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Fasili ya 5(1)(b), ikisomwa pamoja na Fasili ya Pili ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala ilishughulikia Mkataba unaopendekezwa kuridhiwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 63(3)(e) iliyorejewa katika maelezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi wa Umma), inahusu Madaraka ya Bunge ya Kuridhia Mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa. Kwa mantiki hiyo, Bunge linaombwa kuridhia Mkataba wa Misingi na Kanuni za Utumishi wa Umma na Utawala Barani Afrika.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kikao cha Kamati na Serikali kilichofanyika tarehe 23 Machi, 2015 katika Ofisi za Bunge Mjini Dodoma, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma), alitoa maelezo kuhusu mapendekezo ya Serikali kwamba, Bunge liridhie kujunga na Mkataba wa Misingi na Kanuni za Utumishi wa Umma na Utawala Barani Afrika wa Mwaka 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupokea maelezo ya Mheshimiwa Celina O. Kombani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma), katika Kikao cha Kamati, Wajumbe walijadili kwa kina maudhui ya Mkataba unaohusika pamoja na dhana nzima ya Misingi na Kanuni za Umma na Utawala Barani Afrika. Lengo lilikuwa ni kuona kama kuna tija kwa nchi yetu kuuridhia Mkataba huu pamoja na kujiridhisha kuhusu faida au hasara na mafanikio au madhara ya kutoridhia Mkataba huu.

Ili kufanikisha azma ya Bunge katika uridhiwaji wa Mikataba ya Kimataifa Kamati, ilifanya mambo yafuatayo:-

Moja, kupitia ibara zote za Mkataba tangu ibara ya kwanza inayohusu tafsiri kwa mujibu wa Mkataba hadi ibara ya 34 inayohusu Nchi Wanachama kutoweka masharti yatakayoathiri matakwa ya Mkataba huu wakati wa kuridhia.

Mbili, kuchambua na kutafakari kuhusu maoni na maelezo ya mtoa hoja.

Tatu, kupitia baadhi ya sheria zinazohusiana na maudhui ya Mkataba unaopendekezwa kuridhiwa na hasa Sheria ya Utumishi wa Umma, Namba 8 ya Mwaka 2002.

Nne, kupitia Tovuti ya Umoja wa Afrika na kuona maelezo yanayotolewa kuhusu asili ya Mkataba, nchi zilizosaini mwanzoni, nchi zilizosaini baadaye, nchi zilizoridhia na nchi ambazo hazijaridhia.

Tano, kupembua faida na hasara kwa madhumuni ya kulishauri vyema Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rasimu ya Awali ya Mkataba huu iliridhiwa na Mawaziri wa Utumishi wa Umma wa Nchi Wanachama wa Afrika katika Mkutano wa Tatoo uliofanyika Mjini Windhoek Nchini Namibia mnamo mwezi Februari, 2001.

Baada ya kupitia katika hatua zake zote, Mkataba huu uliwasilishwa na kuridhiwa na Wakuu wa Nchi Wanachama mnamo tarehe 31 Januari, 2011 Nchini Ethiopia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa nchi zifuatazo zimekwishasaini Mkataba huu nazo ni Kenya, Lesotho, Chad, Gabon, Cameroon, Msumbiji, Namibia, Togo, Zambia, Angola, Benin, Burundi, Côte d'Ivoire, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Gambia, Ghana, Guinea Bissau, Guinea Conakry, Mauritius, Nigeria, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Arab Sahrawi, Senegal, Sierra Leone na Tanzania.

Mkataba huu unasisitiza kuhusu kuboresha huduma za umma, kupambana na rushwa, kulinda haki za raia watumiaji wa huduma za umma na kuhamasisha utawala bora na maendeleo endelevu ya Bara la Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 3(2) ya Mkataba pamoja na mambo mengine, inaweka misingi ya kukataza ubaguzi wa aina yoyote pahala pa kazi. Hii itawezesha Nchi

Wanachama kuajiri kwa kuzingatia taaluma na uwezo wa mtu na siyo misingi ya rangi, kabilia, mahali mtu atokako, itikadi ya siasa, jinsia, ulemavu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 6 ya Mkataba inahusu upatikanaji wa taarifa zinazohusiana na huduma zinazotolewa na Taasisi za Umma. Mkataba unazitaka Nchi Wanachama kuweka wazi taarifa kuhusu utaratibu na namna ya upatikanaji wa huduma kwa umma pamoja na kutoa sababu za maamuzi kufikiwa dhidi ya watumiaji wa huduma za umma.

Kwa upande wa Tanzania, kumekuwa na mifumo isiyo rafiki katika upatikanaji wa taarifa zinazohusiana na utoaji wa huduma kwa umma. Kwa sababu hizo, uridhiwaji wa Mkataba huu ni fursa kwa Tanzania kuweka mifumo bora ya upashanaji wa habari zinazohusu huduma za umma zinazotolewa na Taasisi za Umma ili kuendana na matakwa ya Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 8 ya Mkataba inahusu uimarishwaji wa Utumishi wa Umma na Utawala kwa kuzitaka Nchi Wanachama kusisitiza matumizi ya teknolojia ya kisasa katika kutoa huduma kwa Wananchi. Kuridhiwa kwa Mkataba huu kutawezesha Tanzania kuendelea kuimarisha na kuboresha utendaji kazi katika Utumishi wa Umma kwa kutumia mbinu za kisasa ikiwemo matumizi ya teknolojia katika kuwatumikia Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 11 inahusu mgongano wa masilahi katika Utumishi wa Umma na Ibara ya 12 inahusu kuzuia na kupambana na rushwa katika Utumishi wa Umma.

Kuhusu mgongano wa masilahi, Mkataba unazuia Watumishi wa Umma kushiriki katika maamuzi ambayo wana masilahi binafsi. Mkataba unazitaka Nchi Wanachama kutunga sheria za kudhibiti mgongano wa masilahi kwa Watumishi wa Umma. Aidha, Mkataba unazitaka Nchi Wanachama kuweka mikakati madhubuti ya kupambana na rushwa ikiwemo kuanzisha taasisi zinazojitegemea na kupambana na rushwa pamoja na kutoa elimu kwa umma juu ya mikakati ya kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiasi kikubwa Tanzania imeshaanza kutekeleza masharti yaliyomo katika ibara hizi pamoja na kuwa bado haijaridhia Mkataba huu. Hata hivyo, kuridhiwa kwa Mkataba huu kutasaidia nchi kuendelea kuimarisha mifumo yake ya kukabiliana na changamoto zinazoikabili, mapambano dhidi ya rushwa na mgongano wa masilahi katika Utumishi wa Umma. Mkataba unasisitiza kuhusu uboreshaji wa mazingira ya kazi katika Ibara ya 16, stahili za watumishi wa umma katika Ibara ya 17 na haki za watumishi ikiwemo likizo, hifadhi ya jamii na mafao ya uezemi katika Ibara ya 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuridhiwa kwa Mkataba huu kutawezesha nchi yetu kuendelea kuboresha mifumo ya sheria zinazosimamia masuala haya ili kuongeza tija katika shughuli za Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba huu ni mzuri na wenye tija kwa Taifa kwa kuwa unasisitiza Nchi Wanachama ikiwemo Tanzania, kufuata Misingi ya Utumishi wa Umma na utawala. Pamoja na kuwa kati ya nchi 53 Wanachama wa Umoja wa Afrika ni nchi mbili tu zimekwisharidhia Mkataba huu ambazo ni Kenya na Mauritius, Kamati yangu inashauri Bunge lako Tukufu kuridhia Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaona kuwa manufaa makubwa nchi yetu itayapata ikiwa itaridhia Mkataba huu kama tulivyoeleza hapo juu. Aidha, Kamati inaendelea kushauri kuwa Taifa letu litekeleze kwa ukamilifu wake Mkataba huu kwa kutunga sheria zinazoendana na matakwa ya Mkataba huu kama ambavyo imekuwa ikifanya katika Mikataba mingine ambayo nchi yetu imekwisharidhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuhitimisha, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii adhimu ili niweze kuwasilisha Maoni ya Kamati kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia na Kuijunga na Mkataba wa Misingi na Kanuni za Utumishi wa Umma na Utawala Barani Afrika (*The African Charter on Values and Principles of Public Service and Administration*, 2011).

Namshukuru Mheshimiwa Celina O. Kombani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma) na Wataalam wa Wizara hiyo, kwa kutoa ufanuzi uliohitajika katika Kikao cha Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati hii kwa michango yao mizuri na ninaomba kwa kazi kubwa waliyoifanya, nitaje majina yao.

Mheshimiwa Gosbert Blandes - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Abbas Mtemvu, Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mheshimiwa Nimrod Elirehema Mkono, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Fakharia Shomari, Mheshimiwa Rukia Ahmed, Mheshimiwa Ali Seif, Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir, Mheshimiwa Mustafa Akunaay, Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Deogratius Ntukamazina, Mheshimiwa William Ngeleja, Mheshimiwa Nyambari Nyangwine, Mheshimiwa Ramadhani Saleh, Mheshimiwa Zahra Hamad, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha na mimi mwenyewe Jasson Rweikiza - Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, nawashukuru Ndugu Mariamu Ndulugu na Ndugu Matamus Fungo, Makatibu wa Kamati hii, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati. Nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Dkt. Kashililah - Katibu wa Bunge, kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali na kuridhia kuijunga na Mkataba wa Misingi na Kanuni za Utumishi wa Umma na Utawala Barani Afrika (*The African Charter on Values and Principles of Public Service and Administration*, 2011).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (*Makofij*)

MWENYEKTI: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati. Sasa naomba nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Tundu Lissu!

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa ruhusa yako kutoa Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu kuhusu Azimio la Kuridhia Mkataba wa Misingi na Kanuni za Utumishi wa Umma na Utawala Barani Afrika wa Mwaka 2011 (*The African Charter on Values and Principles of Public Service and Administration*, 2011).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufanya hivyo kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge lako Tukufu za Mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa Misingi na Kanuni za Utumishi wa Umma na Utawala Barani Afrika (*The African Charter on Values and Principles of Public Service and Administration*), ulikubaliwa na Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika katika kikao cha kawaida cha Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika kilichofanyika Addis Ababa, Ethiopia mnamo tarehe 31 Januari, 2011.

Huu ni Mkataba wa Kimataifa. Kwa sababu hiyo, Ibara ya 29(1) ya Mkataba huu imeweka masharti ya kusainiwa, kuridhiwa au kuthibitishwa na Nchi Wanachama kufuatana na taratibu zao za Kikatiba. Kwa Tanzania kama zilivyo nchi nyingine zinazofuata mila na desturi za Kisheria na Kikatiba za Jumuia ya Madola, Mikataba yote ya Kimataifa inayosainiwa na nchi yetu, inatakiwa kuridhiwa na Bunge lako Tukufu. Ndiyo maana Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 imelipa Bunge lako Tukufu mamlaka ya kujadili na kuridhia Mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa kwa mujibu wa orodha ya nchi zilizosaini, kuridhia na kuwasilisha nyaraka za kuridhia iliyowasilishwa pamoja na Azimio hili, ni Nchi Wanachama 21 tu ndizo ambazo zimesaini Mkataba huo.

Kwa kufuatana na Ibara yake ya 30(1), Mkataba huu utaanza kutumika baada ya Nchi Wanachama 15 kuwasilisha nyaraka za kuuridhia. Hadi sasa kwa mujibu wa orodha ya Nchi Wanachama zilizousaini, kuuridhia na kuwasilisha nyaraka za kuuridhia ni Nchi Wanachama mbili tu; Kenya na Mauritius ndizo ambazo zimesaini na kuridhia Mkataba huu. Kwa sababu hiyo, Mkataba huu haujapata nguvu za kisheria na kuanza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, orodha ya Nchi Wanachama zilizosaini, kuridhia na kuwasilisha nyaraka za kuridhia, inaonyesha kwamba, katika Nchi Wanachama 21 ambazo zimeshasaini Mkataba huu hadi sasa, Tanzania ni Nchi Mwanachama wa 21, yaani wa mwisho katika kusaini Mkataba huu. Orodha hii inaonyesha kwamba, Tanzania ilisaini Mkataba huu tarehe 19 Septemba, 2012. Kwa maelezo ya mtoa hoja mbele ya Kamati, Tanzania ilisaini Mkataba huu bila masharti yoyote. Leo tarehe 25 Machi, 2015, yapata miaka minne na miezi miwili tangu Mkataba huu ukubaliwe na Wakuu wa Nchi Wanachama akiwemo Rais Dkt. Jakaya Kikwete na miaka miwili na miezi sita tangu tulipousaini, ndiyo Bunge lako Tukufu linaombwa na Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi kuuridhia Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu inaamini kwamba, Rais Dkt. Jakaya Kikwete alikwenda kwenye Kikao cha Wakuu wa Nchi Wanachama wa Mkataba huu, akijua fika kwamba Mkataba huu utapitishwa na kikao hicho.

Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu inaamini kwamba, Serikali hii ya CCM ilimpeleka Rais Kikwete Addis Ababa ikijua kwamba siyo tu kwamba atatakiwa kushiriki katika sherehe za upitishwaji wa Mkabata huu, bali pia Serikali yake itatakiwa kuusaini Mkataba wenyewe. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu inaamini kwamba, Serikali hii ya CCM ilikuwa inajua kwamba, baada ya kuusaini itatakiwa ili kutimiza masharti husika ya Kikatiba, kuuleta Mkataba huu mbele ya Bunge lako Tukufu ili upate ridhaa ya chombo hiki kikuu cha uwakilishi wa Wananchi.

Hali kadhalika, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu, inapenda kuamini kwamba, Tanzania ilishiriki katika kuupitisha Mkataba huu kwa nia ya kuutekeleza na siyo kwa lengo la kujionyesha tu kuwa na sisi ni sehemu ya Umoja wa Afrika. Kwa sababu zote hizi, pengine swali la kwanza ambalo Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu inataka lijibiwe na mtoa hoja ni kwa nini imechukua muda mrefu kiasi hicho kwa nchi yetu kusaini Mkataba huu na kwa Serikali ya CCM kuleta Azimio la kuuridhia mbele ya Bunge lako Tukufu?

Swali hili ni muhimu kujibiwa kwa ufasaha kwa sababu imekuwa *fashionable* kwa Serikali hii ya CCM kusaini Mikataba ya Kimataifa kwa mbwembwe ili kujionyesha kwenye Jumuia ya Kimataifa kwamba, inatilia maanani matakwa ya Jumuia hiyo kuhusu masuala yanayohusu Mikataba hiyo.

Hata hivyo, mara baada ya kusaini Mikataba hiyo, Serikali hii ya CCM husahau wajibu wake kwa Jumuia ya Kimataifa kwa kusahau au kushindwa au kupuuzia kuileta Mikataba hiyo Bungeni ili iweze kupata ridhaa ya Bunge lako Tukufu. Mifano miwili inathibitisha tabia hii mbaya ya Serikali hii ya CCM. (Makof)

Mfano wa kwanza ni Mkataba wa Afrika Kuhusu Chaguzi, Demokrasia na Utawala Bora (*The African Charter on Democracy, Elections and Governance*), uliopitishwa na Kikao cha Kawaida cha Wakuu wa Nchi na Serikali wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika tarehe 30 Januari, 2007. Hadi sasa Mkataba huu muhimu umesainiwa na Nchi Wanachama 38 kati ya 53 wa Umoja wa Afrika. Tanzania siyo moja ya nchi hizo miaka minane baada ya kupeleka ujumbe mkubwa wa watalii na wafanya shopping kwenye kikao cha AU kilichoupitisha Mkataba huu. (Makof)

Kwa sababu hiyo, siyo na haiwezi kuwa ajabu kwamba, kumekuwa na maandalizi ya hovyo kama tunayoyashuhudia hivi sasa ya Kura ya Maoni kuhusu Katiba Inayopendekezwa. Na ndiyo maana hadi sasa Tume ya Taifa ya Uchaguzi haijaanza maandalizi hata ya Uchaguzi Mkuu wa baadaye mwaka huu. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Bunge lako Tukufu, inapenda kujua kutoka kwa mtoe hoja na kwa Serikali hii ya CCM ni lini Mkataba huo wa Uchaguzi, Demokrasia na Utawala Bora utasainiwa na Serikali hii na kuleta Bungeni kwa lengo la kupata ridhaa ya Bunge lako Tukufu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa pili unahuhi Itifaki ya SADC Kuhusu Fedha na Uwekezaji (*SADC Protocol on Finance and Investment*) ya Mwaka 2006, iliyotiwa saini na Wakuu wa Nchi 14 wa Jumuia ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika, yaani SADC, katika Mji wa Maseru Lesotho mnamo tarehe 18 Agosti, 2006. Illichukua zaidi ya miaka minane hadi mwaka jana kwa Itifaki hiyo kuleta mbele ya Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kupata ridhaa inayotakiwa Kikatiba na kwa mujibu wa Itifaki yenye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maeleo ya mtoe hoja mbele ya Kamati ya Bunge lako Tukufu ya Katiba, Sheria na Utawala, Nchi Wanachama zinatambua kuwa Mkataba huu ni nyenzo muhimu katika kujenga Utumishi wa Umma wa Kisasa, wenye uadilifu na weledi utakaoliwezesha Bara la Afrika kukabiliana na changamoto mbalimbali za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Kama kauli hii ni ya kweli na siyo propaganda za kisiasa za Serikali hii ya CCM katika mwaka huu wa uchaguzi, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu inamwomba mtoe hoja aliambie Bunge lako Tukufu ni sababu zipi kwa maoni ya Serikali hii ya CCM, zimezifanya Nchi Wanachama nyingine za Mkataba huu kutokuuridhia hadi sasa; au pengine ndiyo kusema ni Kenya na Mauritius pekee katika Bara zima la Afrika ambazo zinataka kuwa na Utumishi wa Umma wa Kisasa wenye uadilifu na weledi utakaoliwezesha nchi hizo kukabiliana na changamoto mbalimbali za kiuchumi, kisiasa na kijamii?

Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu inapenda kujua kutoka kwa mtoe hoja kama baada ya zaidi ya miaka minne tangu Nchi Wanachama 53 wa Umoja wa Afrika kuukubali Mkataba huu ni Nchi Wanachama mbili tu ndiyo zimeuridhia wakati takribani asilimia 40 tu ya Nchi Wanachama zimeusaini; kulikuwa na haja gani ya kuuharakisha Mkataba huu ambao ni wazi kwa ushahidi huu Nchi Wanachama hazikuwa tayari kubanwa na masharti yake?

Vilevile, tunapenda kuelezwaa na mtoe hoja, kwa speed hii ya Nchi Wanachama mbili tu kuridhia kila baada ya miaka minne ni lini kwa matarajio ya Serikali hii ya CCM Mkataba huu utafikisha ridhaa ya Nchi Wanachama 15 inayotakiwa ili Mkataba uweze kupata nguvu za kisheria kama inavyotakiwa na Ibara yake ya 30(1)?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuchelewa kuusaini Mkataba huu kwa zaidi ya miaka miwili na nusu baada ya kupitishwa na Wakuu wa Nchi Wanachama kunatilia shaka kuwepo na utashi wa kisiasa wa Serikali hii ya CCM juu ya Mkataba huu. Kushindwa kwa zaidi ya miaka minne kuuleta mbele ya Bunge lako Tukufu ili upate ridhaa ya chombo hiki cha uwakilishi na hivyo kuwa sehemu ya sheria za nchi yetu, kunahoji nia na malengo ya kuuleta sasa katika mwaka wa uchaguzi!

Hata hivyo, haya siyo mambo pekee muhimu yanayoitatiza Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu kuhusu Mkataba huu. Yapo mambo mengine ambayo yanatufanya tuhoji nia na malengo halisi ya Serikali hii ya CCM kuuleta Mkataba huu kwa sasa. Mambo hayo ni haya yafuatayo na tunamwomba mtoa hoja ayajibu kwa ukweli na ufasaha ili Bunge lako Tukufu liridhike kwamba, Mkataba huu unaletwa kwa sasa kwa ajili ya manufaa ya nchi yetu na siyo kwa ajili ya malengo ya kisiasa ya Serikali hii ya CCM katika mwaka huu wa uchaguzi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 3(1) ya Mkataba huu inatambua usawa wa watumiaji wote wa Utumishi wa Umma na Utawala. Ibara ya 3(2) inakataza aina zote za ubaguzi kwa msingi wowote, ikiwa ni pamoja na asili ya kutoka, rangi, jinsia, ulemavu, dini, ukabila, msimamo wa kisiasa, uanachama wa chama cha wafanyakazi au vyama vingine halali.

Ibara ya 3(7) inahusu uhamashaji na hifadhi ya haki za binadamu za watumiaji na Mawakala wa Utumishi wa Umma. Neno watumiaji limetafsiriwa kwenye ibara ya kwanza ya mkataba kumaanisha mtu yeyote wa asili au wa kisheria anayehitaji huduma ya utumishi wa umma. Kwa upande wake maneno Mawakala wa Utumishi wa Umma yametafsiriwa kwenye ibara hiyo hiyo kuwa ni mfanyakazi au mwajiriwa yeyote wa dola au wa taasisi zake ikiwa ni pamoja na wale walioteuliwa au kuchaguliwa kuendesha shughuli kwa jina la au kwa niaba ya dola katika ngazi zake zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misingi iliyotajwa katika Ibara ya 3 ya Mkataba huu imefafanuliwa kwa ufasaha mkubwa katika Sura ya 4 ya Mkataba inayohusu haki za Mawakala wa Utumishi wa Umma. Hivyo; kwa mfano, Ibara ya 14(1) inazitaka Mamlaka za Utumishi wa Umma na Utawala kuendeleza usawa mionganoni mwa Mawakala wake. Ili kufikia lengo hilo, Ibara ya 14(2) inaelekeza kwamba, Utumishi wa Umma na Utawala hautahamasisha au kuendeleza ubaguzi kwa misingi ya asili, rangi, jinsia, ulemavu, dini, ukabila, msimamo wa kisiasa au sababu nydingine yoyote. Aidha, kwa mujibu wa Ibara ya 15(1), Mawakala wa Utumishi wa Umma watakuwa na uhuru wa maoni kwa kuzingatia hadhi yao kama Watumishi wa Umma. Vilevile, kufuatana na masharti ya Ibara ya 15(2), Mawakala wa Utumishi wa Umma watakuwa na haki ya kuunda au kuijunga na mashirika, vyama vyta wafanyakazi au makundi mengine ili kuendeleza na kulinda haki zao kwa mujibu wa sheria za nchi.

Muhimu zaidi, Ibara ya 15(3) inatamka wazi; bila kujali sheria za nchi, uanachama au ukosefu wa uanachama katika chama cha siasa, hautaathiri kwa namna yoyote ile utumishi wa Mtumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwa mujibu wa masharti haya ya Mkataba huu tunaotakiwa kuupatia nguvu za kisheria katika nchi yetu kwa kuridhia Azimio hili kwamba, watumishi wote wa umma wa ngazi zote, wana haki ya kuijunga na vyama vyta wafanyakazi pamoja na mambo mengine, vyama vyta siasa vyenye usajili halali kwa mujibu wa Sheria za Tanzania.

Kwa mujibu wa Ibara ya 34 ya Mkataba huu, Tanzania ilikuwa na haki ya kuweka masharti, yaani reservations, kwa Lugha ya Sheria za Kimataifa, wakati wa kusaini Mkataba huu ili tusije tukafungwa na masharti ya Mkataba yanayopingana na Katiba na sheria mbalimbali za nchi yetu.

Hata hivyo, kama tulivyosema mwanzoni, Serikali hii ya CCM ilisaini Mkataba huu bila kuweka au kuingiza masharti yoyote. Kwa maana hiyo, Tanzania ilikubali masharti yote ya Mkataba huu. Sasa kwa maana hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu, inamwomba mtoe hoja aliambie Bunge lako Tukufu kama Majaji wa Mahakama ya Rufani ya Tanzania, Majaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Wasajili wa Mahakama za ngazi zote na Mahakimu wa ngazi zote, ambao wote ni Mawakala wa Utumishi wa Umma kwa mujibu wa Mkataba huu, wana haki ya kuijunga na vyama vya wafanyakazi au vyama halali vya siasa licha ya kupigwa marufuku kufanya hivyo na Ibara ya 113 (a) ya Katiba. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu inapenda kuelezwaa na mtoe hoja kama watu wanaohusika na uchaguzi kama wanavyotafsiriwa na Katiba yetu na ambao ni Mawakala wa Utumishi wa Umma kwa mujibu wa Mkataba huu sasa wataruhusiwa kuijunga na vyama vya siasa licha ya kukatazwa kufanya hivyo na Ibara ya 74(14) ya Katiba ya nchi yetu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanaohusika na uchaguzi kwa mujibu wa Katiba yetu ni Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi, Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi, Wajumbe wote wa Tume ya Uchaguzi, Mkurugenzi wa Uchaguzi pamoja na Watumishi wote wa Tume ya Uchaguzi na Wasimamizi wote wa Uchaguzi katika Miji na Wilaya zote. Hii ni kwa mujibu wa Ibara ya 74(15) ya Katiba na wote hawa kwa mujibu wa Mkataba huu ni Mawakala wa Utumishi wa Umma na wanaruhusiwa kuijunga na vyama vya siasa na vyama vya wafanyakazi. (Makofii)

Vilevile, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu inataka kujua kutoka kwa mtoe hoja, endapo wanajeshi kama wanavyotafsiriwa na Ibara ya 147(4) ya Katiba ambao pia ni Mawakala wa Utumishi wa Umma, wana haki ya kuanzisha au kuijunga na vyama vya wafanyakazi au vyama halali vya siasa kwa mujibu wa Mkataba huu licha ya makatazo ya Ibara ya 147(3) ya Katiba? (Makofii)

Kama majibu ya maswali haya ni hapana, basi Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu inaomba ielezwe na mtoe hoja kwa nini Serikali hii ya CCM haikuweka reservations kwa Ibara ya 3(2) pamoja na Sura ya Nne ya Mkataba huu ili kutambua na kuhalalisha makatazo ya Ibara za 74(14), 113(a) na 147(3) za Katiba yetu. Au ndio kusema tulipeleka ujumbe wa Tanzania Addis Ababa kwa lengo la kwenda kutalii na kufanya shopping badala ya kwenda kupitisha Mkataba kwa kuzingatia masharti ya Katiba yetu kuhusu Utumishi wa Umma? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba Serikali hii ya CCM inaweza kuwa inaandaa mazingira ya kisheria ya kuwa na au kuingiza au kuhalalisha uwepo wa Makada wa CCM katika taasisi za dola zinazokataza uanachama wa vyama vya siasa siyo hofu au dhana njama, yaani conspiracy theory isiyokuwa na msingi wowote.

Itakumbukwa kwamba, mwaka 2012 Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu, ilihoji uhalali wa Wanajeshi kuteuliwa kuwa Wakuu wa Wilaya. Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu ilisema yafuatayo na ninaomba kunukuu: "Wakuu wa Mikoa na Wilaya wote ni na wanatakiwa kuwa Wanachama wa CCM." Hii ni kwa sababu tangu kuanzishwa kwake mwaka 1977, Wakuu wa Wilaya wamekuwa ni Wajumbe wa Vikao vyote Vikuu vya CCM katika ngazi ya Wilaya. Kwa mfano, kwa mujibu wa Katiba ya CCM, Toleo la Mwaka 1982, Mkuu wa Wilaya ni Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Wilaya, ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Wilaya na ni Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Wilaya.

Hata baada ya miaka 30 tangu Toleo hilo la Katiba ya CCM litolewe na licha ya miaka 20 ya Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa nchini, hali bado ipo vilevile kuhusiana na nafasi ya Wakuu wa Wilaya katika vikao rasmi vya CCM. Ndiyo maana kwa mujibu wa Katiba ya CCM, Toleo la 2010, Mkuu wa Wilaya ni Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Wilaya, ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya na ni Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie kusema kwamba, Wakuu wa Wilaya nao ni Mawakala wa Utumishi wa Umma kwa mujibu wa Mkataba tunaoombwa kuuridhia leo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya utata wa Kikatiba unaohusu Wanajeshi kuwa Wakuu wa Wilaya na Mikoa na hivyo kulazimika kuwa Wanachama wa CCM na washiriki wa vikao vyake mbalimbali vya maamuzi, Serikali hii ya CCM imeendelea kuwateua Wanajeshi kwenye nafasi hizo kama uteuzi wa hivi karibuni wa Zelote Stephen, ambaye miaka michache iliyopita alikuwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa kuwa Mkuu wa Wilaya. Aidha, sasa kuna hofu ya msingi kwamba, hata Majaji wetu wanaweza wasiwe salama sana kama taarifa za hivi karibuni za vyombo vya habari zilizomhusisha aliyekuwa Jaji Mkuu wa Tanzania Augustino Ramadhani na mbio za kuwania Urais kwa Tiketi ya CCM kwenye Uchaguzi Mkuu baadaye mwaka huu zitakuwa za kweli. (Makofi)

Kwa Maoni ya Kambi Rasmi ya Bunge lako Tukufu, kwa masharti ya Ibara ya 3 na Sura ya 4 ya Mkataba huu, itakuwa ni halali sasa kwa Mawakala hawa wa Utumishi wa Umma kuwa Wanachama wa CCM licha ya marufuku zilizopo kwenye Ibara za 74(14), 113(a) na 147(3) za Katiba. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu, inamwomba mtoa hoja kutoa ufanuzi juu ya mgongano huu wa wazi kati matakwa ya Mkataba tunaoombwa kuuridhia na masharti tajwa ya Katiba yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ushahidi mwengine unaothibitisha kwamba, Serikali hii ya CCM haina utashi wa kisasa wa kutekeleza matakwa na masharti ya Mkataba huu. Ushahidi huu unahu haki ya Watumishi wa Umma wa ngazi za juu kuijunga na vyama vya wafanyakazi na kuchaguliwa kuwa viongozi wa vyama hivyo. Kwa utaratibu wa sasa wa kisheria, Watumishi hawa wa Umma wanaruhusiwa kufanya hivyo. Hii ipo katika Kifungu cha 9 (1) (a) na 2 (c) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, sura ya 366. Hata hivyo, mwezi Aprili, 2013, Katibu Mkuu Kiongozi alitoa Waraka Na. 2 wa Mwaka 2013 uliowataka Watumishi wa ngazi za juu Serikalini ambao pia ni Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi, kuijuzulu nafasi zao za uongozi katika vyama vya wafanyakazi au vinginevyo wataondolewa katika Utumishi wa Umma.

Katika kesi ya *Tanzania Local Government Workers Union (TALGWU)* na wenzake wawili dhidi ya Katibu Mkuu Kiongozi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Divisheni ya Kazi ya Mahakama Kuu ya Tanzania iliizua Serikali kutekeleza Waraka huo kwa Watumishi wote wa Umma. Uamuhi huo ultolewa tarehe 9 Aprili, 2014. Badala ya kutii uamuhi huo wa Mahakama Kuu na badala ya kutii matakwa ya Mkataba huu ambao unalinda na kuhifadhi haki ya Mawakala wa Utumishi wa Umma kuijunga na Vyama vya Wafanyakazi, sasa Serikali hii ya CCM, imeleta Muswada mbele ya Bunge lako Tukufu wa kurekebisha, pamoja na mengine, Kifungu cha 9 cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini kwa lengo la kuifuta haki ya Watumishi wa ngazi za juu wa Umma kuijunga na kuwa Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ushahidi huu, Serikali hii ya CCM inazungumza kwa ndimi mbili kama za nyoka: Kwa upande mmoja inaleta kwenye Bunge hili Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa unaotambua, kulinda na kuhifadhi haki ya watumishi wa ngazi zote za Utumishi wa Umma kuijunga na kuwa viongozi wa vyama halali vya wafanyakazi. Kwa upande

mwagine, Serikali hiyo hiyo inaleta Muswada wa Sheria katika Bunge hili hili ambao ukipitishwa na kuwa sheria, utafuta kabisa haki hiyo ya Mawakala wa Utumishi wa Umma!

Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu, inawaomba Wabunge wote, kama kweli wanataka kupitisha Azimio hili kama wanavyoombwa na mtoa hoja, wawe tayari kukataa mapendekezo ya Muswada huo ya kufuta haki ya watumishi wa ngazi za juu ya kuijunga na kuwa Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi pale utakapoletwa mbele ya Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa kuwa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya mrefu, naomba kuwasilisha Maoni haya kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. (Makof)

MWENYEKITI: Mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Wenje!

MHE. EZEKIAH D. WENJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kupewa fursa hii ya kuwa mchangiaji wa kwanza katika Azimio hili muhimu siyo tu kwa Bara la Afrika bali pia katika nchi yetu. Tunapozungumzia suala la Utawala Bora katika Afrika ni suala linalogusa sana. Wakati mwagine huwa ninajuliza kwa nini Afrika ni maskini?

Jibu kubwa ninalolipata ni kwa sababu ya matatizo makubwa tuliyonayo katika suala la Utawala Bora na Utawala katika Bara la Afrika. Nimesoma hili Azimio vizuri sana, lina masuala mengi mazuri yanayohusu Utawala Bora; kwa mfano, ukisoma Article 3(8) inazungumzia masuala ya uwajibikaji, uadilifu na uwazi. Masuala mengi sana mazuri ambayo kwa bahati mbaya kuna mengine hata kwenye Katiba Inayopendekezwa mliamua kuyachomoa halafu leo hapa tunataka kuridhia Mkataba ambapo masuala mengine hata kwenye Katiba mlikataa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizungumzia suala la uwajibikaji, uadilifu na uwazi, unapozungumzia suala la uadilifu kinyume chake ni rushwa. Leo mimi ninaamini kwamba, tatizo kubwa la umaskini lililopo Afrika ni tatizo linalotokana na ukosefu wa uadilifu. Akina mama wanakosa maji vijiji kwa sababu pesa ambazo Serikali ingetumia kupelekea maji, kuna watu wanakula kwa sababu ya ukosefu wa uadilifu.

Watu wanakosa dawa hospitalini hapa Afrika, akina mama wanafariki wakiwa wajawazito, watoto wachanga wanafariki, kwa sababu hakuna uadilifu Afrika. Nchi za Afrika tunajengewa barabara mbovu hata Dar es Salaam mimi *ninaziita disposable roads* zinazojengwa Dar es Salaam. Inajengwa barabara leo, baada ya miezi mitatu hakuna barabara, kwa sababu ya rushwa, ukosefu wa uadilifu Barani Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo yapo lukuki; ukienda hospitalini Afrika watu wanalala chini hadi Muhibili ambayo ni National Referral Hospital watu wanalala chini kwa sababu ya ukosefu wa uadilifu Afrika. Afrika tuna migodi, chukulia Tanzania tuna migodi mingi hata huko Kanda ya Ziwa tunakotoka, ambayo haina faida kwa wenyeji ni kwa sababu ya aina mikataba mibovu tunayoingia kwa sababu ya ukosefu wa uadilifu Afrika. (Makof)

Afrika watu wanapata tabu, hakuna kazi, watu wanakufa wakiwa na umri mdogo, vijana wanaendesha bodaboda toka asubuhi mpaka jioni, kwa sababu wanaotutawala Afrika hawana uadilifu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana ninasema, tunapozungumzia masuala ya Utawala Bora Afrika ni suala linalogusa sana moyo, ni suala linalogusa hisia. Afrika ni Bara

ambalo tuna vitu vingi, Mwenyezi Mungu alitupa rasilimali nyngi, lakini hatuzitumii ipasavyo kwa sababu ya ukosefu wa uadilifu uliopo Barani Afrika. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wanakaa chini shulen Tanzania kwa sababu ya ukosefu wa uadilifu. Shule hazina chaki, watoto wanakaa chini, hakuna maabara, hakuna maktaba, kwa sababu ya ukosefu wa uadilifu Barani Afrika. Fedha zinapatikana nyngi, wananchi wanalipa kodi, lakini bado tunawalazimisha kuchangia maabara kwa sababu ya ukosefu wa uadilifu Barani Afrika. (Makof)

Fedha zinazokusanywa, kodi inayolipwa inaliwa, kwa sababu hakuna *discipline* katika kutumia rasilimali chache zilizopo ambazo Serikali inachukua kutoka kwa Wananchi. Afrika kuna matatizo mengi, ingawa mimi Wenje ninaamini kuwa *there are still future in Africa*, lakini future Afrika itapatikana kwa Azimio kama hili tunaloridhia. Tatizo siyo Sheria Afrika, tatizo siyo Azimio Afrika, Sheria zipo; ukisoma article 12 inazungumzia masuala ya *preventing and combating corruption*.

Hata hapa Tanzania kuna PCCB; hivi PCCB imetusaidia kiasi gani? Kwa hiyo, tatizo tulilonalo Afrika na Tanzania ikiwemo siyo Azimio, tatizo siyo Sheria, Sheria tunazo; tuna PCCB, tuna Polisi, tuna Usalama wa Taifa, lakini ndiyo bado kuna scandal kubwa Tanzania, ndiyo bado kuna scandal kubwa Afrika. Zungumzia masuala ya *Anglo-leasing* kama ya Kenya utakuta Afrika, zungumzia masuala ya *EPA* utayakuta Afrika, zungumzia masuala ya Richmond utayakuta Afrika, zungumzia masuala ya mabilioni ya Escrow unayakuta Afrika! Wananchi wanakufa kwa kukosa maji ya kunywa lakini Afrika, *huge continent with corrupt Leaders*.

Mheshimiwa Mwenyekiti ukosefu wa uadilifu unaua Afrika. Changamoto ninayota kwa Serikali yetu na Viongozi wote Afrika, kwa sababu nchi nyngi zinataka kuridhia Azimio hili siyo Tanzania tu, *is high time we walk the talk*. Tumechoka na hizi Serikali za Afrika zinazosema na kusema, sasa tunahitaji Serikali itakayosema na kutenda. Ukisoma Article 4 ya Mkataba huu inazungumzia masuala ya Haki za Binadamu, ni Afrika peke yake ndiyo polisi anaweza kuua na kukupa kesi anayotaka, ni hapa Afrika. (Makof)

Afrika peke yake kuna kipindi tulisikia sehemu inayoitwa Dumila, kuna polisi walichukua kichwa cha mtu wakapeleka kwenye nyumba ya mtu ili wamkamate wamfunge kwa sababu wana matatizo naye. *That can only happen in Africa. Is only in Africa* ndiyo Mwandishi wa Habari kama Mwangosi anapigwa risasi na polisi; *that can only happen in Africa*. Hapa Afrika ndiyo polisi wanaua watu, wakiua watu wanakemewa na Serikali, yaani hapa watu wanapigwa halafu Wabunge wengine wanasema wanawapongeza kwa sababu wamewapiga wahusika wakuu; *that can only happen in Africa*. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio hili linazungumzia masuala ya Haki za Binadamu, lakini ni nchi yetu tu hapa Tanaznia peke yake ndiyo kuna *huge violation of Human Rights, is only in Africa* ndiyo Waziri Mkuu anaweza kusimama pale akasema wapigwe tu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio hili ni muhimu kama tutaamua kutekeleza kwa vitendo haya masuala yaliyoandikwa kwenye Azimio hili *Africa that is why is called dark continent*; kwa sababu masuala yanayotokea Afrika leo yalipaswa kufanyika three hundred years back ndiyo bado yanafanyika leo. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *is only in Africa* ndiyo watu wanauawa hovyo hovyo. Ukisoma *Human Rights Report* hata ya Tanzania ni mbovu, *is very dark Human Rights Reports* za Tanzania. Halafu ndiyo bado wanaume wa Afrika *in the name of Leadership* ndiyo bado wanapambana kujitoa ICC, wanataka kuvunja room statute ili watu wauawe vizuri, ili political parties viongozi

wapigwe vizuri. Wanaume wanataka kujitoa, wana-mobilise all over Africa kujiondoa kwenye room statute.

Halafu hapahapa tunasaini Mkataba in Human Rights and Governance sijui ku-promote good leadership and all that in Africa. Mimi ninasema, tunaweza tukaridhia Mikataba mingi kama hakuna political will ya kusema na kutenda, kufanya haya mambo kwa vitendo, we are doing nothing; na hata hapa tunafanya tu rubber stamping process, alivyosema Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuwa, tunaingia kwenye Mikataba kama hii kwa mbwembwe sana just to be seen, kuonekana tu huku Duniani kuwa na sisi tumeridhia, lakini in real sense kwenye utekelezaji actual hakuna kitu kinachotokea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata tukisaini mikataba 100 kama hakuna ile push from the heart ya kutenda haya tunayosaini, hakuna kitu tutakachobadilisha Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika na watu wote wanajua Duniani kwamba, Afrika na ukichukua hata mfano wa Tanzania, rasilimali tulizonazo kama Taifa ni aibu leo watu wetu kukosa maji ya kunywa, ni aibu leo watu wetu kukosa barabara, ni aibu leo watu wetu kukosa dawa hospitalini, ni aibu leo wanawake na watoto kufa Afrika kwa vifo ambavyo vinatibika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie kwa kusema kwamba, ninaunga mkono Azimio hili, lakini Serikali yetu iende...

Ninashukuru sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Wenje, lakini mimi ninaamini Tanzania haiendi kwenye mikutano kwa kufanya shopping wala kwenda kujionyesha. Ninaamini hivyo, kwa sababu hata kwenye delegation hizo huwa Wabunge tumo.

Mchangiaji wetu wa pili atakuwa Mheshimiwa Felix Mkosamali, atafuatiwa na Mheshimiwa John Mnyika!

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na mimi kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia Azimio la Kuridhia Misingi na Kanuni za Utumishi wa Umma. Kabla hujachangia kuna maswali ya kujiliza kama walivyoeleza watu wengine kwamba; tunapitisha Mkataba kama huu ili itokee nini? Ili iweje kwa Serikali ya namna hii? (Makofi)

Nimejaribu kuangalia ratiba yetu, toka tumefika tunapitisha Sheria na Mikataba hii miwili, Sheria hizi tutakazopitisha zote ukiziangalia, zinaanzisha Vyombo, Taasisi, Idara, Tume, Kamati na nini, lakini hakuna kinachofanyika; kwa sababu uwezo wa CCM kuongoza umeshafika mwisho. Ninawashangaa hata Wananchi amba wanazungumzia Wagombea Urais wa CCM, hakuna mtu hata mmoja kwenye CCM anayeweza kuiongoza nchi hii. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utunge Sheria nchi hii, Legal and Human Rights Center wamefanya utafiti, utekelezaji wa Sheria nchi hii haufiki asilimia 40. Kwa hiyo, hata uridhie Mikataba 10,000 kwa hawa watu, hawawezi kuitekeleza kwa asilimia 40. Hapa wewe angalia, wanakwambia tunaridhia ili tuweke mikakati ya kuzuia ya kupambana na rushwa. Hosea aliwaambia kabla ya Bunge la Katiba kwamba, Sheria yangu mniingize kwenye Katiba mnipe meno; mmefika hapa kwenye Bunge la Katiba mmeepiga piga yowe mmeacha vilevile! Leo mmeleta tena Muswada kwamba, tutaweka mikakati ya kupambana na rushwa. Sasa hivi ninyi mafanya maigizo au mko serious mnaendesha nchi? (Kicheko/Makofi)

Hii ni drama, ninyi hamna uwezo wa kupambana na rushwa wakati ninyi ni wala rushwa, hata tukipitisha huu Mkataba hamna uwezo wa kupambana na rushwa. Watumishi wa Umma huko ukienda kwenye Ofisi za Serikali unachelewa kuingia ndani, mmeshindwa hata tukipitisha hili. Sheria zilizopo tu mmeshindwa kuzitekeleza, tukipitisha hizi mtafanya nini? (Kicheko/Makofi)

MWONGOZO WA SPIKA

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chief Whip!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, ninaomba mwongozo wako, ajenda iliyoko hapa inayochangiwa ni kuhusu kuridhia Mkataba huu. Tunatakiwa kujikita katika ajenda tuliyonayo, badala yake wachangiaji wamehamisha hii ajenda na kuingia kwenye ajenda nyingine tofauti, pamoja na kutumia maneno ya kuudhi na maneno ambayo hayatoi afya katika mjaddala huu muhimu sana ambaa tunaendelea nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba mwongozo wako; hivi tunaendelea kufanya ajenda hii kwa maana na tafsiri ya malumbano yetu, ugombeaji wa Urais na vitu vingine au tunatakiwa kujikita katika ajenda iliyopo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo, kwa mtazamo wangu tunahama kwenye ajenda. Ninaomba mwongozo wako.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunazungumzia Azimio ambalo liko mbele yetu kuhusu Mkataba wa Misingi ya Kanuni za Utumishi wa Umma na Utawala Bora Barani Afrika. Mimi ninaomba Waheshimiwa Wabunge tuelewane, tunaridhia Mkataba huu na ninyi mmesema kwamba nchi nyingi zimesharidhia na nchi za Afrika ni chache. Ninaomba tujikite kwenye maudhui yaliyoko ndani ya huu Mkataba. Ninawaomba, kwa sababu ni kweli tunaenda mbali, naomba tujikite kwenye hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mkosamali!

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayozungumza ndiyo yamo humu labda kama huo Mkataba hauna. Kwa mfano, Kifungu cha 13 kinasema; "Public service agents shall declare their assets and income at the beginning, during and at the end of their service as prescribed in there National Laws and Regulations." Mbona mnapiga kelele? (Kicheko/Makofi)

Watumishi wa Umma wanatakiwa waeleze assets zao. Tunazungumza kila siku hapa, ninyi mmeshindwa kuipa fedha Sekretarieti ya Madili ya Viongozi wa Umma ili iwasimamie.

MWENYEKITI: Zungumza na Kiti usizingumze nao.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa si ndiyo ninazungumza mbona una-panic! (Kicheko/Makofi)

Ninachosema ni kwamba, CCM haina uwezo wa kusimamia Utumishi wa Umma, haina uwezo wa kukagua rasilimali, Mtumishi gani ameiba, hata ukipitisha hii hawawezi! Sheria iliyopo sasa hivi inasema, Watumishi tujaze fomu na sisi Wabunge, mimi toka nimeingia humu sijawahi kukaguliwa, watu hawakaguliwi, hawana pesa, tukiwapitishia hii ndiyo mtawea kukagua? Hamuwezi! Hivi vitu ni kupoteza muda, you are tired, hamna uwezo, mwisho wenu inatakiwa iwe mwaka huu. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ina sheria nyingi tumejaza maboksi kila sehemu, lakini hamna uwezo ninyi wa kufanya shughuli hizi. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmesema tuweke haki za binadamu, Utumishi wa Umma uzingatie haki za binadamu, ninyi hamna uwezo wa kulinda haki za binadamu. Serikali ya CCM ndio taasisi inayovunja haki za binadamu Tanzania kuliko taasisi yeyote. CCM mnnavunja haki kuliko taasisi yoyote. Mtapitisha hapa, tumeingiza ibara ya tisa inasema hivi haki za binadamu zimeanza kwenye Mkataba huu?

Mmeridhia mikataba mingapi ninyi ya haki za binadamu? Mmekwishardhia mikataba zaidi ya 20 ya haki za binadamu lakini hamtekelezi kitu hata kimoja, tukiwapitishia huu Mkataba mtafanya kitu gani? (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Martha Mlata!

MHE. MARTHA M. MLATHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe taarifa kwako kwamba, mzungumzaji anayeongea anazungumzia masuala ya uadilifu na kwamba Serikali ya CCM haiwezi imeshindwa. Ninataka nitoe taarifa kwamba, Serikali ya Chama cha Mapinduzi inaweza na ndio maana imeendelea kupata ridhaa hata kwenye Serikali za Mitaa na Vitongoji iliongoza, lakini bado yeye katika masuala ya uadilifu Mheshimiwa ana kesi, aseme uadilifu wake uko wapi? (Kicheko)

MWENYEKITI: Endelea Mheshimiwa Mkosamali!

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nafikiri alikuwa hafuatilii, ulikuwepo Bungeni wakati naanza kuchangia au ndio umekuja? Maana taarifa yake haihusiani na Muswada, anazungumzia mambo sijui ya nini! Kesi zilizoko Mahakmani hazipo hapa, wala hatuzungumzii hayo. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu zuia fujo basi, watu wanafanya vurugu.

MWENYEKITI: Wewe zungumza.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachosema, kwa mfano; Ibara ya 2(6) ya Mkataba inazungumza ku-improve working conditions za Wafanyakazi, wapate nyumba, wapate nini, wapate magari; mna ubavu? (Kicheko)

Sasa hivi ukienda huko kwa Mahakimu, nyumba za Mahakimu, Mahakama, nyingine watu wanaofuga kuku wa kisasa Dar es Salaam unakuta banda la kuku ni nzuri kuliko nyumba ya Hakimu, kuliko Mahakama. Tukipitisha hii ndio mtawezwa kuwapatia magari? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachosema, hawa watu wasitake kuchekesha jamii, mmeefeli. Hii ni procedure tu kwamba tunaridhia, hamna uwezo wa kufanya kitu chochote kwenye haya. Ninyi mna uwezo wa kujenga nyumba za Walimu? This is so worse, haiwezekani! Haya mnaleta tu hapa kupoteza, lakini you cannot... (Kicheko)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuelewane, wakati mwengine tunapojadili masuala ya msingi haya ni lazima tuweke utaratibu unaotakiwa wa Kibunge. Kwa mfano, Mheshimiwa Mbunge anaposema Seikali hii imeshindwa hiki, imeshindwa hiki, leo Serikali hii inapoanza kufanya mkakati mzito wa kujenga hizo nyumba za Walimu anazozitungumzia anataka kusema

haijafanya, barabara zinajengwa anataka kusema hazijajengwa, umeme umefika mpaka kwenye vijiji huko anataka kusema hakuna!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa huyu Mheshimiwa Mbunge anayechangia kwamba, zipo shughuli muhimu kabisa zinaonekana na Serikali hii imefanya; kwa hiyo, ajikite kwenye hoja iliyopo Mezani kwetu na siyo kusema hayo maneno ambayo siyo ya msingi na hayaendani na hoja iliyopo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mkosamali jikite kwenye hoja iliyopo!

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa hatuzungumzii mambo ya barabara. Sasa ninaendelea na Kifungu cha 15. Kifungu hiki kinazungumzia uhuru wa kupata habari na association.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa hawawezi kutengeneza mfumo wa watu kupata habari. Muswada wa Habari wameleta wameuficha. Mpaka sasa tumezunguka kila mahali tupate huo Muswada wa Habari tuusome, tuchangie, wameuficha halafu wanasema turidhie Mkataba ili kuwe na uhuru wa habari na nini ku-associate, haiwezekani! (Kicheko/Makofi)

Watu ambao wanafungia magazeti, leo mmefungia magazeti, mnaleta hapa turidhie Mkataba wa Afrika ili na ninyi mijulikane Rwanda na wapi kwamba wale wameridhia watazingatia uhuru na nini, haiwezekani! Ninyi hamna uwezo wa kufanya hivi, *you are wasting our time*, mnatupotezea muda kwa kutuletea turidhie Mikataba ya vitu mnavyojua hamna uwezo wa kuvitekeleza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Anayefuata Mheshimiwa Mnyika hayupo, ninamwita Mheshimiwa Peter Msigwa!

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Relax, nitakuwa mpole. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza na mimi niunge mkono hoja nzuri ambazo Kiongozi wa Upinzani ametoa maoni, ambayo ningedhani Serikali kwa ujumla wake ingeweza kuyazingatia. Niseme tu ndugu zangu, Muswada huu kama alivyosema Mheshimiwa Wenje, marihdiano haya ni ya muhimu sana na ya msingi, kwa sababu ukiyasoma yana-appeal na ndiyo msingi mkubwa wa maendeleo. Kwa bahati mbaya kama alivyosema, kwa nchi yetu na Bara zima la Afrika, hili ndiyo tatizo na ndiyo changamoto kubwa tulionayo katika continent.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla hatujaenda kwenye continent au kabla hatujaenda kwenye nchi, values na principles zinaanzia kwenye family. Unapokuwa na father una weak family, ukiwa na weak family una mtaa dhaifu. Kwa hiyo, tunapozungumzia haya masuala hayaanzii juu na ndiyo maana msemaji aliyepita, Mheshimiwa Mkosamali, anazungumzia haya masuala yana-appeal kwa sababu huku juu yanaonekana mazuri, lakini tukienda chini yanaonekana hayajakaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizungumzia suala la values, haya ni maadili ya msingi. Tukijiuliza wote kwa pamoja kabla hatujaenda kwenye makubaliano haya na nchi zingine, maadili ya msingi katika Taifa letu ni nini kama unaweza kusema. Kwa kumbukumbu zangu naona wakati wa Mwalimu kidogo kulikuwa na maadili, kulikuwa na core values za Taifa. Leo tukisimama hapa tunaposema tunaridhia haya kwenye nchi nyingine tunashirikiana,

ninaangalia katika Afrika jinsi Afrika ilivyoanguka, ni nchi mbili tu mpaka leo ambazo zimeridhia, zingine zote hazijafanya na Tanzania imekuwa ikisuasua kwa sababu kwanza, kama Taifa hatuna core value.

Values ndiyo road map ya maisha yako, unataka uende wapi, kipi unakataa na kipi unakubali, kwa sababu kwenye maisha ni lazima ujue unataka nini na hutaki nini. Kwa hiyo, haya mambo kabla hatujaenda huko mbele ni suala la kujiangalia wenyewe kwenye maofisi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi amezungumza Mheshimiwa Lissu, kwenye maridhiano haya ukiangalia tunatuma watu wanaenda kuridhia Mikataba, lakini Mheshimiwa Kombani uliyetuletea maridhiano haya kimsingi ni yapi yanatekelezwa na Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi?

Haki za binadamu zinakiukwa, uadilifu maofisini haupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilinde naona Mheshimiwa Assumpter hapa ...

MWENYEKITI: Wewe endelea kuongea na mimi, usiongee na Mjumbe, ongea na mimi.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini unilinde kidogo, naona hatulii, utadhania yeye ni Chief Whip.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni zinasema hivyo labda tunavunja Kanuni, wote tunaweza kupiga kelele tukitaka, lakini atulie.

MWEYEKITI: Ongea na Kiti, endelea.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachowenza kusema, maridhiano haya yanakuja bado tunarudia kusema hii ni *political gimmick*, mnataka mwoneshe ulimwenguni kwamba Tanzania sasa kwa sababu inaenda kwenye uchaguzi, inataka ioneckane inalinda haki za binadamu, kuna good governance, wakati haya mambo yote hayapo.

Tumeshuhudia hivi karibuni, Viongozi Wakubwa wa Vyama, Mheshimiwa Profesa Lipumba, anapigwa hadharani na huku mnasema mnaridhia mambo ya good governance, ambayo kimsingi ham-practice. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya tuna Bunge ambalo kazi yake ni kuzomea, tukienda kwenye mambo ya msingi hatusomi kwa pamoja tukaona yana faida gani. Mfano mzuri, hapa ndani ya Bunge tulipitisha Sheria ya Fire, leo Wabunge wote tunanung'unika hapa kwa sababu ya mambo ya kusema Ndiyo na kuitikia. Leo ukienda kwenye Halmashauri zetu, tumeambiwa majengo yote ya umma; kwa mfano, pale kwangu Iringa Mjini kuna shule zaidi ya 40 tunaambiwa tulipie. Wananchi wakitaka kujenga nyumba ni lazima waende Fire walipie laki mbili ambayo ina-encourage ujengaji holela, ni kwa sababu ya kuitisha mambo kama haya hovyo hovyo, kiushabiki bila kuyasoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaposoma wenzenu wamedadavua wamechukua muda. Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani ametoa vifungu vya Katiba vinavyokinzana, lakini watu bado mnazomea, hamtaki kukubali; hiyo good governance katika nchi yetu iko wapi unaweza kusimama ukajidai kwamba kuna good governance?

Wapinzani tunapigwa mabomu tunapotaka kutoa uhuru wetu wa kujieleza; hiyo good governance iko wapi? Halafu tunaenda kwenye Jumuiya za Kimataifa tunataka tuonekane sisi tuko vizuri, mnasema *look*, tunaridhia hii Mikataba wakati kimsingi katika nchi yetu hivyo vitu vyote havipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza mwanzoni kwamba ukitaka haya mambo yaende vizuri unaanzia na ngazi ya chini, *values* ni *road map*, kama hujui unakokwenda kila njia inaweza kukuchukua. Taifa letu ukienda ndani miundombinu haijatengenezwa vizuri, watu hawa hawajaandalialiwa, hawajafundishwa core values za Taifa hili ni nini mpaka tusimame hapa tunasema tunataka tuwe na *values and principles*. Sisi wenyewe kabla hatujaenda katika continent tunasimamia nini?

Ningeomba Mheshimiwa Celina Kombani, haya maswali aliyokuuliza Mheshimiwa Tundu Lissu kwenye Hotuba, tupate majibu ya kina, siyo majibu ya ubabaishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikataba mingi na Miswada mingi hapa tunaipitisha kiushabiki hatusomi. Kama mtu ana hoja, tangua hizi hoja alizozizungumza Msemaji wa Kambi ya Upinzani tuone amekosea wapi. Kimsingi, kama nilivyosema mwanzo tena, hatuanzii kule tunaanza humu ndani, hiyo good governance iko wapi, watu hizo ethics kwenye kazi ziko wapi?

Tungekuwa tunafanya hivyo, vyombo vyote viro, wamezungumza wenzangu hapa, ukienda Polisi hawasimamii sawasawa na kazi zao zinavyotakiwa. Ukienda Mahakamani hivyo hivyo, ukienda macofisini hivyo hivyo, watu hawazingatii taratibu hizo. Sisi kama Taifa tuna kipi ambacho tunakipigania ambacho tunajivunia kwamba Taifa letu tunasimamia hivi, kwa hiyo, mfanyakazi wa umma yeyote anaposimamia ofisi ya umma, hivi ndivyo tunavyosimamia na *this is what is expected from him or her*, ni yapi tunayasimamia katika nchi yetu?

Tunakuja na ngojera nyingi na kupiga kelele nyingi. Nilichotaka kusema ni ili tupate MPs wazuri, ni lazima tuwe na societies nzuri. Ili tuweze kuwasimamia Watendaji, kwa mfano, sisi Wabunge ili tuwe na haki ya kuwasimamia watendaji hata wanapoenda kwenye Mikataba hiyo, ni lazima kwanza sisi wenyewe tuwe bora, tukione hata tunachokisimamia. Mara nyingi tunapoenda huko Majimboni mpaka huwa tunaanza kushangaa, Wabunge wengine wameanza kushangaa hata hizi sheria ambazo zimeletwa kwamba zilitungwa lini wakati wote tulikuwepo hapa!

Wakati mwingine nimekutana na Watendaji mpaka wanatucheka wanasema Wabunge wa Bunge la Tanzania na Madiwani bwana wanachowenza kukosoa kwenye makabrasha wanayoleta sana sana huwa wanakosoa jina kama limekosewa na *spelling* ndiyo wanachowenza, lakini kujadili *content* hamna! Hili ndiyo jukumu letu sisi hapa tujadili *content*, madhara yake ni yapi, wapi tumeshindwa na tunatakiwa tufanye nini, tusifike hapa tufanye mambo ya funika kombe mwanaaharamu apite.

Wenzangu wamezungumza sheria hizi siyo tatizo, sheria zipo nyingi, tumeziona sheria kila mahali mmefungia kwenye makabati nyingi hazitumiki. Zipo sheria nyingi mwisho wa siku tunaishia kulindana na kuwekeana wigo tusikosoane. Sheria tulizonazo kama zingekuwa zinafanya kazi, watu wengi wangekuwa na adabu, nchi yetu ingekuwa imesonga mbele. Kinachofanya uchumi wetu ushuke chini ni kwa sababu hizi sheria hazitekelezwi na hazitekelezwi kwa sababu wale wanaopaswa kusimamia hizi sheria hawana maadili, hao wanaopaswa kusimamia kwanza wenyewe hawana *values*, kama mtu huna *core values*....

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Kengele ya pili?

MWENYEKITI: Kengele ya pili.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kengele ya kwanza hii.

MWENYEKITI: Ya pili.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Na yule aliyesoma vizuri *Assumption*? (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Ninamwita Mheshimiwa Ntukamazina atafuatiwa na Mheshimiwa Ole-Medeye.

MHE. DEOGRATIUS A. NTUKAMAZINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Nianze kwa kuunga mkono Azimio hili muhimu la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Misingi ya Kanuni za Utumishi wa Umma na Utawala Barani Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeusoma vizuri Mkataba huu na nimeusoma katika hali ya kwamba, nilikuwa Katibu Mkuu Mtumishi Mstaafu na pia *Consultant* kwa mwaka mmoja katika African Union, Addis, ambaye nilishiriki katika *transition* kutoka OAU kwenda African Union.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba huu ni mzuri na hauna masharti magumu kama alivyoeleza Mheshimiwa Tundu Lissu. Nini umuhimu wa Mkataba huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2004 tulishuhudia mabadiliko makubwa katika Muundo na Malengo ya Umoja wa Nchi Huru za Afrika. Ilikuwa ni *transition* kutoka Organization of African Unit kwenda African Union. Organization of African Unit ambayo ilianza mwaka 1963, ilijihuisha zaidi mwanzoni na ukombozi wa nchi ambazo zilikuwa bado hazijakombolewa, lakini pia kutatua migogoro katika nchi mbalimbali. Ilipokuja African Union, walibadilisha malengo wakasema msisitizo uwe kwenye *economic integration*, mtangamano wa kiuchumi. Bahati nzuri kama nilivyosema, nilishiriki katika kuwahoji au *interview* za Wakurugenzi wapya wa African Union pamoja na Senior Managers.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ushirikiano ni wa kiuchumi na tunajua uchumi unasihamiwa na kuendeshwa na Watumishi wa Umma au *Public Service* ndicho chombo muhimu ambacho kinaongoza uchumi na kusimamia uchumi, ni vizuri Kanuni na Misingi ya Utumishi wa Umma iwe inafanana katika nchi mbalimbali na hasa wakati huu ambapo tunazungumzia mambo ya *free movement of people*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika East African Community tuna protocol ya common market. Sasa hivi Watanzania wanaweza kwenda kufanya kazi Uganda au Kenya, ni vizuri wakatawaliwa na mazingira yanayofanana, Misingi na Kanuni za *Public Service* zinazofanana. Ndiyo maana ni muhimu sana kuwa na *public service* zinazofanana kwa sababu kutakuwa na *free movement of people* na ushirikiano wa kiuchumi katika nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu nyingine ambayo ninaiona, kuna nchi ambazo bado hazina misingi yoyote wala Kanuni za Utumishi wa Umma; kwa mfano, DRC Congo ni ungovernable, yaani haina misingi yoyote, haina Kanuni zozote au Central African Republic.

Tanzania tuna bahati kwamba, kuanzia mwaka 1993 tulianzisha a big reform ya *public service* na tukaboresha Kanuni za Utumishi wa Umma. Tuliweka miundo mizuri ya utumishi

(Schemes of Service), kwamba, mtu anapoingia kweye Serikali anajua atapandaje vyeo. Tukaweka miundo mizuri ya mishahara. Tukaweka maadili mazuri (*code of ethics*).

Tukaweka misingi mbalimbali na Kanuni mbalimbali. Lengo kubwa la reform yetu katika Tanzania ilikuwa ni kubadilisha *public service* kutoka chombo chenye urasimu mkubwa kuwa chombo cha kuharakisha maendeleo na siyo kikwazo cha maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema sisi hatuna shida na nchi mbalimbali, tukisharidhia Mkataba huu, nchi za DRC na nchi nyingine zitakuja kujifunza kwetu kwa sababu tumeweka system nzuri, tumeweka kanuni nzuri, lakini tuna changamoto kubwa ambayo itatufanya na sisi tuende kujifunza kutoka kwa wenzetu. Ingawa tuna mifumo mizuri ya Utumishi wa Umma, ingawa tuna Kanuni nzuri, ingawa tuna *Code of Ethics* lakini changamoto ya kwanza tuliyonayo ni *non compliance* na misingi hii! Watumishi wa Umma hawazingatii kanuni hizi ambazo tumeziweka. Hatuko makini katika ufanyaji kazi wetu. We are not serious at work! Iko laissez-faire kubwa sana. Hatujibiki ipasavyo. Tuna tatizo la uadilifu kama wenzangu walivyokwishasema. Hatuheshimu utaalamu (*professionalism*). (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna erosion ya confidentiality yaani siku hizi hakuna kutunza siri za Serikali! Siku hizi nasikia siri za Serikali zinauzwa sokoni kama njugu, *that is erosion of confidentiality*. Tunaweka maslahi yetu mbele kuliko uwajibikaji. Ajira hazizingatii merit, zimekuwa zaidi za udini na urafiki! Kwa sababu ya matatizo hayo na kutokana na Mkataba huu, itabidi tujifunze kwa wenzetu ambao wana uadilifu mkubwa, ambao bado wanazingatia *Code of Ethics* zao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mimi nikiwa Katibu Mkuu na huko zamani nyakati zetu hizo, *public service* ilikuwa based on meritocracy. Meritocracy maana yake ni kuwa na sifa, unaingia kwenye *public service* kwa sababu ya sifa, sio kwa sababu ya urafiki au udini! Siku hizi kumeingia kitu kinaitwa mediocrity yaani watu wanaajiriwa hawana sifa. Sasa Mzee kama mimi nasikitika sana. Hayo mambo itabidi tujifunze kutoka kwa wenzetu kutokana na Mkataba huo. Mkataba huu ni mzuri sana, watakuja kujifunza kwetu kwa sababu tumeweka misingi mizuri ya *public service* lakini na sisi tutajifunza kutoka kwa wenzetu ambao wana maadili kuliko sisi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika management kuna kitu tunaita Peter Principle. Peter Principle maana yake ni nini? Peter Principle maana yake, you promote somebody to his highest level of incompetence. Peter Principle ni somebody is promoted to his highest level of incompetence yaani kwa sababu ya upendeleo unampandisha cheo mtu na kumpa kazi ambayo hana uwezo nayo anakuwa ni kituko. Sasa hayo ndiyo mambo ambayo yameingia kwenye civil service yetu lakini nawahakikishia wenzangu katika Upinzani kwamba, Mkataba huu ni mzuri sana, hauna masharti magumu, tuuridhie, watakuja kujifunza kwetu na sisi tutakwenda kujifunza kwao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimalizie kwa kusema kwamba, mimi nimetoka Serikalini nazidi kujifunza maana ya mwanasiasa halisi. Mwanasiasa halisi ni mtu mwenye sura mbili; mimi sio mwanasiasa ni mtendaji wa Serikali. Hotuba ya Upinzani inanionesha jinsi Mheshimiwa Tundu Lissu pamoja na Mheshimiwa Mkosamali walivyo wanasiasa hodari lakini wajanja sana. Wao tuko pamoja kwenye Kamati ambayo alipokuja Waziri wa Utumishi tulikubaliana kabisa na kumuunga mkono lakini wanapofika hapa wanabadilika, hiyo ndiyo maana ya mwanasiasa halisi. Ahsante sana. (Makofi/Kicheko)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Ole-Medeye atafuatiwa na Mheshimiwa Jafo.

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa fursa hii uliyonipa. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha Azimio hili ili kuridhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sisemi kwamba Azimio hili limechelewa kwa sababu ninajua kabisa na ninao uzoefu kwamba kuna Mikataba ambayo imekuja kuridhiwa hapa Bungeni baada ya miaka 10 au zaidi, kwa hiyo, huu haujachelewa. Inawezekana kulikuwa na vipaumbele zaidi kuliko hiki ndiyo sababu haukufika mara baada ya kusainiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuchangia mambo yafuatayo. Kwanza niseme kwamba, naungana kabisa na Mheshimiwa Ntukamazina kusema kwamba Mkataba huu au Charter hii ni nzuri sana. Nilipopitia, bahati mbaya tumeipata leo mchana huu na hili linakuja Mezani kwako kwamba tunaomba nyaraka tunazotakiwa kuititia sisi ili tutunge sheria ama kuridhia Mikataba zitufikie mapema tuweze kuzisoma na kuzichambua ili tukifika tuweze kutoa mchango mahsus kwa ajili ya kuboresha waraka unaohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipopitia nilifikiri kwamba pengine consultant aliyeandaa Mkataba huu ni Mtanzania kwa sababu yote yaliyoainishwa humu yamo katika Sera, Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma nchini Tanzania, yote yamo. Ukienda kwenye Sera ya Utumishi wa Umma, ukienda kwenye Sheria ya Utumishi wa Umma, ukienda kwenye Kanuni za taasisi mbalimbali haya mambo yamo humo, wanayo! Tatizo kama alivyosema mwenzangu aliyetangulia kuzungumza ni utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji labda tuanze na eneo ambalo huwa ni nyeti sana katika utumishi wa umma nalo ni ajira. Tumeanzisha Sekretarieti ya Ajira, nini *impact* ya kuwepo kwa Sekretarieti ya Ajira katika kutekeleza maamuzi ya kuajiri kwa haraka na kwa ufanisi? Tumepunguza kwa kiasi gani upendeleo katika ajira? Je, *impact* hiyo imeonekana vipi katika utoaji tija na ukuaji wa uchumi wa Taifa letu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naweza nikakuhakikisha kuna Wizara ambazo ukienda leo unaweza ukakuta watu waliozaliwa tumbo moja watatu wao kwenye Idara moja au wako kwenye Wizara moja. Sasa hilo hatujengi. Utaratibu wa kuajiri ukakuta kwamba nusu ya watumishi katika Wizara ni kabilia moja ndiyo inayotuletea utamaduni mbovu katika Serikali. Tunahamisha *inefficiency* katika utamaduni wa kabilia letu kama ndiyo tumezidi pale tunaleta pale, kama ni wizi tunaleta pale. Kwa hiyo, naomba kwa Mkataba huu tunahitaji tupitie upya sheria zetu, tuanzie na Sera ya Utumishi wa Umma. Tunahitaji tupitie upya Sheria na Kanuni zilizopo ili kuendana na yaliyomo katika Mkataba huu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo katika Ibara ya 19 ya Mkataba huu, tunaelekezwa tuhakikishe kwamba katika ajira tunazingatia haki za wanawake kwa maana ya usawa wa wanawake, makabila madogo na watu wenye ulemavu. Tunapozungumzia makabila madogo, kabilia linaweza kuwa kubwa kwa maana ya wingi wa watu lakini katika utumishi wa umma ukakuta wako wawili au watatu kwa sababu ya upendeleo unaofanyika katika ajira. Akishakuwepo mmoja anawavuta wenzake ndiyo wanaoingia pale. Tuwe na utaratibu wa kugawana nafasi hizi kwa kuzingatia Wilaya na Mikoa badala ya kufanya tu ajira bila kuzingatia Watanzania wote wamewakilishwa katika Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uadilifu. Uadilifu katika utumishi wa umma hauko juu kwa kiasi cha kutosha. Jana tulipokuwa tukijadili Sheria ile ya Kuanzisha Wakala wa Dawa za Kulevyta, tulibishana hapa kwamba lazima mtu atokane na utumishi wa umma. Katika sheria zijazo, kama tunataka Askari basi tuandike pale kwamba tunataka Askari. Tusiweke blanketi kwamba tunataka mtumishi wa umma lakini tunapofika hapa tunasema, aah, tunataka mtu

awe Askari, tuseme kabisa tunataka Askari. Tuelewe ndugu zangu kwamba mimi ni Mbunge, watoto wangu wanaweza wasiwe katika utumishi wa umma lakini wanaweza wakawa ni wazalendo na waadilifu sana kuliko wale walio katika utumishi wa umma. Kwa hiyo, hili la kuanza kufungafunga tusishirikishe wengine, hapana! Nashukuru sana kwamba Mkataba huu unasisitiza juu ya haja ya wananchi kusimamia watumishi wa umma lakini watawasimamiajue kama hatutafungua milango na kuwashirikisha yale ambayo yanafanyika? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda unakwenda, lipo suala la efficiency katika matumizi ya resources, tumezungumza katika Mkataba huu. Naomba tupunguze misafara. Misafara ya viongozi inatugharimu sana, ipunguzwe, magari yapungue! Kama Rais tulishaweka vigezo kwamba ni magari tisa yawe tisa! Kama Waziri Mkuu ni magari saba yawe saba yasizidi hapo, inatugharimu kila gari moja linapoongezeka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni wajibu wa watumishi wa umma. Yako maeneo ukienda katika utumishi wa umma hupati huduma mpaka uombe na siyo kwamba uombe mpaka ubembeleze hata kwa haki yako. Mtumishi amefanya kazi na anastahili kulipwa anaambiwa hujalipwa kwa sababu hujadai. Kwa nini adai wakati kuna mtu ambaye ni wajibu wake ye ye kuandaa malipo yale na kumpatia mtumishi yule? Naomba tuhakikishe kwamba kweli tunawaijibika katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ushiriki katika sherehe. Ukipitia kwenye bajeti za Wizara mbalimbali sehemu kubwa ni ushiriki katika sherehe. Tupunguze ushiriki katika sherehe, tushiriki sherehe za sekta inayotuhusu na siyo kwenda katika kila sherehe kwa sababu ni gharama ya bure kwa Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (Makofi)

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda sana kumshukuru Mwenyezi Mungu na mimi kupata fursa kuweza kushiriki katika ajenda hii ya leo jioni. Mimi kwanza nawaomba sana Wabunge wenzangu, maana michango ya mwanzo watu walikuwa wanaona imeenda juu kweli, watu walipata moto kwelikwel! Naomba Watanzania wajue kwamba hiki ndiyo kipindi cha lala salama, kila mtu anataka atumie muda wake vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima la utawala bora maana wengine wananyooshea kidole Chama cha Mapinduzi lakini leo hii tunamuona mtu alikuwa muhimu katika Bunge hili, Mheshimiwa Zitto Kabwe alikuwa muhimu lakini amefukuzwa wakati wananchi wake wakimhitaji. (Makofi)

WABUNGE FULANI: Aaaaah!

MHE. SELEMANI S. JAFO: Lakini huko kuna utawala bora huko!

MBUNGE FULANI: Mansour mmempeleka wapi?

MHE. SELEMANI S. JAFO: Akina Hamad Rashid watu muhimu sana leo hii wanakuwa Wabunge wa Mahakama! (Makofi)

MBUNGE FULANI: Hayakuhusu hayo!

WABUNGE FULANI: Mansour.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Lakini hiyo hawaoni kama utawala bora. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niweke jukwaa sawa tu kwamba...

MBUNGE FULANI: Mchukueni ninyi!

MBUNGE FULANI: Inawauma eeh?

MHE. SELEMANI S. JAFO: Na binadamu ukiona umemkanyaaga akisema umenikanyaaga basi ujue hapo kaumia. (Makofi/Kicheko)

MBUNGE FULANI: Hamad si mmeshamchukua! (Makofi)

MBUNGE FULANI: Hayakuhusu!

MBUNGE FULANI: Inawauma eeh?

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania naona watakuwa wameshaelewa nilikuwa namaanisha nini. Nilikuwa nataka niweke jukwaa sawa kidogo. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Sawasawa.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashangaa leo ajenda hii muhimu sana imekuja, ajenda inayohusu wafanyakazi wa Tanzania. Ibara ya 16, 17 na ya 19 inazungumza haki za Watanzania hasa wanaofanya kazi katika sekta ya umma, hatutaki kwenda ndani sana kuweza kujadili kwa kina. Tutakuwa tunafanya dhuluma kubwa sana kwa watumishi wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kumshukuru Mheshimiwa Waziri, kuleta ajenda hii leo ni jambo la msingi, naomba tuelewe hilo. Tumeambiwa kuna nchi 53 lakini nchi ambazo zimesharidhia ni mbili na sisi Tanzania ni wa tatu. Hili ni jambo kubwa sana lazima tuseme kwamba tunaenda kulifanya kazi na kuiagiza Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote hapa huwa tunalalamika kwamba watumishi hawapati pesa zao za likizo, watumishi hawaendelezwi, hili ndiyo jambo la kujadili. Ina maana tunaporidhia Mkataba huu, Serikali sasa ina wajibu kuhakikisha kwamba mafao ya wafanyakazi yanasmamiwa vipi, tuweke vigezo vya kuhakikisha kwamba suala hili sisi kama Watanzania tumeridhia. Hili ni jambo la msingi lazima kusema kwamba hili leo limekuja suala muafaka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa tunazungumzia jinsi gani tutawatetea watumishi wa Tanzania, tusizungumzie ajenda za kwetu sisi wanasiwa. Tuwaangalia Watanzania hawa tunaowazungumzia, tuwatetee vipi! Hii ndiyo benchmark ya kuwatetea wafanyakazi wa Tanzania. Hatuwezi kusema tunawatetea wafanyakazi wa Tanzania bila kulipitisha hapa Bungeni, tutakuwa sisi ni wanafiki, siyo watu wa kuzungumza sawasawa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tutaipitisha document hii hapa Bungeni, tupitie vipengele vyote na kuangalia jinsi gani Serikali itajielekeza kila mwaka. Kipengele cha 17, kinazungumzia hasa mafao ya wazee, sisi Bunge hili tumefanya nini katika suala zima la mafao ya wazee? Kila mtu hapa analalamika suala la mafao ya wazee, sasa leo tukipitisha hapa maana yake tuna nafasi ya kuikaba Serikali yetu ni jinsi gani wazee wa Tanzania watapata fursa ya kuhakikisha

kwamba nchi yao inasimamia vizuri suala hili? Hilo ndiyo jukumu la Wabunge lakini tutakuwa na meno vizuri endapo tunavyoridhia kwa umoja wetu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kipengele cha corruption na hili ni jambo kubwa sana, kila mtu amezungumza katika eneo lake na ni kweli! Ni kwamba, tutakaposimamia suala zima la rushwa ndiyo tutaweza kutengeneza hata maslahi ya wafanyakazi. Mimi siku zote nasema wakati mwingine hatuendi vizuri ni kwa sababu kuna wachache sio wengi, ni wachache ambao wanafanya dhuluma kubwa sana katika nchi hii. Kuna wengine rasilimali hizi za nchi badala watumishi na watu mbalimbali waweze kunufaika kuna baadhi ya watu wachache wanafanya dhuluma kubwa sana. Kwa kupitisha document hii, tunataka tuwafahamu hao watu, Serikali iweze kusimamia na kuwachukulia hatua watu wote wanaofanya dhuluma katika rasilimali za nchi hii na hii ni commitment ambayo tunaiweka leo Bungeni. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengine wamesema, katika corruption kuna sehemu nyininge ambazo badala ya mapato kwenda Serikalini kuwasaidia Watanzania wote, kuna watu wachache wanajilimbikizia wao wenyewe. Mimi nina imani katika ajenda hii tunayoipitisha hapa leo, ina maana tunaiagiza Serikali sasa ikasimamie vizuri rasilimali zake zote, mwisho wa siku rasilimali zile ziweze kuleta manufaa kwa watumishi wa umma na Watanzania wote kwa ujumla. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 3 kuna suala zima la ajira. Azimio hili linatuelekeza kwamba ajira zisitolewe kwa upendeleo. Tumeona ukienda katika taasisi nyininge utakuta 70% taasisi hiyo imejaa watu wa kabile moja, kwa nini? Ina maana hakuna watumishi kutoka katika makabila mengine mpaka taasisi hiyo iwe na watu wa kabile moja au dini moja kwa nini? (Makofii)

MBUNGE FULANI: Sema!

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba huu sasa unasema suala la ajira lazima liangalie upana wa nchi husika. Haiwezekani kabisa! Mimi naomba niwaambie, leo hii ukienda katika taasisi nyininge utakuta kabila moja watu wamejazana mpaka mfagia chooni, wote ni kabile moja, hicho kitu hakiwezekani! (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukipitisha hii sasa maana yake ni commitment na Serikali ihakikishe kwamba inaenda kusimamia vizuri suala hili. Ni jinsi gani suala zima la ajira liwe linatawanyika bila kugusa dini zao, bila kugusa makabila yao. Mimi nashukuru sana, hata kama tumesema katika suala zima la utumishi, sasa hivi tumeshusha katika Halmashauri ili kuweza kupata vijana wa maeneo yao, naipongeza Serikali kwa hili. Vilevile nashauri siyo kushusha zile kada tatu tu au nne za watu wa chini, hata ikiwezekana watu wenye competence fulani waweze kuajiriwa na Halmashauri tutaweza kuweka wigo mpanga sana kwa sababu Halmashauri nydingi hivi sasa kuna vijana wengi wamesoma lakini wanakosa ajira kwa sababu mpaka akafanyiwe interview kwenye Sekretarieti ya Ajira, akienda kule bahati mbaya, inawezekana ukatumika utaratibu huu wa kikabila, utakuta watu wa kabile moja peke yake ndiyo wanapata kazi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuridhia kwa Mkataba huu leo, mimi naipongeza Serikali sisi tumekuwa nchi ya tatu kati ya nchi 53, lengo kubwa ni kwamba tunafanya vipi sasa tuhakikishe kila mwaka tunaweza kupima kila kipengele tumekitekeleza vipi. Nina imani katika

hili sasa litatupeleka mahali pazuri kuhakikisha kwamba watumishi wetu wanafanya kazi vizuri na kuhakikisha nchi yetu inaenda mbele. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna suala zima la kuwaendeleza wafanyakazi. Mkataba huu unaeleza kwamba wafanyakazi lazima wawezeshwe kuendelezwa ili kazi zao wazifanye vizuri. Kuna watu wengine muda mrefu sana wako Serikalini wanafanya kazi lakini hata siku moja hawajapata short course! (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kuna shirika moja linaitwa NIP (National Institute of Productivity) wanatoa kozi nzuri sana za kuwasaidia vijana na watumishi wa Serikali kujenga uwezo wao katika maeneo ya kazi. Ni jinsi gani Serikali sasa itasaidia kuhakikisha kwamba vijana wengi na watumishi wengi wa Serikali wanapelekwa katika taasisi hizi mbalimbali kwa ajili ya kujenga uwezo wao? Mimi nina imani, mtu aliyepewa training ataweza kufanya kazi vizuri kwa ajili ya kuwatumikia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho na kubwa zaidi japo tunapitisha mkataba huu leo, niwaombe wafanyakazi wote wa Tanzania amba wao ni watumishi wa umma wahakikishe kwamba sasa hivi tumepitisha Mkataba huu wana jukumu kubwa la kutekeleza wajibu wao katika maeneo yao ya kazi. Nakushukuru sana. (Makofii)

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa nampa nafasi Mheshimiwa Shekifu, Mheshimiwa Mnyaa na Mheshimiwa Chomboh.

MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwanza kukushukuru wewe lakini pia kuishukuru Serikali kwa kuleta azimio hili tuweze kuliridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika na bahati nzuri Waziri ameeleza, tuna bahati mbaya sana ya kupotosha ukweli na kuweka mambo ambayo hayana msingi, pengine kuwachanganya wananchi. Mimi nitajielekeza katika maeneo yale ambayo tunapata faida gani kama tukiingia katika Mkataba huu. Waziri ameeleza kwa uzuri sana katika ukurasa wa pili wa Azimio ni mambo gani tunapata. Pengine Watanzania niwaambie ili wasipotoshwe kama walivyoanza kupotoshwa. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuridhiwa kwa Mkataba wa msingi na Kanuni za Utumishi wa Umma na Utawala Barani Afrika ni fursa kwa Tanzania katika mambo yafuatayo:-

Kwanza, kuweka viwango katika kuendesha utumishi wa umma na kupima kwa kuangalia wenzetu wanachokifanya katika kuboresha utumishi wa umma. Huu ni mkataba wa nchi, tunaungana na wenzetu, tujifunze tupate faida hiyo.

Pili kupata misaada ya kimaendeleo kutoka washirika wa maendeleo amba watafadhilli miradi itakayotokana na utekelezaji wa mkataba huu. Nani anayekataa faida hii?

Tatu kupata tuzo za ubunifu katika utumishi wa umma zitakazokuwa zinatolewa kutokana na masuala mengi yaliyopo katika Mkataba. Tayari nchi yetu inayatekeleza masuala hayo ya sera pamoja na kanuni na taratibu. Hivi ni nani analikataa hili kwamba si faida kwa nchi yetu?

Nne, kujenga uwezo wa utumishi wa umma na taasisi zake kupambana na changamoto mbalimbali za ukuaji wa mahitaji ya kiuchumi, huduma za umma, umaskini, majanga asilia kama vile njaa na ukame, uharibifu wa mazingira, ukiukwaji wa haki za binadamu na rushwa, ni

mambo yamezungumzwa humu. Juzi tulikuwa tunatunga sheria inayohusu maafa leo tunasema tuache kuungana na wenzetu ili tunufaikie siyo busara.

La mwisho, kuimarisha utumishi wa umma katika nchi yetu kwa kuongeza ujuzi, maarifa, ubunifu, tija, ufanisi na uwezo na utendaji kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitawashangaa sana wenzetu ambao wanadandia *condemn* yaani kukataa kwamba hatuna faida katika hili. Wanachukua upungufu mdogo ambayo ni ya kawaida na Serikali yoyote hakuna Serikali timilifu, hakuna nyumba inayojengwa kwa siku moja. Afadhali sisi tuna uzoefu lakini vijana wangu hawa wanaolalamika uzoefu ni mdogo sana katika haya na haya tunayaleta kwa nia njema. Bahati nzuri wamekubali kwamba Mkataba huu ni sahihi na ni mzuri kwa hiyo hatuna ugomvi. Tumeleta sisi sasa ubaya wetu ni nini, kwa nini tugombane na kwa nini tuwapotoshe wananchi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakubaliana sana na Mheshimiwa Ntukamazina ameeleza kwamba tunao upungufu, kinachotakiwa hapa ni kurekebisha ule upungufu lakini siyo kusema hatuwezi, sasa sisi ndiyo tuliopewa dhamana ninyi mnaweza lipi? (Makofii)

MBUNGE FULANI: Hakuna wanaloweza.

MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nachozidi kushauri ni wana-CCM, babu yangu alinipa kahadithi kadogo aliniambia hivi, kuna mtu aliquwa anaoga Ziwanibahati mbaya akaja mtu akachukua nguo zake akakimbia nazo. Sasa busara ikamtuma, je, nimkimbize yule anayekimbia na nguo zangu? Hekima ikamtuma hapana baki hapo hapo Ziwanibahati msada utaletewa nguo nyingine. Wana-CCM nawaonya tuiswasikie watoto hawa, sisi tusije tukatoka katika nia yetu ya kuongoza nchi. (Makofii)

MBUNGE FULANI: Kuhusu utaratibu.

MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nachoomba na ninachosisitiza ...

MWENYEKITI: Tuwe na uvumilivu.

WABUNGE FULANI: Aaaaah!

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kidogo.

MWENYEKITI: Endelea Mheshimiwa Shekifu.

MBUNGE FULANI: Mbona wengine uliwapa.

MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Mkosamali tulia mwanangu uwe na subira.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Taarifa kwanza maana na sisi walitupa taarifa.

MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU: Ngoja atoe taarifa yake namruhusu, toa taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa Mheshimiwa Mkosamali.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa, kwanza nimpige marufuku kwamba sisi siyo watoto humu ndani. Sisi ni Wabunge tulioigaragaza CCM

kwa kura nyingi. Hakuna mtoto anayeigaragaza CCM. Tumeingia humu Kikatiba na tunasoma labda yeye ndiyo atufafanulie kuhusu ripoti ya Msema Kweli ilisemaje kuhusu Udaktari wake feki na ku-forge vyeti ndiyo maana anachangia mambo ya kurembaremba kwa sababu ana kashfa ya ku-forge vyeti. (Makofi/Kicheko)

MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kijana huyu na naendelea kumuita kijana...

WABUNGE FULANI: Sawa siyo mtoto.

MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU: Na niseme ni mtoto kwa sababu hata anayoyazungumza hayana hekima na umma wote unajua ...

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali kaa.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU: Utaratibu gani?

MHE. MOSES J. MACHALI: Ni suala la Kanuni Mwenyekiti.

MBUNGE FULANI: Mwenyekiti unapendelea.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali kaa.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni suala la utaratibu, kuhusu utaratibu.

MBUNGE FULANI: Mwenyekiti acha kupendelea.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali, naomba ukae. Tumeshakubaliana Waheshimiwa Wabunge tuvumiliane mbona mlikuwa mnasema mambo ya mauaji hapa wengine wamevumilia.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mbona umewapa CCM?

MWENYEKITI: Tuvumiliane.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu, umewapa mara ngapi, Kanuni zinavunjwa, zinakanyagwa, *be fair*, siyo kufanya mambo ya ajabu hapa tunaomba kuhusu utaratibu.

MJUMBE FULANI: Hawezi kupendelea CCM waziwazi hivi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali kaa.

MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naendelea. Naomba kuliomba Bunge lako kuvumiliana. Sisi ni watu ambao tumepewa dhamana na wananchi na kama tumepewa dhamana na wananchi unapomtukana mwenzako elewa naye anakasirika kama ninyi mnavyokasirika. (Makofi)

Suala hili kila mnapoamka mnasema CCM hamuwezi, ni jambo baya, hatuzungumzi kichama hapa. Kwa hiyo, sisi tunachokisema ni kwamba haya mema tunayoyafanya muyakubali, yale mabaya hatuyakatai tuambieni. Hujini yale ambayo mnaona katika Mkataba huu ni mabaya ni yapi. Hakuna aliyemka kati yenu aliyesema kwamba kifungu hiki na hiki hakileti tija tuweke hiki. Utendaji wa kazi ndivyo unavyotakiwa na ndiyo Upinzani lazima uwe na mawazo constructive, mmenielewa?

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Naomba Mheshimiwa Mnyaa endelea, hatuna muda wa utaratibu sasa hivi, namruhusu Mheshimiwa Mnyaa aendelee.

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwanza kwa kupata nafasi hii na nikupongeze wewe angalau kwa kuona uwiano wa vyama kwa sababu kitendo cha kwamba niliomba na nikakosa na ningekosa nafasi hii ungekuwa siyo haki, kwa hiyo, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nitambue uwepo wa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar katika Bunge hili ambaye pia ni Mbunge wa Kitope na Kiongozi wa Shughuli katika Baraza la Wawakilishi ambapo Azimio hili la Mkataba wa Msingi wa Kanuni za Utumishi wa Umma na Utawala Barani Afrika limekuja siku nzuri sana kwamba na yeye yupo. Tunapitisha mara nydingi sana Maazimio kama haya na inavyoonekana na imezoeleka yanahusu Tanzania Bara tu, hili halihusu Tanzania Bara linahusu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwemo Zanzibar. Kwa hiyo, siku ya leo kupitisha Azimio hili yumo ni vizuri sana. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, Azimio hili katika lugha ya Engineering linaleta standardization kwa nchi zote za Kiafrika kuhusu masuala ya kiutumishi na taratibu zote zile za agency na mambo mengine. Kwa hiyo, kwa lugha ya kingwini linaleta harmonization kiasi kwamba tutakuwa tunazungumza lugha moja na dunia hii yetu ya leo ambapo tuna Jumuiya ya Afrika Mashariki, tuna kanda ya SADC, tuna AU ni jambo zuri kwamba huko mbele tunakokwenda kutakuwa na kubadilishana watumishi kutoka hapa kwenda hapa kiasi kwamba ikiwa kuna harmonization, ikiwa kuna standardization ya mambo haya ya utumishi ni jambo zuri, hakutakuwa na ugeni kwamba mtu anaweza kutoka Tanzania akafanya kazi Kenya, akafanya kazi Ethiopia, akafanya kazi Nigeria na vise versa ikawa ni jambo zuri sana. Kwa hiyo, kwa kweli tupongeze Azimio hili kwa mantiki hiyo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kupongeza na kulikubali Azimio hili haimaanishi kwamba Tanzania hatuna matatizo. Kwa mujibu wa ripoti hii ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani ambayo ni sahihi sana na maelezo aliyoyleza yanahitaji kujibiwa vilivyo na Mawaziri husika na mifano kibao ipo au mifano tele kwa lugha nydingi ipo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano kuna Maazimio ambayo mpaka leo hayajaridhiwa Tanzania na ni kwa sababu fulani. Hayajaridhiwa kwa sababu hatujakubali jambo fulani. Mfano ukichukua Azimio la SADC la mambo ya uchaguzi unoitwa Mkataba wa Afrika kuhusu Chaguzi, Demokrasia na Utawala Bora (*The African Charter on Democracy, Elections and Governance*) uliopitishwa na kikao cha kawaida cha Wakuu wa nchi za Serikali za wanachama toka 2007 halijaridhiwa Tanzania kwa sababu katika Azimio lile kuna mambo ya haki ya mpiga kura na haki ya uchaguzi yanayohusiana na Tume Huru, Tanzania haipo! Yanayohusiana na mifano kibao ipo au mifano tele kwa lugha nydingi ipo. (Makofii)

popote duniani kwa vile ni Mtanzania anaweza kupiga kura huko aliko, Tanzania hayapo! Yanayohusiana na kwamba wewe leo Mtanzania unayetoka Chokocho au Mkanyageni lakini unaishi Ununio, unaishi Mafia kwa sababu za kiuchumi unataka kwenda kupiga kura Zanziabar unakatazwa, limesababisha hata Rais wa Zanzibar asijipigie kura mwenyewe kule Zanzibar uchaguzi uliopita. Haya mambo ndiyo sababu Tanzania haijariidhia Maazimio kama haya. Kwa hiyo, Tanzania ikichelewesha kuridhia Azimio ni kwa sababu hizo zitawafunga wenyewe na kuna mambo hawayataki ambayo ndiyo hayo ya utawala bora, demokrasia ya kweli, usistaajabu Mwenyekiti hilo ni kweli (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwininge contrary na nilioutoa ni kwamba Tanzania inapotaka jambo haraka haraka italetwa Azimio hilo. Kwa mfano, tumepitisha mwaka jana hapa Azimio la Postal Union, kwa nini? Ni kwa sababu tunataka Makao Makuu ijengwe Arusha, tunataka pesa ambazo zitatoka kwa nchi wanachama, tumelipitisha haraka haraka hapa. Kwa hiyo, hii tabia ya kwamba Azimio fulani tunalichewesha kwa sababu linatukwaza kwa mambo yetu tunayotaka kufanya ya kiunyanyasaji tuisililete Bungeni lakini Azimio ambalo tunalihitaji kwa haraka haraka kuna faida fulani tunalileta Bungeni, hii tabia tuiache. Nimetoa mifano miwili hii kwa makusudi ili tuache tabia hii na kama Serikali ina sababu za ukweli basi wanapowasilisha hapa Azimio lolote watueleze kwa undani sababu gani za kucheleva kuleta Azimio hilo kama hayo nayosema siyo kweli, hilo ni la pili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la tatu Article ya 14 inasema, *public service administration shall not encourage or perpetuate discrimination based on religion, race, gender, disability, religion, ethnic, political opinion or any other consideration.* Sasa hiki kipengele kwa Kiswahili kinasema katika utumishi wa umma na utawala hautahamasisha au kuendeleza ubaguzi kwa misingi ya asili, rangi, jinsia, ulemavu, dini, kabilia au misimamo ya kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikueleze kwamba Zanzibar mambo haya yapo ya ubaguzi wa namna hii na Makamu wa Pili wa Rais pale anajua na mifano iko mingi, hata hizi ajira za vikosi, kunaletwa ajira mia mbili Zanzibar Pemba wanapata watu kumi zilizobakia zote zinachukuliwa Zanzibar. Ajira leo zinakwenda kwa majina ya watu, Zanzibar na hapa Tanzania Bara na ukitaka ushahidi huo yako mashirika ya hapa unakuta ajira zinakwenda kwa majina ya watu, sasa huu ndiyo ubaguzi na *discrimination* zenyewe. Kwa hiyo, tukipitisha Azimio hili Waheshimiwa ni zuri sana kwa sababu tutaweza kuishtaki Serikali sasa kimataifa kwamba walisaini na tuliridhia Azimio hili na wanafanya huo ubaguzi. Ajira za Zanzibar zinakwenda katika ubaguzi wa kisiasa na Makamu wa Pili wa Rais yupo pale analijua hilo. Sasa leo tutakapopitisha Azimio hili litaondoa tatizo lile ambalo liliikuta Jamhuri ya Muungano wa Tanzania miaka ya 1995, 1996, 1997 ambapo tuliwekewa vikwazo hata vya watu kwenda masomoni kwa sababu ya chaguzi mbovu zinavyokwenda Zanzibar. Jamhuri ya Muungano ikawa imewekewa baadhi ya vikwazo kwa sababu ya Zanzibar. Leo tukiridhia Azimio hili nadhani mtakuwa ma-referee wa kuwaambia wenzeni wa Zanzibar, hiyo Serikali ya CCM iliyoko Zanzibar kwamba wafuate utaratibu wa utawala bora na waache ubaguzi. Jambo hili ni zuri na mimi niwaombe Waheshimiwa Wabunge tukubali, tupitishe, turidhie Azimio hili ili hawa wajifunge na sasa tupate kuwashtaki katika Jumuia ya kimataifa ambapo matatizo yatatuliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache nashukuru sana kwa kunipa nafasi na nadhani nimeelewaka vizuri sana, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Chomboh.

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili name nichangie katika hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja na ... (Makofi)

MBUNGE FULANI: Asilimia 70 ya waajiriwa ni CUF.

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Na natangulia kusema kwamba nimefurahi kweli kama alivyotangulia kusema Mheshimiwa Mnyaa kwamba leo Makamu wa Rais yuko hapa na pia kusema Mkataba huu na Zanzibar ni vizuri ukatumika. Ameona umuhimu wa mambo ambayo huwa yanaamuliwa hapa na yanahu Zanzibar ambayo wakati mwingine yeye huwa anaweka vikwazo. Juzi yeye aliweka kikwazo kwa Sheria ile ya *Immigration* kwa kusema kwamba lazima ipitishwe kwa two *third* sijui na hii atataka kuwe na two *third* katika kuridhia ili na Zanzibar itumike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachotaka kusema Mkataba huu madhumuni yake au lengo kubwa ni kwamba watumishi wa umma wawe na uadilifu, wawe na weledi, wawe na uwajibikaji ili kuleta maslahi mazuri katika Taifa letu na Afrika kwa ujumla. Kweli tuna tatizo moja kubwa sana la wafanyakazi, naona ndugu yangu Mnyaa anatoka, ningefurahi angekuwepo...

MBUNGE FULANI: Sema tu.

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Kwa kuwa Waafrika hasa Tanzania tuna matatizo makubwa sana ya uwajibikaji na tukiridhia Mkataba huu ni kweli Serikali itakuwa ina nyezo za kuwawajibisha wale wafanyakazi ambao hawawajibiki katika majukumu yao ya kila siku na hilo ndio tatizo tulilokuwa nao. Watu wengi sana wakishaajiriwa kazini anajijua yeye sasa hivi kwake ni kupokea mshahara tu lakini wajibu wao hawatekelezi kulingana na maslahi yale wanayopewa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haina chombo cha kuweza kuwawajibisha ipasavyo kwa sababu hakuna uwezekano au sijui hakuna chombo cha kuweza kufuatilia ule uwajibikaji wao, wao kubwa zaidi wanaunda vyama vya kuweza kudai haki zao lakini hakuna chama cha kuweza kuhoji na wajibu wao pia katika ile ambayo wanaidai. Kwa hiyo, kwa kuridhia Mkataba huu, Serikali itakuwa ina nyenzo kubwa sana ya kuweza kuwasimamia na kuwawajibisha wale wafanyakazi ambao hawatimizi majukumu yao kwa mujibu wa mikataba ya kazi zao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo amezungumzia Ndugu yangu Mnyaa hapa kuhusiana na ubaguzi wa ajira kule kwetu Zanzibar, ni kweli nakubaliana naye. Kwa taarifa za uhakika asilimia 70 wafanyakazi wa Zanzibar ni watu wa kutoka kisiwa cha Pemba-CUF. Asilimia 70, hilo ni kweli na halikuanza jana. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Uwongo.

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Hilo lilianza toka Mheshimiwa Seif Sharif Hamad alipokuwa Chief Minister.

MBUNGE FULANI: Uwongo.

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Ilikuwa anayechaguliwa kwenda kusoma kwa ajili ya kupata ajira, anayekaa kutoka Pemba, atatoka Mpemba, anayetoka Zanzibar atakuwa ni mtu mwenye asili ya Pemba, kwa makusudi. (Makofi)

WABUNGE FULANI: Uwongo huo.

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Nakupeni historia na Mheshimiwa Aboud Jumbe alivyomuona anapitisha akamfukuza kazi. Akamfukuza kazi kwa matatizo hayohayo, sisi ndiyo Wazanzibar tunaojua.

MHE. HOROUB MUHAMMED SHAMIS: Kuhusu utaratibu Mheshimiwa Mwenyekiti.

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Nalizungumza hili kwa uhakika ubaguzi upo na kweli Makamu wa Rais hili jambo lazima ukalifuatilie.

MBUNGE FULANI: Uwongo.

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Mimi nazungumza hivyo kwa sababu nimefanya kazi Serikalini Zanzibar...

(Hapa baadhi ya Wabunge wa Chama cha Wananchi CUF walikuwa wamesimama)

MWENYEKITI: Naomba mkae.

MHE. HOROUB MUHAMMED SHAMIS: Utaratibu Mwenyekiti.

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Na najua na naelewa ...

MHE. HOROUB MUHAMMED SHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni za Bunge haziruhusu mtu kusema uwongo ndani ya Bunge alete ushahidi.

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Na wakati huo wakati ajira zinatolewa nilikuwa nafahamu kweli yalikuwa yanatendeka.

MHE. HOROUB MUHAMMED SHAMIS: Alete ushahidi wa haya anayoyasema.

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Na siyo ubaguzi wa kazi tu, kuna ubaguzi mpaka wa kwenda kusoma vyuo vikuu.

MHE. HOROUB MUHAMMED SHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu, utaratibu.

WABUNGE FULANI: Mwongo!

(Hapa baadhi ya Wabunge wa Chama cha Wananchi CUF walikuwa wamesimama)

MWENYEKITI: Naomba mkae.

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Ni kweli ubaguzi upo si leo, si jana, si juzi. Kwa hiyo, Mkataba huu ukipidhiwa hapa ni kweli ukatumike na Zanzibar...

(Hapa baadhi ya Wabunge wa Chama cha Wananchi CUF walikuwa wamesimama)

MWENYEKITI: Waheshimiwa naomba mkae.

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Mimi nakubaliana nao.

WABUNGE FULANI: Mwongo!

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ninayozungumza si ya kubuni, ni ya uhakika, ninayazungumza kwa kujua, mimi nimeajiriwa na nimefanya kazi Serikalini. Mimi nawafahamu wanaozungumza hao, zaidi ya miaka 40 ya maisha yangu nimekaa nao, nawajua nje na ndani hao, hawanidanganyi...

MBUNGE FULANI: Kuhusu utaratibu.

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Na yule bwana alitoka kwa sababu anajua ninachokizungumza kitamshika yeye. (Makofii)

MBUNGE FULANI: Uwongo.

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Kwa hiyo, Mkataba huu nakubaliana nao na turidhie hapa na ni kweli na Baraza la Wawakilishi liupokee kwa ajili ya kutumika Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. (Makofii)

MBUNGE FULANI: Utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa naomba ukae, hatuna muda naomba ukae.

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mwongozo wa Mwenyekiti.

MBUNGE FULANI: Amemtaja.

MWENYEKITI: Waheshimiwa, tumeshaomba uvumilivu...

WABUNGE FULANI: Aaaah!

MWENYEKITI: Naomba tuvumiliane. Mheshimiwa Mnyaa, naomba ukae.

WABUNGE FULANI: Aaaah!

MWENYEKITI: Naomba sasa nimuite Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Prof. Mwandosya.

WABUNGE FULANI: Aaaah!

WAZIRI ASIYEKUWA NA WIZARA MAALUM (KAIMU KIONGOZI WA SHUGHULI ZA SERIKALINI BUNGENI): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ingawa umeniita Naibu Waziri Mkuu lakini ile...

MWENYEKITI: Kaimu Mheshimiwa.

WAZIRI ASIYEKUWA NA WIZARA MAALUM (KAIMU KIONGOZI WA SHUGHULI ZA SERIKALINI BUNGENI): Barua niliyopata ilisema Kaimu Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni.

MWENYEKITI: Nimesahihisha Kaimu wa Shughuli za Serikali Bungeni.

WAZIRI ASIYEKUWA NA WIZARA MAALUM (KAIMU KIONGOZI WA SHUGHULI ZA SERIKALINI BUNGENI): Hata hivyo, nakushukuru kwa kunitakia baraka. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikiliza kwa makini sana mchango wa Waheshimiwa Wabunge. Jana na asubuhi leo tulikuwa na mijadala mikali lakini ilikuwa mizuri na yenye faida na tulikaa kama watu ambao tunatunga sheria na nadhani waliokuwa wanatutazama huko walisema Bunge limetulia linafanya kazi. Jioni hii hali ya hewa ikabadilika lakini ndivyo Mabunge inabidi yawe. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mabunge yana misingi na misingi ni jamii. Siyo lazima Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lifanane kwa vurugu na kwa kelele kama liliyo Bunge la India kwa sababu tunatoka katika jamii tofauti sana. Jamii ya Kiafrika ni jamii ya kuheshimiana, ni jamii ya kusikilizana, ni jamii ambayo watu walikaa chini ya mti katika kijiji wazee na vijana waliiwtwa na akinamama kulikuwa na kesi lakini walikubaliana wakakaa hata saa tano na mwishoni wakakubaliana na wakaamua mambo yao na ndiyo misingi ya demokrasia ya Kiafrika, unaweza kuita African democracy. Kwa hiyo, hii tunayoiona hapa nadhani ndiyo ile ambayo tunajaribu kuangalia wenzetu wanafanya nini na sisi kuiga na kusema basi tuifanye sasa iwe demokrasia ya Kiafrika, sidhani! Ni mfano ambao siyo mzuri kwa wale wanaotuangalia wala kile kizazi ambacho kitafuata. Hata wale watoto ambao wanakuja hapa kuangalia Bunge wakati mwininge bila shaka wanasema alalah na sisi tukukua ndiyo tutakuwa hivyo. Nadhani wao pia wanasema mbona sisi afadhali katika mijadala yetu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ni vyema tukavumiliana na hili ndiyo nilitaka kulisema. Nalisema hilo kwa sababu jana na juzi kulitokea jitihada za kupunguza heshima ya Mwanasheria Mkuu au mchango wa Mwanasheria Mkuu. Mara nyininge Mbunge anatokea anamwambia kaa chini Mwanasheria Mkuu, wewe siyo mshauri wetu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza kwa sababu wakati mwininge anayezungumza hivyo ni Mwanasheria. Mimi ni Mhandisi lakini najaribu kupitia sheria na humu ndani ni wajibu wangu kusaidia katika utungaji wa sheria kama Mbunge na naelewa wajibu wa Mwanasheria Mkuu, si humu isipokuwa dunia nzima katika Mabunge yote na katika Serikali zote. Tumezoeana nao lakini sehemu zote duniani hawa ni watu wa kutetemesha, hawa ni watu wa kuheshimika, hawa ni watu ambao hata viongozi wa nchi wanawategemea kwa ushauri wao. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaposema hamna mtu ambaye yuko juu ya sheria unaweza kusema chini ya sheria yuko Mwanasheria Mkuu. Kama kipimo juu na chini basi pale chini yupo Mwanasheria Mkuu wengine wote anatusaidia kuelewa sheria. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nieleze umuhimu wa Mwanasheria Mkuu na huyu si Mwanasheria Mkuu Mshauri wa Serikali, mimi naomba kusema kwamba huyu ni Mwanasheria Mshauri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mihimili mitatu ya Mahakama, mihimili wa utawala na mihimili wa Bunge. Kati yetu labda ni Rais tu ambaye anahusika na mihimili yote, wa pili ni Mwanasheria Mkuu na nitasema anahusikaje. Katiba inamruhusu kwenda kwenye Mahakama yoyote nchini. Wewe kama Mbunge huwezi na mtendaji katika Serikali hawezo, yeye ana mamlaka hayo Kikatiba, kwa kesi zote za jinai anaweza Mahakama yoyote kuanzia chini mpaka juu. Anaendesha mashauri ya madai kwa niaba ya Serikali, kwa niaba ya Bunge, yaani mihimili wa Bunge, kwa niaba vilevile ya mihimili wa Mahakama. Mambo yote ya madai katika mihimili yote mitatu anayesimamia ni Mwanasheria Mkuu. Vilevile kwa upande wa Mahakama anashiriki katika uteuzi wa Majaji na watumishi wa ngazi ya juu wa Mahakama, hamna mwininge mwenye nafasi ya namna hiyo katika mihimili huo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa Bungeni, haya tunasema kwamba ni mshauri wa Serikali lakini humu ndani ya Bunge, juzi tulikuwa tunamsikia Mwanasheria mmoja anasema sisi Bungeni hapa tuna Mwanasheria wetu, huyo Mwanasheria haruhusiwi kuingia wala kukanyaga humu. Siku zote Mwanasheria Mkuu wa Serikali amechukua nafasi ya kulishauri Bunge.

WABUNGU FULANI: Aaaah!

WAZIRI ASIYEKUWA NA WIZARA MAALUM (KAIMU KIONGOZI WA SHUGHULI ZA SERIKALINI BUNGENI): Hiyo ndiyo imekuwa tradition na tunamsikia yaani ukisimama wewe, nikisimama mimi na akisimama yeye hawatanisikiliza mimi katika kufafanua sheria wala hatutakusikiliza wewe, atakayesikilizwa ni Mwanasheria Mkuu. (Makofij)

WABUNGE FULANI: Aaaah!

WAZIRI ASIYEKUWA NA WIZARA MAALUM (KAIMU KIONGOZI WA SHUGHULI ZA SERIKALINI BUNGENI): Mheshimiwa Mwenyekiti, twende lingine ambalo tunahusika nalo sisi kama Wabunge, kama Wabunge uhusiano wetu na Mwanasheria Mkuu. Hapa tunaringa kwa sababu tayari tumeshapita uchaguzi na tumeshaapa na tumeendelea na karibu tunamaliza. Nawarudisha nyuma miaka minne iliyopita, kesi za madai, *election petition*, anayemsimamia Mbunge katika Mahakama, anayeunganishwa na Mbunge ni Mwanasheria Mkuu. Sasa leo hii unakuja kusema Mwanasheria Mkuu hatufai, ndiye aliyekusaidia kushinda kesi zote za uchaguzi, kwa hiyo, lazima tuheshimu ngazi hii. Kwa upande wa Serikali hiyo ndiyo siwezi kusema tena kwa sababu kazi zake ni nyingi zaidi. Yeye anatushauri mambo yote ya Katiba na Sheria, anaendesha mashauri ya jinai kwa niaba ya Serikali na mambo mengine mengi. Kwa hiyo, nadhani ni kuheshimiana tu katika masuala haya. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme tu kwamba labda ni vyema tutakubaliana kwamba watu huko nje wanatuita Waheshimiwa mimi nimeorodhesha mambo kumi wanayotutegemea sisi kwa nini wanafikiri ni Waheshimiwa. Wanatuita Waheshimiwa kwa sababu wanategemea na wanatarajia tutaheshimiana.

MBUNGE FULANI: Sawa kabisa.

WAZIRI ASIYEKUWA NA WIZARA MAALUM (KAIMU KIONGOZI WA SHUGHULI ZA SERIKALINI BUNGENI): Halafu wana matarajio kwamba katika yale mambo muhimu tutakubaliana.

MBUNGE FULANI: Sawa kabisa.

WAZIRI ASIYEKUWA NA WIZARA MAALUM (KAIMU KIONGOZI WA SHUGHULI ZA SERIKALINI BUNGENI): Halafu wanajua kwamba katika mambo mengine tutakubaliana kutokubaliana. Vilevile wanajua kwamba hawa watu wataheshimu Kanuni zao. Pia wanatutegemea sana kwamba tutatumia lugha yenyе staha. Wanatutegemea tutavumili ana wanategemea kwamba hoja zetu zikishindwa tutakubali kushindwa. Vilevile na sisi au wale wanaoshinda wawe wanyenyekevu katika ushindi (*humiliate in success*). Halafu mwisho ni kwamba itakuwa jambo baya sana kama wananchi wanasema kipindi cha Bunge kimefika twende tukaangalie igizo la Bunge, comedy ya Bunge linatupunguzia sana heshima, kwa hiyo, tusilifikishe Bunge hapo. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimegongewa kengele ya kwanza, nilitaka kuchangia kuhusu masuala mengine yanayohusu Muswada huu lakini nadhani nitapata nafasi ya kuchangia kwa

njia moja au nyine. Naomba niishie hapo, Muswada huu unahu utawala bora na yote niliyoyazungumza yanahu utawala bora. Muswada huu unahu masuala yote ambayo sisi tumeyazingatia katika Katiba Inayopendekezwa. Wala hatukuusoma, kumbe wenzetu duniani nao wanafanya mambo haya, sisi hatukuusoma lakini mambo yote yamo katika Katiba Inayopendekezwa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitaka tu kumalizia na moja ambalo nadhani Mheshimiwa Mkosamali kwa faida yako ni kwamba suala la kuzuia na kupambana na rushwa sasa kwa mara ya kwanza linaingizwa katika Katiba, limo katika Katiba Inayopendekezwa, kwa hiyo, hilo si hoja tena. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa hili na mimi nimefaidika. Jana nilihudhuria kikao cha Kamati moja na Afisa Mtendaji Mkuu aliyebla katika Kamati akasema fedha hazitoshii kwa hiyo hatuwezi kutekeleza mambo haya na haya. Leo nakuja kumsikia Ndugu yangu Mkosamali anaaja hapa anasema Serikali ya CCM, hamtoi fedha, fedha zinatolewa na Bunge na wewe mwenyewe ni Mbunge. Ndiyo maana hatukaguliwi, nimeshatoa na siri nani aliyesema na wale walisema hawawezi kukagua, wanakagua kwa sampling. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na Waheshimiwa Wabunge nawashukuru kwa kuniskiliza. (Makof)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunakushukuru sana Mheshimiwa. Mimi nimeshakaguliwa, kwa hiyo, mimi niko kati ya wale waliokaguliwa. Naomba sasa nimuite mtoho hoja, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwashukuru Waheshimiwa wote waliochangia kwa njia moja au nyine katika kuridhia mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyine watu wanapenda kuchangia lakini pengine hawajajiandaa. Mimi naomba tu yule ambaye hajajiandaa ni vyema akaacha badala ya ku-fumble-fumble kwenye kitu ambacho hana uhakika nacho. Kwa hiyo, ni vyema wakapewa nafasi wale amba pengine wamesoma hicho kitu badala ya wale amba hawakusoma badala yake wana heat around the bush.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba huu ni Misingi na Kanuni ya Utumishi wa Umma na Utawala Barani Afrika. Kwa hiyo, waliosema kwamba mbona kuna mikataba mingine kwa mfano ule wa uchaguzi, haupo, huo utakuja kwa wakati muafaka. Kwa hiyo, mkataba huu umekuja kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ndugu yangu wa Kambi ya Upinzani amesema kwa hisia kali kama kawaida yake. Yeye amesema kwamba Mkataba huu umechelewa, ni kweli umechelewa na una sababu. Kila Mkataba ili uridhiwe unapita procedure mbalimbali, Waheshimiwa Wabunge lazima tufahamu. Lazima upite Serikalini na Serikalini lazima Makatibu Wakuu wauone kwenye kikao chao cha IMTC wajiridhishe, Wanasheria wauone wajirishie na mwisho Baraza la Mawaziri lazima liuone na kuuridhia ndipo uje Bungeni. Kwa hiyo, kuridhia Mkataba hauna tofauti na Miswada mingine. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge naomba hilo tulifahamu, kwa hiyo, kuchelewa kwake ni kujiridhisha. (Makof)

Mheshimiwa Tundu Lissu aliposema kwamba hawajasoma sijui Ibara ya Katiba, yeye inaonekana ndiye hajasoma, sisi katika Serikali nzima tumeupitia, Wanasheria wameupitia ndiyo maana tumeuleta hapa. Hatuwezi tukaleta kitu ambacho wenye hatujaridhika na

hatujajiridhisha. Ndiyo maana tumesema Mkataba huu haujakinzana na Katiba ya nchi na Sheria za nchi wala Kanuni na taratibu za nchi hii. Mheshimiwa Tundu Lissu alivyo sema kwamba zinakinzana, kwa kweli hiyo ni hoja yake na ni uwongo, sisi Serikalini tume pitia katika hatua zote na tumeridhika na haujakinzana na kifungu chochote cha Katiba wala Kanuni za nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zilizoridhia, napenda kutoa taarifa kwamba mpaka tarehe 30 Juni, 2014 ni nchi nne ambazo ni Algeria, Kenya, Mauritius na Namibia. Nchi nyiningine ni utaratibu wa kawaida tu, hawawezi wakachukua tu Mkataba wakaridhia bila kupitia kanuni, sheria na taratibu zao. Kwa hiyo, hatuwezi kuwasemea nchi nyiningine bali mimi nimeleta hapa naisemea nchi yangu, wengine lazima wafuate taratibu za nchi yao. Hivyo, wengine wataridhia kwa wakati muafaka na lazima pia wafuate taratibu za nchi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani pia wamesema kwamba Mkataba huu umeletwa sasa hivi ni sababu za kisiasa. Mtu aliyesoma *between the lines* kwenye Mkataba huu anaona kabisa kwamba ni wa msingi sana, hauna siasa ndani yake bali ni Kanuni za Utumishi. Pia sisi katika Sheria zetu za Utumishi wa Umma tumegusa baadhi ya sehemu nyangi sana katika Mkataba huu na tumeshatekeleza mambo mengi sana katika Mkataba huu. Kwa hiyo, hauna sura yoyote ya kisiasa bali ni wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kusaini bila kuweka masharti yoyote, nimesema umepita katika hatua mbalimbali na hatukuwa na shaka yoyote na ndiyo maana tumeuleta katika Bunge hili kwa sababu haukinzani na Katiba, Sheria na Kanuni na taratibu za nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani pia imesema kwamba kuna Muswada au Marekebisho ya Sheria yanayokuja. Mimi naomba tuiswahishe mada, tungoje huo Muswada au Marekebisho ya Sheria yatakapokuja hapo ndiyo tu-argue kesi zetu kwamba kuna *conflict of interest* na vitu kama hivyo, tuiswahishe mada kabla ya siku zake. Tumeona kabisa *miscellaneous amendment* ipo kwenye ratiba zetu za Bunge, kwa hiyo, tungoje ili tuweze ku-argue siku hiyo ambapo itakuja.

Mheshimiwa Ezekia Wenje, mimi nimshukuru tu kwamba yeye amesoma, ameelewa na aling'ang'ania sehemu moja ya uadilifu. Kuhusu uadilifu ni mimi, wewe na jamii kwa ujumla. Kwa hiyo, siyo suala la kunyoo sheana kidole bali ni sisi wote tunatakiwa tuwe waaminifu, waadilifu kwa nchi yetu na kwa Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Felix Mkosamali, nafikiri hakuusoma Mkataba huu kwa undani ndiyo maana alikuwa anapigapiga maneno, nafikiri ameshajibwa na wenzangu.

Mheshimiwa Mch. Peter Msigwa, ni kati ya wale ambao hawakusoma, kwa hiyo ni kati ya wale ambao wamepiga porojo.

Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina, ameusoma Mkataba huu vizuri ndiyo maana ameelezea umuhimu wake halafu akaweka changamoto ambazo zipo. Mimi nikushukuru sana Mheshimiwa Ntukamazina, ni kweli utumishi wa umma ukisimama vizuri ndiyo unaosimamia uchumi na uchumi wetu utakuwa vizuri sana iwapo utakuwa na maadili, utazingatia utawala bora, utazingatia *ethics* na kadhalika. Changamoto hizi ndizo tunazotaka kuzifanyia kazi kwamba baada ya kuridhia Mkataba huu tutaangalia ni sehemu zipi ambazo sisi kama nchi hatujatekeleza ili tuzifanyie kazi, tuweze kuwa sawa na wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli wengi wameshakuja kuangalia katika nchi yetu, mimi ni mmojawapo ambaye nimealikwa katika nchi mbalimbali za Afrika tukawasaidie kutengeneza miundo na mifumo katika nchi mbalimbali ambazo pengine zimetoka katika vita na nyiningine

zinataka tu kupata ile miongozo mbalimbali ambayo inatolewa na nchi yetu. Kwa hiyo, sisi tunaweza tukawa na upungufu tunaenda kuchota kwa wenzetu na wenzetu wanaweza wakawa na upungufu wanakuja kusoma kwetu.

Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye, nakushukuru pia umesema kwamba tuangalie sheria na taratibu zilizopo za utumishi wa umma, nyininge zimepitwa na wakati. Mimi nasema tukiridhia Mkataba huu ni kweli tuna-review Sheria yetu ya Utumishi wa Umma ili iweze kuendana na Mkataba huu na mambo mengine ambayo yamepitwa na wakati kwa sababu sasa hivi ni wakati tofauti ukilinganisha na wakati sheria zetu zinatungwa mwaka 2008/2009. Kwa hiyo, tunataka tuiangalie ile Sheria ya Utumishi wa Umma tuingize baadhi ya mambo ambayo yapo katika Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amesoma ile Ibara ya 19 ni kweli kwamba ajira zisikandamize wanawake, makabila madogo madogo na walemaru, hilo nalo tutalizingatia. Kikubwa kinachoingatiwa kwenye ajira ni sifa za mtu, linaweza likawa kabila kubwa sana lakini pengine wengi hawakuenda shule na hawana sifa. Kwa hiyo, huwezi ukamchukua tu kwa sababu ya kabila lake bali tunaangalia zaidi sifa za huyo mtumishi husika. Hivyo, ukisema kwamba twende huko kwenye makabila itakuwa ngumu sana na pale anapo-apply hatumuambii aindike yeye ni kabila gani na kadhalika, hata kwenye fomu siku hizi hatuangalii vitu kama hivi, tunaangalia tu ule uwezo wa mtu. Hata hivyo, sasa hivi makabila mengi wamesoma. Mimi sidhani kama kuna kabila lolote Tanzania ambao hawajaenda shule na uanzishwaji wa shule za kata umesaidia kiasi kikubwa sana kufanya makabila mengi Tanzania wawe wameenda shule.

Mheshimiwa Selemani Jafo, yeye ameangalia Article 17 na 19, ni kweli zinatetea wafanyakazi. Kwa hiyo, sheria hii ikipita tutaziangalia hizi articles kuhakikisha kwamba tunaweza tukaziweka vipi katika sheria zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la rushwa wengi mmelizungumzia, mimi niseme kwamba suala la rushwa kwa Tanzania limeshughulikiwa sana. Tukiangalia TAKUKURU imefanya kazi nzuri, wale amba wanabeza kazi ya TAKUKURU mimi nasema kwamba wanafanya kazi. Mtu yejote au taasisi yoyote ina upungufu wake lakini kwa kazi wanafanya kazi nzuri na wanatuwakilisha vizuri sana na ndiyo maana wanajulikana Kitaifa na Kimataifa, wanashika nyadhifa mbalimbali kutokana na umahiri wao wa kufanya kazi.

Ndugu yangu Rukia Kassim Ahmed, amesema kwamba hakuna utawala bora katika nchi hii. Mimi nasema utawala bora upo ndiyo maana tupo, ndiyo maana iko Wizara inayoshughulika na mambo ya Utawala Bora. Yote hayo ni katika kuhakikisha kwamba tunakuwa na utawala bora. Open Government Partnership tunajulikana Kimataifa na Kikanda kwa sababu ya Utawala Bora, transparency katika nchi yetu.

Mheshimiwa Dkt. Henry D. Shekifu, yeye amezitaja faida ambazo ziko katika Mkataba huu. Mimi ninamshukuru sana lakini pia ameangalia na upungufu. Mimi nasema kwamba tukisharidhia Mkataba huu tutaangalia mazingira yetu ili tuweze kuingiza sheria hizo kulingana na mazingira yetu na kweli tutakuwa tunabadilishana uzoefu na wenzetu ili tuweze kuendana na hizo sheria ambazo zinaweza zika-guide nchi zote za Afrika. Kama alivyosema mwenzangu mmoja kwamba, sasa hivi kuna free movement of labour, kwa hiyo, tukiwa na sheria ambazo ni common at least zitasaidia katika kuleta harmonization kwenye free market of labour.

Mheshimiwa Eng. Mohammed Habibu Mnyaa naye ameanza vizuri kwa kweli, lakini amelia kwa nini tunaridhia mikataba mingine, mingine tunaifinyafinya. Mimi nasema suala la

Nakala ya Mtandao (Online Document)

mikataba mingine, Mkataba wa Uchaguzi utaletwa kwa wakati muafaka. Sasa hivi tupitishe hili wakati muafaka ukifika Mkataba huu unaohusu Uchaguzi utaletwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Tume Huru, nafikiri angebaki kwenye Bunge la Katiba, hilo angelizungumzia vizuri na limo katika Katiba Inayopendekezwa. Mimi namwoba tu aweze kulipitisha suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema kidogo kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni Serikali ya CCM, lakini mimi ninavyojua Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Makamu wa Kwanza Rais, Mheshimiwa Maalim Seif ni wa CUF, Mawaziri na Naibu Waziri ni wa CUF. Kwa kama Serikali ya Zanzibar ni mbovu ina maana ubovu huo unaletwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa na siyo Serikali ya Chama cha Mapinduzi. (Makofi)

Mheshimiwa Muhammad Amour Chomboh, matatizo ya uwajibikaji, ni kweli changamoto zipo na changamoto hizi tunazifanya kazi. Tukisharidhia Mkataba huu tutaangalia sheria zetu tuweze ku-*fit in* sehemu zile ambazo tunaona kwamba uwajibikaji ni tatizo. Ni kweli baadhi ya sehemu uwajibikaji ni tatizo na hakuna chombo maalum kinachosimamia suala hili la uwajibikaji. Kwa hiyo, mimi nikuombe tu Mheshimiwa Chomboh kwamba hizo changamoto tutazifanya kazi ili ziweze kuendana na matakwa ya sheria, taratibu na kanuni za nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba Bunge lako Tukufu liridhie Mkataba wa Msingi na Kanuni za Utumishi wa Umma na Utawala Barani Afrika (*The African Charter on Values and Principles of Public Service and Administration*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa)

(Azimio la Mkataba wa Msingi na Kanuni za Utumishi wa Umma na Utawala Barani Afrika la mwaka 2011 Liliridhiwa na Bunge)

MWENYEKITI: Wote wamekubali, kwa hiyo, Bunge hili tumeridhia Mkataba huu muhimu kwetu na naipongeza sana Serikali kwa sababu kama yaliyomo ndani yatazingatiwa basi tutakuwa tumepiga hatua muhimu sana. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tunazungumzia utawala bora, tunatakiwa hata mambo tunayozungumza yafanane na utawala bora. Mimi nimemuacha tu Mheshimiwa Machali, kwa ujumbe alioniletea hapa ningekuwa nafuata misingi ya utawala bora, basi tuzungumze yale ambayo ni muhimu. Mimi nimekusamehe bure, message uliyoleta hapa Mezani nimeiacha.

Waheshimiwa Wabunge, tulikuwa na hoja hiyo moja tu kwa leo, mengine yatakuwa kesho, kuridhia Azimio la Mto Nile. Sasa naahirisha Bunge mpaka kesho asubuhi saa tatu.

(Saa 01.33 Usiku Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,
Tarehe 26 Machi, 2015, Saa Tatu Asubuhi)

